




KIMEPIGWACHAPA NA MPIGACHAPA MKUU WA SERIKALI, DODOMA-TANZANIA

www.nishati.go.tz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI MHESHIMIWA DEOGRATIUS JOHN NDEJEMBI (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2026/27





**DODOMA** **APRILI, 2026**



Waziri wa Nishati Mhe. Deogratius Ndejembi (Mb.), akikagua mradi wa uchimbaji wa visima vitatu kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa gesi asilia katika Kitalu cha Mnazi Bay mkoani Mtwara.



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Salome Makamba (Mb.), akizindua mfumo wa nishati safi ya kupikia katika Shule ya Msingi Bunge, jijini Dar es Salaam.




Katibu Mkuu Wizara ya Nishati (Umeme na Nishati Jadidifu), Mha. Felchesmi Mramba akizindua matumizi ya gari la umeme nchini ambalo matumizi yake ni nafuu kwa takriban asilimia 85 ikilinganishwa na gari linalotumia petroli au dizeli.



Katibu Mkuu Wizara ya Nishati (Mafuta na Gesi Asilia), Dkt. James Mataragio akikagua shughuli za utafiti wa mafuta na gesi asilia katika Kitalu cha Eyasi-Wembere.

# HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI MHESHIMIWA DEOGRATIUS JOHN NDEJEMBI (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2026/27

# VIONGOZI WA WIZARA YA NISHATI



Mhe. Deogratius John Ndejembi (Mb.),
Waziri wa Nishati



Mhe. Salome Wycliffe Makamba (Mb.),
Naibu Waziri wa Nishati



Mha. Felchesmi Jossen Mramba
Katibu Mkuu Wizara ya Nishati
(Umeme na Nishati Jadidifu)



Dkt. James Peter Mataragio
Katibu Mkuu Wizara ya Nishati
(Mafuta na Gesi Asilia)

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AfDB | African Development Bank |
| BADEA | Arab Bank for Economic Development in Africa |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| CMS | Corporate Management System |
| *COP* | Conference of the Parties |
| CSR | Corporate Social Responsibility |
| EAC | East African Community |
| EACOP | East African Crude Oil Pipeline |
| ETDCO | Electrical Transmission Distribution Construction and Maintenance Company |
| EWURA | Energy and Water Utilities Regulatory Authority |
| ESIA | Environmental and Social Impact Assessment |
| GN | Government Notice |
| GRMF | Geothermal Risk Mitigation Facility |
| JNHPP | Julius Nyerere Hydro Power Project |
| KOJ | Kurasini Oil Jet |
| KV | Kilovolts |
| LNG | Liquefied Natural Gas |
| LPG | Liquefied Petroleum Gas |
| MoU | Memorandum of Understanding |
| MPSA | Model Production Sharing Agreement |
| MW | Megawatt |
| NEEC | National Economic Empowerment Council |
| NEMC | National Environmental Management Council |

| | |
|---|---|
| PBPA | Petroleum Bulk Procurement Agency |
| PSA | Production Sharing Agreement |
| PURA | Petroleum Upstream Regulatory Authority |
| REA | Rural Energy Agency |
| SADC | Southern African Development Community |
| SBM | Single Buoy Mooring |
| SCADA | Supervisory Control and Data Acquisition |
| SDGs | Sustainable Development Goals |
| SGR | Standard Gauge Railway |
| SPR | Strategic Petroleum Reserve |
| SRT | Single Receiving Terminal |
| TANESCO | Tanzania Electric Supply Company |
| TCPM | Tanzania Concrete Poles Manufacturing Company Limited |
| TGDC | Tanzania Geothermal Development Company Limited |
| TPDC | Tanzania Petroleum Development Corporation |
| TREEP | Tanzania Rural Electrification Expansion Program |
| UNCDF | The United Nations Capital Development Fund |
| UNIDO | United Nations Industrial Development Organization |
| VETA | Vocational Education and Training Authority |

## A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyochambua na kujadili Bajeti ya Wizara ya Nishati (Fungu 58); Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2025/26. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa Mwaka 2026/27.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kutujalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Mkutano huu wa tatu wa Bunge la 13 ili kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa Mwaka 2026/27.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Hotuba hii kama Waziri wa Nishati, naomba kwa namna ya

kipekee kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Wizara hii. Naomba niseme kuwa, uteuzi huu ni dhamana na heshima kubwa kwangu katika kusimamia na kuendeleza Sekta ya Nishati, ambayo ni kichocheo cha ukuaji wa Sekta nyingine za kiuchumi na kijamii, maendeleo ya Taifa na wananchi kwa ujumla. Naahidi kuwa kwa rehema za Mwenyezi Mungu, na kwa kuzingatia miongozo na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, nitatekeleza majukumu yangu kwa weledi na uadilifu, kwa kushirikiana na Bunge lako Tukufu na wadau wengine wa Sekta ya Nishati, ili kuhakikisha maono ya Mheshimiwa Rais katika maendeleo ya Sekta hii na Taifa kwa ujumla yanafikiwa.

## SALAMU ZA PONGEZI

4. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM), kufuatia Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Oktoba, 2025. Ushindi

huo unadhihirisha kukubalika kwake kwa Watanzania, kutokana na umahiri katika uchapakazi na ufuatiliaji katika utendaji wa Serikali ili kuhakikisha sote tunawajibika ipasavyo katika kufikia matarajio ya Watanzania ya kuwaletea maendeleo. Kwa kuwa safari ya kuelekea kwenye maendeleo ya nchi yetu inahitaji ushiriki na uwajibaki wa kila mmoja kwa kuzingatia nafasi, kipaji, uwezo na karama tuliyobarikiwa na Mwenyezi Mungu, nitumie fursa hii kuwaomba Watanzania kuendelea kumuunga mkono Mheshimiwa Rais katika kuliongoza Taifa letu na kujiletea maendeleo.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** nampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuchaguliwa kwake kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nampongeza Dkt. Hussen Ali Mwinyi, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kumpongeza pia Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mbunge wa Jimbo la Iramba Magharibi) kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania. Nawashukuru kwa maelekezo na miongozo wanayonipa, ambayo imekuwa chachu katika kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ipasavyo ya kusimamia na kuendeleza Sekta ya Nishati. Nawapongeza pia Mawaziri wote kwa kuteuliwa kuziongoza Wizara mbalimbali katika Awamu hii, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote walioaminiwa na kuchaguliwa na wananchi ili kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu.

7. ***Mheshimiwa Spika***, nakupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mbunge wa Jimbo la Ilala) kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini) kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge letu Tukufu. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge kwa kuchaguliwa kwao kuliwezesha Bunge hili kutekeleza majukumu yake.

8. ***Mheshimiwa Spika***, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu (Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo) kwa

kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile (Mbunge wa Jimbo la Busega) kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Aidha, nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa ushauri na maoni yao katika kuendeleza na kusimamia Sekta ya Nishati. Naishukuru Kamati kwa kupokea, kujadili na hatimaye kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2026/27 tarehe 24 Machi, 2026, na nitumie nafasi hii kuahidi kuwa Wizara itazingatia ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati, kwa maendeleo ya Sekta hii muhimu katika ukuaji wa Sekta nyingine za kiuchumi na kijamii nchini.

9. ***Mheshimiwa Spika***, nimshukuru pia Katibu wa Bunge Ndg. Baraka I. Leonard, Makatibu wa Kamati na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushikirikiano mkubwa wanaotupatia katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** sina budi kuwashukuru kwa dhati viongozi wenzangu katika Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba (Mb.), Naibu Waziri; Mha. Felchesmi Jossen Mramba, Katibu Mkuu (Umeme na Nishati Jadidifu); na Dkt. James Peter Mataragio, Katibu Mkuu (Mafuta na Gesi Asilia) kwa umahiri na umakini wao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu tuliyokasimiwa na Taifa letu. Niwashukuru pia Makamishna, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi za Taasisi zilizo chini ya Wizara, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake, kwa ushirikiano wanaonipa pamoja na kutekeleza kikamilifu majukumu yao kwa kujituma, tija na ufanisi.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kwa unyenyekevu mkubwa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Chamwino kwa upendo, imani, uelewa na ushirikiano mkubwa wanaonipatia, ambao umeniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kuwatumikia jimboni na kitaifa kwa mafanikio. Kupitia Bunge lako

Tukufu, niwaahidi wananchi wa Jimbo la Chamwino utumishi uliotukuka katika kipindi chote nitakachokuwa nikiwawakilisha katika Bunge hili Tukufu, na kwamba tutaendelea kushirikiana bega kwa bega katika kuhakikisha changamoto zilizopo zinapatiwa ufumbuzi na Jimbo linapiga hatua kubwa za maendeleo. Aidha, namshukuru mke wangu mpedwa Bi. Subira Adadi Rajabu pamoja na wanangu wote wapendwa kwa uvumilivu na ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kijimbo na kitaifa.

**SALAMU ZA POLE**

12. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa, napenda kutoa pole kwako, Bunge lako Tukufu, familia, ndugu, jamaa na wananchi kwa ujumla kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Jenista Joackim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Peramiho, Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) na Mbunge wa Isimani. Wakati wote tutaendelea kukumbuka na kuenzi

michango yao katika maendeleo ya Taifa letu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii pia kuwapa pole Watanzania wenzetu waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki na wengine waliopata madhara mbalimbali kutokana na ajali za barabarani na matukio mengine. Ninamuomba Mwenyezi Mungu awape subira waliopoteza ndugu, majeruhi wapone kwa haraka na marehemu wote wapumzike kwa amani. Amina.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia maudhui ya Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2025/26 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2026/27.

## A.1 MAJUKUMU YA WIZARA

15. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Tangazo la Serikali (GN) Na. 386/2025 la tarehe 19 Desemba, 2025, Wizara imekasimiwa usimamizi na uratibu wa majukumu yafuatayo:

a) Kutunga na kutekeleza Sera kuhusu nishati, mafuta na gesi asilia;
b) Kusimamia rasilimali za nishati na petroli;
c) Kuongeza thamani katika rasilimali za petroli;
d) Kuendeleza miundombinu ya mafuta na gesi;
e) Ununuzi wa mafuta kwa pamoja;
f) Huduma za umeme mijini na vijijini;
g) Kuwezesha ushiriki wa watanzania katika shughuli za nishati na petroli;
h) Kuendeleza vyanzo jadidifu na visivyo jadidifu vya nishati;
i) Uratibu wa masuala ya nishati safi ya kupikia;
j) Udhibiti wa nishati na maji;

k) Kuimarisha utendaji na Rasilimali watu ya Wizara; na

l) Kusimamia Idara, Mashirika ya Umma, Wakala, Programu na Miradi iliyo chini ya Wizara.

Aidha, Wizara pia inatekeleza majukumu yake kupitia Taasisi zilizo chini yake zikiwemo Kampuni Tanzu ambazo ni:

i. Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lenye Kampuni tanzu ambazo ni Kampuniya Kuzalisha Nguzo za Umeme za Zege Tanzania *(Tanzania Concrete Poles Manufacturing Company Limited - TCPM)*; Kampuni ya Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Usafirishaji na Usambazaji Umeme *(Electrical Transmission Distribution Construction and Maintenance Company - ETDCO)* na Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (*Tanzania Geothermal Development Company-TGDC*);

ii. Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(Tanzania Petroleum Development Corporation - TPDC)* lenye kampuni zake tanzu ambazo ni TANOIL na GASCO;

iii. Wakala wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Agency - REA)*;

iv. Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (*Petroleum Upstream Regulatory Authority - PURA)*;

v. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(Energy and Water Utilities Regulatory Authority - EWURA)*; na

vi. Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja *(Petroleum Bulk Procurement Agency - PBPA)*.

## A.2 MWELEKEO WA SEKTA YA NISHATI NCHINI

16. ***Mheshimiwa Spika***, maendeleo ya Taifa lolote yanahitaji uhakika wa upatikanaji wa nishati kwa gharama nafuu. Ni kwa muktadha huo, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 (Dira 2050) imeitambua nishati kama moja ya vichocheo vitakavyowezesha kufikiwa kwa Malengo na Shabaha za Dira hiyo, ikiwemo kuwa na maisha bora na ustawi kwa wote. Hivyo, mwelekeo wa Dira 2050 katika Sekta ya Nishati ni pamoja na kuwezesha kuwepo kwa mfumo bora wa

nishati safi ulio stahimilivu, wenye ufanisi, wa kuaminika na wa gharama nafuu; kuwa na miundombinu thabiti ya nishati inayochochea maendeleo ya viwanda na ustawi wa kiuchumi na kijamii; na kuliwezesha Taifa letu kuwa mzalishaji wa nishati inayokidhi mahitaji ya ndani na moja ya wazalishaji wakuu wa nishati katika Ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika.

## Uzalishaji wa Umeme

17. ***Mheshimiwa Spika***, nchi yetu imebarikiwa kuwa na vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme ikiwa ni pamoja na vyanzo vya maji, jua, upepo, gesi asilia, tungamotaka, jotoardhi na urani vinavyotuwezesha kuwa na uhakika na usalama wa upatikanaji wa nishati ya umeme kwa maendeleo ya Taifa letu. Katika mwaka 2025/26 Serikali imeendelea kuchukua hatua za kuimarisha uzalishaji wa umeme nchini ambapo hadi kufikia Machi, 2026 uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme uliongezeka na kufikia Megawati 4,522.54 ikilinganishwa na Megawati 4,031.71 zilizokuwepo mwezi Machi, 2025 sawa na ongezeko la **asilimia**

**12.17**. Ongezeko hili la uzalishaji wa umeme limetokana na kukamilika kwa miradi mbalimbali ya kuzalisha umeme katika kipindi hiki, ukiwemo mradi wa kuzalisha umeme jua Kishapu - Shinyanga (Awamu ya Kwanza) wenye uwezo wa Megawati 50. Jedwali Na. 1 ni mchanganuo wa uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali hadi Machi, 2026. Aidha, *Kiambatisho Na. 1* ni uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme iliyounganishwa katika Gridi ya Taifa hadi Machi, 2026.

**Jedwali Na. 1: Uwezo wa Mitambo ya Kuzalisha Umeme hadi Machi, 2026 kwa Kutumia Vyanzo Mbalimbali**

| **Chanzo** | **Uwezo wa Mitambo** | | **Hali ya Uzalishaji Kwa Sasa (MW)** | |
|---|---|---|---|---|
| | **MW** | **Asilimia** | **MW** | **Asimilia** |
| Maji | 2,727.31 | 60.30 | 1,387.50 | 60.20 |
| Gesi Asilia | 1,284.58 | 28.40 | 721.00 | 31.28 |
| Mafuta | 262.36 | 5.80 | 29.40 | 1.28 |
| Jua | 65.00 | 1.44 | 39.00 | 1.70 |
| Tungamotaka | 135.49 | 3.00 | 81.00 | 3.51 |
| Upepo | 2.40 | 0.05 | 1.90 | 0.08 |
| Makaa ya mawe | 45.40 | 1.00 | 45.00 | 1.95 |
| **Jumla** | **4,522.54** | **100** | **2,304.80** | **100** |

Chanzo: **EWURA**

18. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na kiwango cha umeme kilichopo kwenye gridi ya Taifa kupitia vyanzo mbalimbali, hadi kufikia mwezi Machi, 2026, mitambo ya kuzalisha umeme ambayo haijaungwa katika Gridi ya Taifa ilikuwa na uwezo wa jumla ya Megawati 492.94 ambayo inajumuisha mitambo inayomilikiwa na TANESCO yenye uwezo wa kuzalisha Megawati 98.16 na Megawati 394.78 zinazalishwa na kampuni binafsi kwa ajili ya matumizi ya kampuni hizo kama inavyoonekana katika *Kiambatisho Na. 2A* na 2*B*. Aidha, katika kuhakikisha kuwa mikoa ya Kagera na Rukwa inapata umeme wa uhakika, Serikali kupitia TANESCO imeendelea kununua umeme wa jumla ya Megawati 67 kutoka nje ya nchi ambapo Megawati 47 zinanunuliwa kutoka nchini Uganda kwa ajili ya Mkoa wa Kagera na Megawati 20 kutoka nchini Zambia kwa ajili ya Mkoa wa Rukwa.

**Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme**

19. ***Mheshimiwa Spika***, ili umeme unaozalishwa uweze kutumiwa na mlaji wa mwisho/mteja, Serikali imeendelea na jitihada za kuimarisha miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme

nchini. Hadi kufikia Machi, 2026 urefu wa miundombinu ya kusafirisha umeme nchini ulikuwa umefikia jumla ya kilomita 8,500.38, ikilinganishwa na kilomita 7,809.67 zilizokuwa zimefikiwa Machi, 2025 sawa na ongezeko la **asilimia 9**. Kwa upande wa miundombinu ya kusambaza umeme, urefu wa miundombinu hiyo umefikia kilomita 240,229.56 ikilinganishwa na kilomita 200,266.25 zilizofikiwa mwezi Machi, 2025 sawa na ongezeko la **asilimia 20** kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2: Urefu wa Miundombinu ya Kusafirisha na Kusambaza Umeme Nchini**

| Na | Msongo (kilovoti) | Urefu (Kilomita) Hadi Machi, 2025 | Urefu (Kilomita) Hadi Machi, 2026 |
|---|---|---|---|
| **Urefu wa Njia za Kusafirisha Umeme** | | | |
| 1. | 400 | 1,524.75 | 1,524.75 |
| 2. | 220 | 3,860.95 | 4,095.62 |
| 3. | 132 | 1,843.97 | 2,300.01 |
| 4. | 66 | 580.00 | 580.00 |
| **Jumla** | | **7,809.67** | **8,500.38** |
| **Urefu wa Miundombinu ya Kusambaza Umeme** | | | |
| 1. | 33 | 67,241.73 | 83,391.32 |
| 2. | 11 | 12,815.54 | 15,082.35 |
| 3. | 0.4 | 120,208.98 | 141,755.89 |
| **Jumla** | | **200,266.25** | **240,229.56** |

Chanzo: **TANESCO**

20. ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na hatua zinazochukuliwa za ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme, kiwango cha upatikanaji wa umeme nchini (*accesibility*) kimeendelea kuongezeka kutoka wastani wa **asilimia 78.4** mwaka 2020 na kufikia wastani wa **asilimia 85.5.** Aidha, kiwango cha wananchi waliounganishiwa umeme nchini (*connectivity)* kimeongezeka kutoka **asilimia 37.7** mwaka 2020 hadi **asilimia 52.1**, na mwelekeo wa Serikali ni kuunganisha jumla ya wateja wapya 8,300,000 ili kufikia asilimia 75 ya wananchi waliounganishiwa umeme ifikapo mwaka 2030.

## Mahitaji ya Umeme Nchini

21. ***Mheshimiwa Spika***, hatua zinazochukuliwa na Serikali za kuwezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii mijini, vijijini na vitongojini zimechochea kasi ya ukuaji wa mahitaji ya umeme nchini, ambapo yameongezeka na kufikia Megawati 2,199.06 yaliyofikiwa tarehe 04 Februari, 2026 sawa na ongezeko la **asilimia 15.24** ikilinganishwa na Megawati 1,908.15 zilizofikiwa tarehe 20 Februari,

2025. Jedwali Na.3 linaonesha mwenendo wa mahitaji ya juu ya umeme nchini kwa Mwaka 2024/25 na 2025/26.

**Jedwali Na. 3: Mwenendo wa Mahitaji ya Juu ya Umeme (MW) Nchini kwa Mwaka 2024/25 na 2025/26**

| Mwezi | Julai | Agosti | Septemba | Oktoba | Novemba | Desemba | Januari | Februari | Wastani |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **2024/25** | 1,683.57 | 1,670.57 | 1,728.24 | 1,792.53 | 1,888.72 | 1,823.52 | 1,888.72 | 1,908.15 | 1,817.12 |
| **2025/26** | 2,016.65 | 2,050.85 | 2,083.46 | 2,120.21 | 2,151.96 | 2180.5 | 2,186.48 | 2199.064 | 2,123.65 |
| **Ongezeko** | **333.08** | **380.28** | **355.22** | **327.68** | **263.24** | **356.98** | **297.76** | **290.91** | **306.53** |

Chanzo: **EWURA**

## Huduma kwa Wateja

22. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia TANESCO imeendelea kuimarisha utoaji wa huduma kwa wateja kwa kuimarisha matumizi ya mifumo ya kidijitali, ambapo ilizindua matumizi ya mita janja (*smart meters*) zinazowezesha umeme unaonunuliwa na mteja kuingia moja kwa moja kwenye mita. Hadi Machi, 2026 jumla ya wateja 105,739 walikuwa wameunganishwa na mita janja na zoezi hilo linaendelea kwa awamu kwenye maeneo yote nchi nzima. Aidha, wateja waliendelea kupewa taarifa mbalimbali kuhusu makatizo ya umeme yanayotokana na kazi za maboresho ya miundombinu ya

umeme au dharura, kupitia ujumbe mfupi wa simu (*Bulk SMS*). Hadi Machi, 2026 jumla ya wateja 5,770,559 wamefikiwa kupitia njia hii.

23. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia TANESCO pia ilifanya mikutano na wadau mbalimbali wakiwemo viongozi wa Serikali za Mitaa, Wakuu wa Wilaya na Mikoa kote nchini, ili kuwafahamisha mikakati mbalimbali inayotekelezwa ya kuboresha upatikanaji wa umeme katika maeneo yao, kuelimisha wananchi kuhusu ulinzi wa miundombinu ya umeme ili kupunguza vitendo vya uhujumu wa miundombinu hiyo, pamoja na kutoa elimu ya usalama na matumizi ya vifaa vya umeme katika kupikia. Jitihada hizi zimeendelea kuleta matokeo chanya katika kuboresha huduma kwa wateja na kuongeza imani ya wananchi kwa huduma zinazotolewa na TANESCO.

## Mafuta na Gesi Asilia

24. ***Mheshimiwa Spika,*** uagizaji wa mafuta nchini umeendelea kufanyika kupitia Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (BPS). Kati ya Julai, 2025 na Machi, 2026

nchi ilipokea jumla ya lita bilioni 5.84 za mafuta zikijumuisha lita bilioni 1.63 za petroli, lita bilioni 3.94 za dizeli na lita milioni 260 za mafuta ya taa na ndege. Kati ya kiasi hicho kilichopokelewa, lita bilioni 2.56 (sawa na asilimia 43.84) ziliagizwa kwa ajili ya soko la ndani, ambapo lita bilioni 3.28 (sawa na asilimia 56.16) yalikuwa ni mafuta kwenda nchi jirani.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu imeendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta ya petroli (petroli, dizeli, mafuta ya taa na mafuta ya ndege), pamoja na kuwepo kwa changamoto za upatikanaji wa bidhaa hizo na kuongezeka kwa gharama za upatikanaji wake kulikosababishwa na vita baina ya Marekani, Israel na Iran. Vita hiyo imesababisha kufungwa kwa Mlango Bahari wa Hormuz *(Strait of Hormuz*) unaopitisha zaidi ya asilimia 20 ya mafuta yote duniani, kuathiri visima vya mafuta, mitambo ya kuchakata mafuta ghafi (*refineries*) na maghala ya kuhifadhi mafuta na hivyo kuathiri mnyororo mzima wa upatikanaji wa bidhaa hizo duniani.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** vita hii imeziathiri sana nchi za Mashariki ya Kati (Falme za Kiarabu, Saudi Arabia, Bahrain, Oman na Kuwait) ambapo nchi yetu inaagiza kiasi cha asilimia 59 ya mafuta yake. Aidha, kiasi cha asilimia 41 ya mafuta kilichosalia huagizwa nchini India ambayo pia hutegemea kupata mafuta ghafi katoka Mashariki ya Kati. Hatua zilizochukuliwa na Serikali ili kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa mafuta ni pamoja na kuliwezesha Shirika la Maendeleo ya petroli Tanzania (TPDC), ambalo ni Shirika la Taifa la Mafuta *(National Oil Company)* kuagiza kiwango cha mafuta ya kutosheleza kipindi cha miezi mitatu ijayo (Mei, Juni na Julai, 2026). Aidha, Serikali inaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa upatikanaji wa mafuta duniani na itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kimkakati ili kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa mafuta, ili kutoathiri utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii nchini.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa gesi asilia nchini katika kipindi hiki ulikuwa futi za ujazo milioni 41,530.94 kutoka katika vitalu vya Songo Songo (Futi za ujazo

milioni 17,945.19) na Mnazi bay (Futi za Ujazo milioni 23,585.75). Gesi asilia hiyo ilitumika katika uzalishaji wa umeme, viwandani, katika vyombo vya moto, taasisi na majumbani.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo ya utangulizi na ufafanuzi kuhusu Mwelekeo wa Sekta ya Nishati nchini, naomba sasa nitoe taarifa kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka 2025/26 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2026/27.

## B. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2025/26

29. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Serikali kupitia Wizara ya Nishati iliendelea na utekelezaji wa mikakati, programu, miradi na kazi mbalimbali zilizohusu uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme mijini, vijijini na vitongojini; utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia; pamoja na kuendeleza matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini kulingana na bajeti iliyoidhinishwa, ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2026 utekelezaji ulikuwa katika hatua mbalimbali.

## Bajeti ya Matumizi ya Wizara na Mtiririko wa Fedha kwa Mwaka 2025/26

30. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Nishati kwa mwaka 2025/26 iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Tisa Sitini na Tano, Milioni Mia Saba Arobaini na Tano, Mia Nne Arobaini na Tano Elfu (Shilingi 1,965,745,445,000)** ambapo **Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Nane Themanini na Sita, Milioni Mia Tano Kumi na Tatu, Mia Mbili Kumi na Tisa Elfu (Shilingi 1,886,513,219,000)** sawa na **asilimia 95.97** ya Bajeti yote ya Wizara ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na **Shilingi Bilioni Sabini na Tisa, Milioni Mia Mbili Thelathini na Mbili, Mia Mbili Ishirini na Sita Elfu (Shilingi 79,232,226,000)** sawa na **asilimia 4.03** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi mwishoni mwa Machi, 2026 Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Mbili Themanini na Mbili, Milioni Mia Nane Thelathini na Tatu, Mia Tano Arobaini na Tano Elfu, Mia Mbili Thelathini na Nane**

**(Shilingi 1,282,833,545,238),** ambapo **Shilingi Bilioni Kumi na Saba, Milioni Mia Mbili Themanini na Moja, Mia Mbili Shirini na Mbili Elfu, Mia Nne Sitini na Moja (Shilingi 17,281,222,461)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Mbili Sitini na Tano, Milioni Mia Tano Hamsini na Mbili, Mia Tatu Ishirini na Mbili Elfu, Mia Saba Sabini na Saba (Shilingi 1,265,552,322,777)** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

## B 1: SEKTA NDOGO YA UMEME NA NISHATI JADIDIFU

32. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta hii inahusika na kuhakikisha kunakuwepo na uhakika na usalama wa upatikanaji wa nishati ya umeme nchini kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme mijini, vijijini na vitongojini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Sekta Binafsi.

## B 1.1: MIRADI YA UZALISHAJI WA UMEME

33. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali iliendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya uzalishaji wa umeme ambayo hutumia kipindi kirefu hadi kukamilika. Aidha, Serikali iliendelea kufanya maandalizi ya awali ya kutekeleza miradi mingine ya kuzalisha umeme, ikiwa ni pamoja na kufanya Upembuzi Yakinifu, tathmini ya mali za wananchi watakaopisha utekelezaji wa miradi, usanifu, kulipa fidia na kutafuta fedha za kugharamia utekelezaji wa miradi hiyo. Hadi kufikia Machi, 2026 utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme ulikuwa kama ifuatavyo:

### (i) Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP – MW 2,115)

34. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara ya Nishati na TANESCO imeendelea kusimamia mradi huu wa kimkakati ambao tayari umekamilika na umeme unaendelea kuzalishwa kupitia mitambo yote tisa (9) ya uzalishaji, kwa kuzingatia mahitaji ya umeme. Aidha, mbali na usimamizi wa mradi, kazi

nyingine zilizofanyika ni pamoja na kufanya marekebisho madogo madogo (*snags rectification*) na kukamilisha ujenzi wa ghala la kuhifadhia vifaa katika kituo cha kupoza umeme cha Chalinze. Sambamba na kazi hizo, TANESCO na Bodi ya Bonde la Mto Rufiji imeingia makubaliano ya ushirikiano katika kutunza vyanzo vya maji na ushirikishwaji wa wadau katika utunzaji wa vyanzo vya maji yanayoelekea katika mradi.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizofanyika katika mradi huu ni kukamilisha zoezi la udabuaji wa mto Mswiswi wenye urefu wa kilomita 29; na kufanya tathmini ya maeneo ya kupanda miti kwenye madakio (*catchment*) ya bonde la mto Rufiji, ambapo jumla ya miti 5,000 imepandwa katika maeneo ya Wanging'ombe, Kidatu, Kihansi na Mtera. Vilevile, Serikali imefanya zoezi la kufunga mifereji isiyo rasmi katika maeneo ya Wanging'ombe, Kilombero, Mbarali, Ifakara, Iringa, Mahenge na Kilosa na kukamilisha ujenzi wa tuta lenye urefu wa kilomita 11 la kuzuia mafuriko na upotevu wa maji kwenye mto Lumemo katika eneo la Ifakara.

### (ii) Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Jua Mkoani Shinyanga – MW 150

36. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya jua katika eneo la Kishapu mkoani Shinyanga, chenye uwezo wa kuzalisha jumla ya Megawati 150. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Awamu ya Kwanza ya utekelezaji wa mradi huu inayohusisha uzalishaji wa Megawati 50 kwa gharama ya **Shilingi bilioni 118.68** imekamilika na umeme huo umeunganishwa kwenye Gridi ya Taifa. Aidha, mradi huu ni wa kihistoria kwa kuwa ni wa kwanza kutekelezwa na Serikali kati ya miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia chanzo cha nishati ya jua. Mradi huu umewezesha kuongeza wigo wa vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme nchini na ni kielelezo cha utashi wa namna Tanzania inavyochukua hatua mahsusi za kuelekea kwenye uzalishaji wa nishati kwa kutumia vyanzo safi na rafiki wa mazingira.

**(iii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi I Extension – MW 185**

37. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia yenye uwezo wa kuzalisha Megawati 185 pamoja na uboreshaji wa njia ya kusafirisha umeme yenye msongo wa kilovoti 132 kutoka kituo cha kupoza umeme cha Kinyerezi – Gongolamboto – Mbagala. Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 187.99** sawa na takriban **Shilingi bilioni 517.04.**

38. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2026 kazi zilizokamilika ni pamoja na kusimika na kuwasha transfoma Na.3 katika kituo cha kupoza umeme cha Kinyerezi I; ubadilishaji wa nyaya za umeme kutoka kituo cha kupoza umeme cha Gongolamboto hadi kituo cha Mbagala kwa kuweka nyaya zenye uwezo wa kusafirisha MW 170 badala ya MW 80; na kumalizia kazi ya kusimika na kuwasha transfoma mbili (2) katika kituo cha Gongolamboto na Mbagala. Vilevile, kazi ya usimikaji wa tenki

la kukusanya maji kutoka vipoza hewa (*chillers*) vya mashine (*gas turbine*) inaendelea na utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 99** kwa upande wa kituo cha kuzalisha umeme na **asilimia 90.4** kwa upande wa uboreshaji wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Kinyerezi kupitia Gongolamboto hadi Mbagala.

### (iv) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Malagarasi - MW 49.5

39. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea na utekelezaji wa mradi huu ambapo hadi kufikia Machi, 2026 utekelezaji kwa upande wa ujenzi wa kituo cha uzalishaji umeme ulikuwa umefikia **asilimia 23.73** ambapo kazi zilizokamilika ni pamoja na uchepushaji wa mto; uchimbaji wa njia za maji (*water ways*) na tenki la kupumulia (*surge tank*); uchimbaji wa nyumba ya mitambo *(power house*); ujenzi wa kambi za muda za mkandarasi; na usimikaji wa mtambo wa kusaga kokoto na kuchanganyia zege (*batching plant*). Aidha, Serikali imekamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilomita 54 kutoka

Malagarasi hadi Kidahwe, pamoja na kusambaza umeme katika vitongoji 18 vilivyomo ndani ya vijiji saba (7) vilivyopitiwa na mradi ambapo jumla ya wateja 750 zikiwemo shule, vituo vya afya na kaya wamenufaika na mradi huu.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zinazoendelea katika ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme ni pamoja na uchimbaji wa eneo la ujenzi wa tuta (*main dam*) na eneo la kituo cha kupokelea umeme (*switch yard*), ujenzi wa nyumba ya mitambo (*power house*), njia za maji (*water ways*), madaraja (*culverts*) kwenye barabara na kambi za kudumu na ofisi (*permanent camps*). Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 144.14** sawa na takriban **Shilingi bilioni 396.44**.

### (v) Ukarabati wa Mitambo katika Kituo cha Kuzalisha Umeme cha Hale

41. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea na ukarabati wa miundombinu ya kuzalisha umeme katika Kituo cha Hale chenye uwezo wa kuzalisha Megawati 21 ambapo utekelezaji kwa upande wa *Lot 1* iliyohusisha uchimbaji wa handaki na ujenzi wa barabara imekamilika.

Aidha, *Lot 2* inayohusisha ujenzi wa jengo la kupokea umeme (*switchyard)*, njia ya kuchepusha umeme (*by pass line*), matengenezo ya jumba la mitambo (*power house civil works*), eneo la '*intake'*, kituo cha kupoza umeme na nyumba ya mitambo umefikia **asilimia 75.95.** Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 21.2** sawa na takriban **Shilingi bilioni 58.31**.

### (vi) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Kakono – MW 87.8

42. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme chenye uwezo wa Megawati 87.8 kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Kagera na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilomita 38.7 kutoka Kakono hadi Kyaka, mkoani Kagera. Hadi kufikia Machi, 2026 Serikali kupitia TANESCO ilikuwa imekamilisha maandalizi ya nyaraka za zabuni kwa ajili ya kuwapata Wakandarasi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na kituo cha kupoza umeme pamoja na tathmini ya usanifu (*conceptual design*) ya ujenzi wa bwawa. Aidha, Serikali inaendelea

na taratibu za kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi waliopisha mradi. Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 308.38** sawa na takriban **Shilingi bilioni 848.16**.

**(vii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Ruhudji – MW 358**

43. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kuzalisha umeme wa Megawati 358 kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Ruhudji mkoani Njombe na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilomita 170 kutoka Ruhudji hadi kituo cha kupoza umeme cha Kisada mkoani Iringa. Ili kuimarisha kasi ya utekelezaji wa mradi huu, Serikali inakusudia kuutekeleza kwa ushirikiano na Sekta Binafsi kupitia utaratibu wa Ubia Baina ya Serikali na Sekta Binafsi (*Public Private Partnership - PPP*).

**(viii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Rumakali – MW 222**

44. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu unalenga kuzalisha umeme wa Megawati 222 kwa kutumia maji ya mto Rumakali mkoani Njombe pamoja na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme yenye msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilomita 65 kutoka kwenye mitambo ya uzalishaji wa umeme hadi kituo cha kupoza umeme cha Iganjo mkoani Mbeya. Serikali kupitia TANESCO inaendelea kufanya maandalizi ya utekelezaji wa mradi huu pamoja na kufanya majadiliano na wadau mbalimbali walioonesha nia ya kutekeleza mradi kwa kushirikiana na TANESCO kupitia utaratibu wa PPP ili kuongeza kasi ya utekeleza wake.

**(ix) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa kutumia Gesi Asilia wa Mtwara – MW 300**

45. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea na maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme kiasi cha Megawati 300 kwa kutumia gesi asilia mkoani Mtwara,

ambapo hatua za awali za ulipaji wa fidia kiasi cha Shilingi milioni 500 zimetekelezwa, na taratibu za kuwezesha ulipaji wa fidia kwa wananchi waliosalia katika vijiji vya Kisiwa na Namgogoli vilivyopo Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara zinaendelea. Aidha, Serikali kupitia TANESCO iliendelea kuimarisha upatikanaji wa umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara, ambapo katika kipindi hiki ilipeleka mtambo mwingine wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia wenye uwezo wa kuzalisha Megawati 20 na hivyo kuongeza uwezo wa uzalishaji wa umeme katika mikoa hiyo kufikia Megawati 77.90 kutoka Megawati 57.5 zilizokuwepo awali, ambapo mahitaji ya umeme katika mikoa hiyo ni Megawati 38.5.

### (x) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Upepo - MW 100 Kititimo Mkoani Singida

46. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu ni moja ya miradi ya nishati jadidifu inayotarajiwa kuchangia katika kuongeza vyanzo mchanganyiko (*energy mix*) vya uzalishaji wa nishati nchini na hivyo kupunguza utegemezi katika vyanzo vya sasa vya mafuta. Hadi Machi, 2026 taratibu

zilizofanyika ni pamoja na kuendelea kufanya Upembuzi Yakinifu na kusaini Hati ya Makubaliano (MoU) kati ya TANESCO na Mwekezaji kwa ajili ya kutekeleza mradi.

### (xi) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa kutumia Jua - MW 130 wa Zuzu Dodoma

47. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mradi huu umeendelea katika kipindi hiki ambapo hadi Machi, 2026 Serikali kupitia TANESCO ilikuwa imekamilisha Upembuzi Yakinifu wa ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme jua wa Megawati 130 katika eneo la Zuzu mkoani Dodoma. Aidha, Serikali kupitia TANESCO imesaini Hati ya Makubaliano (MoU) na mwekezaji, Kampuni ya Mirambo Power Limited kwa ajili ya kuanza kuzalisha Megawati 15 za awali, ambapo hatua inayofuata ni kufanya upekuzi wa kina *(Due Diligence*) ili kujiridhisha na uwezo wa kampuni hiyo, kabla ya kuendelea na hatua za utekelezaji wa mradi.

### (xii) Mradi wa Kuzalisha Umeme Jua - MW 100 Same

48. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Sweden (*Swedfund*) inakusudia kufanya Upembuzi Yakinifu wa mradi wa kuzalisha umeme jua Megawati 100 katika eneo la Same mkoani Kilimanjaro, ikiwa ni hatua ya maandalizi ya kuzalisha umeme kupitia chanzo hicho. Aidha, hadi Machi, 2026 Serikali kupitia TANESCO ilikuwa katika hatua za mwisho za kumpata Mshauri Mwelekezi atakayefanya Upembuzi Yakinifu katika eneo hilo.

## B 1.2: MIRADI YA USAFIRISHAJI NA USAMBAZAJI WA UMEME

### (i) Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kutoka Bwawa la Julius Nyerere hadi Chalinze – kV 400 na Kituo cha Kupoza Umeme cha Chalinze

49. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekamilisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400

yenye urefu wa kilomita 160 kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha Julius Nyerere hadi Chalinze mkoani Pwani pamoja na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Chalinze ambao kwa sasa upo katika hatua za uangalizi. Aidha, njia hiyo na kituo cha kupoza umeme cha Chalinze vinatumika kusafirisha na kuingiza umeme unaozalishwa JNHPP katika Gridi ya Taifa na kuendelea kutumika nchini. Utekelezaji wa mradi huu umegharimu **Shilingi bilioni 158.1** fedha zilizotolewa na Serikali kwa **asilimia 100**.

**(ii) Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze – Dodoma**

50. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Chalinze hadi Dodoma yenye urefu wa kilomita 345 na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya Chalinze na Dodoma ambapo utekelezaji wake umefikia **asilimia 74.13**. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa misingi kwa ajili ya nguzo za

kusafirishia umeme; ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Chalinze na Zuzu; na ukaguzi na usafirishaji wa vifaa vikiwemo nguzo, transfoma na *reactors*. Kukamilika kwa mradi huu kutaimarisha usafirishaji na usambazaji wa umeme unaozalishwa JNHPP na kuwezesha kuwafikia watumiaji wengi katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Kanda za Kati, Ziwa, Magharibi na Nyanda za Juu Kusini. Utekelezaji wa mradi huu unagharimu **Shilingi bilioni 507.99.**

**(iii) Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya na Tunduma (TAZA)**

51. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Iringa kupitia Mbeya, Tunduma hadi Sumbawanga yenye urefu wa kilomita 616.5 pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme katika maeneo ya Iringa, Kisada, Iganjo, Tunduma na Sumbawanga. Hadi Machi, 2026, utekelezaji ulikuwa umefikia **asilimia 77.06**, na kazi mbalimbali ikiwemo

ujenzi wa vituo zinaendelea. Aidha, taratibu za kusafirisha vifaa vya mradi kutoka Bandari ya Dar es Salaam zikiwemo transfoma na *reactors* kwenda kwenye eneo la mradi zinaendelea. Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 593.19** sawa na takriban **Shilingi trilioni 1.63.**

**(iv) Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze - Kinyerezi – Mkuranga**

52. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilomita 135.5 kutoka Chalinze kupitia Kinyerezi hadi Mkuranga. Mradi huu pia unahusisha ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Kinyerezi na Mkuranga pamoja na upanuzi wa kituo cha Chalinze. Hadi Machi, 2026 utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 60.61**. Kukamilika kwa mradi huu kutaimarisha mfumo wa usafirishaji wa umeme katika Gridi ya Taifa na pia kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa ajili ya uzalishaji katika maeneo ya viwanda wilayani Mkuranga.

Utekelezaji wa mradi huu unagharimu **Shilingi bilioni 560.36.**

**(v) Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Rufiji – Mkuranga**

53. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TANESCO inatarajia kutekeleza mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka katika Bwawa la Julius Nyerere (Rufiji) hadi Mkuranga. Kazi zilizofanyika hadi Machi, 2026 ni pamoja na kukamilisha Hadidu za Rejea kwa ajili ya kufanya Upembuzi Yakinifu na Athari kwa Mazingira *(Environmental Impact Assesment)*. Kutekelezwa kwa mradi huu kutawezesha kuwepo kwa njia mbadala ya kusafirisha umeme unaozalishwa JNHPP.

**(vi) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Ibadakuli, Shinyanga**

54. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Iringa –

Singida - Shinyanga na kituo cha kupoza umeme cha Ibadakuli, Shinyanga. Hadi Machi, 2026 utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 48.8** na ujenzi unaendelea. Utekelezaji wa mradi huu unagharimu **Dola za Marekani milioni 80.62** sawa na takriban **Shilingi bilioni 221.73**.

**(vii) Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa *(National Grid Stabilization Project)* – Gridi Imara**

55. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa Gridi Imara unatekelezwa na Serikali kupitia TANESCO kwa kutumia fedha za ndani ambao unalenga kuimarisha miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme pamoja na vituo vya kupoza umeme katika mikoa mbalimbali nchini. Aidha, mradi unahusisha pia ufungaji wa mitambo na vifaa vya kisasa, ubadilishaji wa nguzo za miti kwa kusimika nguzo za zege, ufungaji wa nyaya zenye uwezo wa kusafirisha umeme mkubwa pamoja na transfoma. Utekelezaji wa mradi huu umefikia **asilimia 54** ambapo miradi saba (7) kati ya 27 imekamilika na utekelezaji kwa miradi

mingine unaendelea. Miradi iliyokamilika ni:

a) Ujenzi wa njia ya kusambaza umeme msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 60 kutoka Nyakanazi hadi Kakonko na kutoka Nyakanazi hadi Lusahunga;

b) Ujenzi wa njia ya kusambaza umeme msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 16 inayounganisha kituo cha Nyakanazi, Bulyanhulu na Geita;

c) Mradi wa kuboresha njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 132 kutoka Ubungo kupitia Chalinze hadi Hale kwa kubadilisha nyaya za umeme kutoka Megawati 80 hadi Megawati 150;

d) Mradi wa kituo cha kuongeza nguvu ya umeme *(Automatic Voltage Regulator)* Songwe Mkwajuni na Mbangala;

e) Mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilomita saba (7) kutoka Ilala hadi Kurasini kwa

kutumia waya wa ardhini *(underground cable)*;

f) Ujenzi wa kituo cha kusambaza umeme *(switching station)* msongo wa kilovoti 33 katika eneo la Msigani lililopo Mbezi; na

g) Ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 132 kutoka Tabora hadi Katavi kupitia vituo vya Ipole na Inyonga.

Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi 20 ya mradi huu iliyosalia ni kama inavyoonekana katika *Kiambatisho Na.3.*

**(viii) Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Kupoza Umeme katika Kila Wilaya Nchini**

56. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unaendelea kutekelezwa kupitia utekelezaji wa mradi wa Gridi Imara Awamu ya Kwanza ukilenga kuimarisha usambazaji na kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika katika kila eneo nchini kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na jamii. Utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya mradi wa Gridi Imara

unahusisha Wilaya 15 ambapo utekelezaji umekamilika katika Wilaya za Mlele, Mpanda, Urambo na Sikonge. Aidha, utekelezaji unaendelea katika Wilaya za Uvinza, Rombo, Masasi, Ukerewe, Kibaha, Mkuranga, Tunduru, Bariadi, Handeni, Lushoto na Kilindi. Gharama za utekelezaji wa mradi huu ni **Shilingi bilioni 639.17.**

**(ix) Mradi wa Ukarabati na Uboreshaji wa Gridi ya Taifa *(Grid Rehabilitation and Upgrading Project - TTGRUP)***

57. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kuimarisha Gridi ya Taifa kwa kukarabati na kuboresha vituo vya kupoza umeme katika maeneo mbalimbali nchini na unagharamiwa na Serikali ya Ufaransa kupitia Shirika lake la Maendeleo (AFD) pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mradi huu unatekelezwa katika mafungu matatu kwa gharama ya **Euro milioni 70.37** sawa na takriban **Shilingi bilioni 222.59** kama ifuatavyo:

- Fungu la kwanza linahusisha ukarabati na maboresho ya vituo

nane (8) vya kupoza umeme kwenye Gridi ya Taifa ambapo ukarabati na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya Mlandizi, Same na Bukoba umefikia **asilimia 87**; ukarabati na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya Mbeya, Tabora na Mufindi umefikia **asilimia 86**; na ukarabati na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya Musoma na Mwanza umefikia **asilimia 73**. Aidha, kwa sasa kazi zinazoendelea ni kukamilisha ukarabati wa vituo pamoja na kufunga mfumo wa *'Automatic Generation Control (AGC)'* kwenye vituo vya kuzalishia umeme wa gesi Kinyerezi I, Ubungo I, Ubungo II, na Tegeta na utekelezaji wake umefikia **asilimia 98.1**.

- Fungu la pili lilihusisha ukarabati na uboreshaji wa miundombinu ya mawasiliano katika njia za kusafirisha umeme za Kondoa – Babati – Mbulu – Karatu; Shinyanga – Mabuki – Mwanza – Bunda – Musoma; na Iringa – Mufindi – Makambako – Mbeya zilizopo katika Gridi ya Taifa

ambapo utekelezaji wake ulikamilika mwezi Desemba, 2024.

- Fungu la tatu linahusisha ufungaji wa vifaa vinavyotumika kuendeshea na kuongozea mfumo wa Gridi ya Taifa (SCADA) ambapo utekelezaji wake umefikia **asilimia 98.3.**

**(x) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Benaco hadi Kyaka**

58. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilomita 166.17 kutoka Benaco hadi Kyaka mkoani Kagera. Hadi Machi, 2026 Mkandarasi ameendelea na uwasilishaji wa vifaa vya ujenzi katika eneo la mradi pamoja na usanifu wa michoro ya mradi huo. Aidha, Serikali inaendelea na taratibu za ulipaji wa fidia ambapo hadi Machi, 2026 jumla ya **Shilingi bilioni 1.6** zimelipwa kwa wananachi wanaopisha eneo la mradi wa njia ya kusafirisha umeme na **Shilingi milioni 351** zimelipwa kwa wananchi wanaopisha eneo la kituo cha kupoza

umeme cha Benaco na taratibu za kukamilisha malipo ya fidia zinaendelea. Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 57.62** sawa na takriban **Shilingi bilioni 61.58**.

**(xi) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Makutopora Hadi Tabora (SGR Lot 3) na kutoka Tabora hadi Isaka (SGR Lot 4) kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme**

59. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 220 kutoka Makutopora hadi Tabora *(SGR Lot 3)* na kutoka Tabora hadi Isaka *(SGR Lot 4)* kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya umeme. Hadi Machi, 2026 kazi zilizokamilika katika *Lot 3* ni pamoja na Upembuzi Yakinifu na usanifu wa muundo dhana *(conceptual design);* na kuendelea na uandaaji wa Hadidu za Rejea kwa ajili ya taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi. Kwa upande wa *Lot 4* kazi iliyofanyika ni kukamilisha Upembuzi Yakinifu wa Awali (*Reconnaissance Survey*). Aidha, Serikali

inaendelea na taratibu za uthamini wa mali za wananchi wanaopisha mradi katika maeneo hayo ili waweze kulipwa fidia.

**(xii) Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Mwanza Hadi Isaka kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme (SGR Lot 5)**

60. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 220 kutoka Mwanza hadi Isaka kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya umeme. Hadi Machi, 2026 uthamini wa mali za wananchi wanaopisha mradi ulikuwa umekamilika na Serikali inaendelea na malipo ya fidia ambapo **Shilingi bilioni 8** zimelipwa kwa wananchi wanaopisha mradi.

**(xiii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 Kutoka Sumbawanga Hadi Kigoma Kupitia Mpanda (Km 480) na Kituo cha Kupoza Umeme Mpanda**

61. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilomita 480 kutoka Sumbawanga hadi Kigoma kupitia Mpanda pamoja na kituo cha kupoza umeme cha Mpanda. Gharama za utekelezaji wa mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 372.5** sawa na takriban **Shilingi trilioni 1.02**. Kwa sasa Serikali inaendelea na majadiliano na Benki ya Maendeleo Afrika kwa ajili ya upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa mradi huu.

**(xiv) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 Kutoka Segera – Same – Lemugur (Kisongo) Arusha**

62. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Segera kupitia Same hadi Lemugur (Kisongo) Arusha. Hadi Machi, 2026 kazi zilizokamilika ni pamoja na Upembuzi Yakinifu na Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA); na uthamini wa mali za wananchi wanaopisha eneo la mradi na taratibu za upatikanaji wa fedha za fidia zinaendelea. Aidha, Serikali

inaendelea na majadiliano na Wadau wa Maendeleo ili kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Utekelezaji wa mradi huu unakadiriwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 182** sawa na takriban **Shilingi bilioni 500.57**.

**(xv) Ujenzi wa Njia za Kusafirisha Umeme *(Submarine Cables)* Msongo wa Kilovoti 220 Kutoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar na Mafia**

63. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilomita 49.95 kutoka Ununio – Dar es Salaam kwenda Unguja na msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilomita 87 kutoka Tanga kwenda Pemba kupitia chini ya Bahari (*submarine cables*). Aidha, mradi unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 109.2 kutoka Mkuranga hadi Mafia. Kazi zilizokamilika ni pamoja na Upembuzi Yakinifu, usanifu wa awali wa mradi na tathmini ya mali za wananchi ambapo taratibu za malipo ya fidia zinaendelea kufanyika. Kwa sasa Serikali

kupitia TANESCO ipo katika hatua za kumpata Mshauri Mwelekezi wa kusimamia ujenzi wa mradi. Utekelezaji wa mradi huu unakadiriwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 282.57** sawa na takriban **Shilingi bilioni 777.17**.

**(xvi) Mradi wa Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Tanzania hadi Uganda (Ibadakuli - Masaka)**

64. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha diplomasia ya uchumi nchi za Tanzania na Uganda zinakusudia kujenga njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Ibadakuli (Tanzania) kwenda Masaka (Uganda). Ujenzi wa njia hiyo utatekelezwa sambamba na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya Ibadakuli, Nyakanazi na Kyaka. Hadi Machi, 2026 zoezi la uhakiki wa mali za wananchi wanaopisha eneo la mradi lilikuwa limekamilika. Aidha, kazi zinazoendelea kutekelezwa ni pamoja na kutafuta fedha za kutekeleza mradi huu.

### (xvii) Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze – Segera na Msongo wa Kilovoti 220 Segera – Tanga

65. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Chalinze – Segera na msongo wa kilovoti 220 ya Segera – Tanga. Mradi unahusisha pia ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Segera na Tanga. Hadi Machi, 2026 kazi zilizokamilika ni pamoja na Upembuzi Yakinifu, Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA) pamoja na usanifu wa mradi. Aidha, taratibu za utafutaji fedha kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha mradi zinaendelea. Utekelezaji wa mradi huu unakadiriwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 237** sawa na takriban **Shilingi bilioni 651.84**.

### (xviii) Mpango Kabambe wa Kuboresha Mfumo wa Usambazaji Umeme Msongo wa Kilovoti 220 katika Majiji ya Mbeya, Arusha na Mwanza

66. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inakusudia kuimarisha mfumo wa usambazaji wa umeme msongo wa kilovoti 220 katika majiji ya Mbeya, Arusha na Mwanza ili kuwezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika utakaochochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo hayo. Aidha, Upembuzi Yakinifu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya usambazaji umeme msongo wa kilovoti 220 katika majiji hayo umekamilika na taratibu za utafutaji wa fedha za utekelezaji wa mradi zinaendelea.

### (xix) Mradi wa Kuboresha Mfumo wa Usambazaji Umeme katika Jiji la Dodoma

67. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kuboresha na kuimarisha miundombinu ya usambazaji umeme katika Jiji la Dodoma, ili kukidhi ongezeko la mahitaji ya umeme linalochochewa na ukuaji wa shughuli za

kiuchumi na kijamii na kuongezeka kwa idadi ya watu katika Jiji hili. Utekelezaji wa mradi huu unakadiriwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 150.1** sawa na takriban **Shilingi bilioni 412.83**. Hadi Machi, 2026 kazi zilizokamilika ni pamoja na Upembuzi Yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa kuimarisha hali ya upatikanaji wa umeme katika Jiji la Dodoma (*Dodoma ring circuit).* Aidha, Serikali inaendelea na taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 220 kutoka Zuzu – Msalato – Ihumwa – Kikombo – Zuzu pamoja na vituo vya kupoza umeme vya Msalato, Ihumwa na Kikombo.

68. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia inaendelea kuimarisha upatikanaji wa umeme mkoani Dodoma kwa kubadilisha nguzo za miti na kuweka nguzo za zege kwenye njia mbalimbali za kusambaza umeme. Hadi Machi, 2026 jumla ya nguzo 3,105 zimebadilishwa sawa na **asilimia 98** ya lengo ambapo zoezi hilo linaendelea. Aidha, Serikali imekamilisha maboresho ya njia ya usambazaji umeme msongo wa kilovoti 11 kutoka mjini kati hadi Bungeni kwa kubadilisha nyaya zisizofunikwa kwa

kuweka nyaya zilizofunikwa (*insulated conductors*).

### (xx) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma

69. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma yenye urefu wa kilomita 280, ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kidahwe Mkoani Kigoma, upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi na usambazaji umeme katika vijiji 18 vilivyopo katika eneo la mradi. Aidha, ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme umekamilika na ipo katika hatua ya uangalizi na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme umefikia **asilimia 45.15.** Gharama za utekelezaji wa mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 186.93** sawa na takriban **Shilingi bilioni 514.13**.

## (xxi) Utekelezaji wa Miradi Mingine na Matengenezo ya Mitambo

70. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TANESCO iliendelea kufanya ukaguzi na matengenezo ya mitambo mbalimbali ya kuzalisha umeme ili kuimarisha hali ya upatikanaji wa umeme nchini. Matengenezo ya mitambo iliyokamilika ni pamoja na Mtwara I (mitambo yote 13); Mtwara II (mtamboNa.16); Tegeta (mitambo yote mitano (5)); Ubungo I (mtambo Na. 2 na Na.12); Ubungo II (mtambo Na. 3) na Ubungo III (mitambo yote mitatu (3)). Aidha, matengenezo mengine yameendelea kufanyika katika kituo cha Kinyerezi I (mitambo yote nane (8)); Kinyerezi II (mitambo yote nane (8)); Somanga (mitambo yote mitatu (3)); Kidatu (mitambo Na.1 na Na.4); Mtera (Mitambo yote miwili (2)); New Pangani (mitambo yote miwili (2)) na Kihansi (mitambo yote mitatu (3)). Vilevile, matengenezo yamehusisha miundombinu ya kusafirisha umeme, ikiwa ni pamoja na kubadilisha nyaya za zamani na kuweka za kisasa zenye uwezo wa kubeba umeme mwingi katika njia za kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 132 za Same - Kiyungi na Hale – Same.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** maboresho ya miundombinu ya umeme yamefanyika pia katika vituo vya kupoza umeme kwa kuongeza transfoma katika maeneo mbalimbali vikiwemo vituo vilivyopo katika mikoa ya Dar es Salaam (Chang'ombe na Mbagala), Dodoma (Dodoma Mjini), Kagera (Kasiga na Muleba), Mwanza (Mwanza South), Arusha (Njiro), Shinyanga (Ibadakuli), Lindi (Lindi Mjini na Mahumbika), Iringa (Mafinga), Tanga (Kange) na Pwani (Mlandizi). Aidha, Serikali inaendelea na maboresho ya vituo vingine katika maeneo mbalimbali nchini kama inavyoonekana katika *Kiambatisho Na.4.*

## B 1.3: UTEKELEZAJI WA MIPANGO NA MIKAKATI YA UENDELEZAJI WA SEKTA NDOGO YA UMEME NA NISHATI JADIDIFU

72. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na utekelezaji wa mikakati na mipango mbalimbali ya uendelezaji wa Sekta Ndogo ya Umeme na Nishati Jadidifu kama ifuatavyo:

### a) Mpango Mahususi wa Nishati wa Taifa

73. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara ya Nishati inaratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango Mahususi wa Taifa wa Nishati *(National Energy Compact)* wa Miaka Mitano (2025 - 2030) ambao unajulikana kama *Mission 300*. Mpango huo unalenga kuongeza kiwango cha upatikanaji wa umeme kutoka asilimia 78.4 mwaka 2025 hadi kufikia asilimia 100 ifikapo mwaka 2030; kuongeza kasi ya kuunganisha umeme nchini kutoka asilimia 46 mwaka 2025 hadi kufikia asilimia 75 mwaka 2030; kuongeza mchango wa nishati jadidifu katika uzalishaji wa umeme kutoka asilimia 61.8 mwaka 2025 hadi kufikia asilimia 75 ifikapo mwaka 2030; kuongeza kiwango cha matumizi ya nishati safi ya kupikia kutoka asilimia 6.9 ya mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 75 mwaka 2030; na kuongeza mchango wa sekta binafsi katika Sekta ya Nishati kwa kiasi cha Dola za Marekani bilioni 4.39 sawa na takriban Shilingi trilioni 11.218 ifikapo mwaka 2030. Hadi Machi, 2026 Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zake zinazotekeleza Mpango huo

imeandaa miradi inayolenga kutekeleza malengo ya Mpango huo, ambapo utekelezaji unaendelea. Aidha, mpango wa kusimamia utekelezaji umeandaliwa ili kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa malengo yaliyokusudiwa.

### b) Mpango Kabambe wa Uendelezaji Sekta Ndogo ya Umeme wa Mwaka 2024 (*Power System Master Plan Update 2024 - PSMP 2024*)

74. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara ya Nishati imekamilisha mapitio ya Mpango Kabambe wa Uendelezaji wa Sekta Ndogo ya Umeme wa Mwaka 2024 kwa kuhuisha Mpango wa Mwaka 2020 ili uendane na hali ya sasa na ya miaka 25 ijayo kuhusu sekta ndogo ya umeme. Hatua hii inatokana na kuendelea kuongezeka kwa kasi ya mahitaji ya umeme nchini, ukuaji wa soko la umeme, maendeleo ya teknolojia na vipaumbele vya Serikali ili kuweza kufikia matarajio ya kitaifa yaliyobainishwa katika Dira 2050, ikiwemo kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika na wa gharama nafuu kwa wananchi wote ifikapo 2050, ili kujenga uchumi wa viwanda na huduma za kijamii zilizo bora. Vilevile,

Mpango umezingatia umuhimu wa kuongeza uwiano wa nishati safi (maji, jua, upepo, jotoardhi na nyuklia) sambamba na kupunguza utegemezi wa vyanzo visivyo endelevu na ambavyo siyo rafiki kwa mazingira ili kulinda mazingira na kuendana na malengo ya kimataifa ya mabadiliko ya tabianchi.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** mpango huo pia umebainisha umuhimu wa kuimarisha mahusiano ya kikanda katika uendelezaji wa Sekta ya Nishati kwa kubainisha miradi ya kipaumbele ili kuimarisha miundombinu ya Gridi ya Taifa na nchi za jirani hususan zilizopo katika Jumuiya za Kikanda za EAC na SADC. Vilevile, Mpango umebainisha mikakati ya kuimarisha ushirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ili kuvutia uwekezaji wa Sekta Binafsi ya ndani na nje ya nchi katika ugharamiaji wa miradi mikubwa na ya kimkakati ya kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme.

c) **Mkakati wa Nishati Jadidifu na Mpango wa Utekelezaji wa Mkakati *(Renewable Energy Strategy and its Implementation Roadmap)***

76. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara ya Nishati imekamilisha uandaaji na kuanza kutekeleza Mkakati wa Nishati Jadidifu na Mpango wake wa Utekelezaji wa Mwaka 2024 - 2034. Mkakati huo pamoja na mambo mengine, unalenga kuimarisha uwezo wa kitaifa wa uzalishaji wa nishati jadidifu utakaoliwezesha Taifa kuwa na vyanzo mchanganyiko vya umeme unaoendana na mahitaji ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii, ikiwa ni pamoja na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na uhamasishaji wa utunzaji wa mazingira.

d) **Mpango wa Utekelezaji wa Matumizi Bora ya Nishati *(Comprehensive Energy Efficiency Action Plan 2025 - 2034)***

77. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara ya Nishati inakamilisha Mpango wa Utekelezaji wa Matumizi Bora ya Nishati (2025 - 2034). Mpango huo utatumika kama

nyenzo muhimu ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi Bora ya Nishati (2024 – 2034). Aidha, Mpango huo pamoja na mambo mengine umebainisha vipaumbele mbalimbali vitakavyotekelezwa ili kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ya nishati, kuongeza ufanisi wa mitambo na vifaa, na kuimarisha usalama wa nishati kwa muda mrefu. Vilevile, Mpango kazi huo pia utajikita katika kuhamasisha Watanzania kutumia nishati kwa ufanisi kwa kutumia teknolojia bora ili kupunguza gharama za matumizi, upotevu wa umeme na kutunza mazingira bila kupunguza uzalishaji au ubora wa huduma.

**e) Ushiriki katika Mkutano wa 30 wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP30)**

78. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilishiriki katika Mkutano wa 30 wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi *(Conference of the Parties - COP 30)* uliofanyika tarehe 10 - 21 Novemba, 2025 Belem nchini Brazil. Ushiriki katika Mkutano huo ulilenga kuimarisha nafasi ya

Tanzania katika maamuzi ya kimataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi, kufanya majadiliano na Washirika wa Maendeleo kuhusu ufadhili wa miradi ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuonesha mafanikio mbalimbali ambayo Nchi imeyapata katika uhamasishaji wa matumizi ya nishati safi. Kwa ujumla, Wizara ilitumia Mkutano huo kama jukwaa la kimkakati katika jitihada za kuimarisha ushawishi katika mikakati ya kuendeleza miradi ya Sekta ya Nishati hususan inayolenga kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

**f) Ushiriki katika Mkutano Mkuu wa 69 wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki *(International Atomic Energy Agency – IAEA)***

79. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilishiriki Mkutano Mkuu wa 69 wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA) uliofanyika Vienna, Austria kuanzia tarehe 15 hadi 19 Septemba, 2025. Mkutano huo ulihusisha Nchi Wanachama 180 kujadili hatua zilizofikiwa katika matumizi salama ya nishati ya nyuklia katika afya, kilimo na

chakula. Tanzania imekuwa mwanachama wa IAEA tangu mwaka wa 1976, na tayari imesaini Mpango wa Nchi (CPF) wa mwaka 2023 hadi 2027 na Shirika hilo, unaotumika kama mwongozo wa ushirikiano wa kimkakati na kiufundi na IAEA, hususan katika kuendeleza na kukuza matumizi ya nishati ya nyuklia nchini. Kupitia Mkutano huo, Serikali ya Tanzania ilitumia nafasi yake ya uanachama kuelezea utayari wake wa kuanza kutumia nishati ya nyuklia kuzalisha umeme kwa kuzingatia miongozo, kanuni na sheria zilizowekwa na IAEA.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mkutano huo pia, Wizara ilifanya mikutano ya pembeni na Wadau mbalimbali wa nyuklia na kueleza lengo lake la kuzalisha umeme wa nyukilia. Maandalizi ya Mpango wa Tanzania kuanza kuzalisha umeme wa nyuklia yanaendelea, ambapo tayari uchambuzi umefanyika kuhusu masuala ya msingi ya kuzingatiwa ili kutekeleza azma hiyo, kuunda Kamati ya Kitaifa ya Kuratibu utekelezaji wa Mpango huo pamoja na kutoa mafunzo kwa wataalam wa ndani katika ngazi mbalimbali.

81. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika hilo la Kimataifa linakusudia kutuma Wataalam wake wa kiufundi ***(Mission for Integrated Nuclear Infrastructure Review)*** kwa ajili ya kufanya ukaguzi na mapitio ya miundombinu na matayarisho ya awali ili kutusaidia kufanya tathmini ya miundombinu iliyopo na kuona utayari wake katika uzalishaji wa umeme wa nyuklia kwa kutekeleza programu itakayohakikisha uzalishaji wa nishati hiyo unakuwa salama kwa binadamu na mazingira; wa uhakika na endelevu kwa kushirikisha wadau wote muhimu ikiwemo wanaohusika na udhibiti, uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme; na uwepo wa miundombinu wezeshi kama vile barabara na maji pamoja na Sera na Mipango madhubuti itakayosaidia uandaaji na utekelezaji wa programu madhubuti ya kuzalisha umeme wa nyuklia. Ujumbe huo unatarajiwa kuwasili nchini katika kipindi cha mwaka 2026/27.

## B 1.4: UTENDAJI WA KAMPUNI TANZU ZA TANESCO

### a) Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania *(*TGDC*)*

82. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Kampuni tanzu ya TANESCO ya TGDC imeendelea kutekeleza miradi ya kuendeleza rasilimali za jotoardhi nchini ukiwemo mradi wa Ngozi uliopo mkoani Mbeya ambao unatarajiwa kuzalisha Megawati 70. Hadi Machi, 2026, TGDC ilikuwa imeanza uchorongaji wa kisima cha kwanza cha jotoardhi (NZB3) ili kuhakiki kiwango na ubora wa rasilimali ya jotoardhi, kukamilisha tafiti na uhakiki unaoendelea pamoja na ununuzi na usimikaji wa mitambo (*turbines*). Gharama za utekelezaji wa mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 336** sawa na takriban **Shilingi bilioni 924.12**. Vilevile, hatua nyingine zilizochukuliwa ni kuendelea na taratibu za ununuzi wa Mshauri Mwelekezi atakayesimamia kuanza kwa uchorongaji wa visima katika mradi wa Kiejo-Mbaka uliopo mkoani Mbeya, kwa lengo la kuhakiki rasilimali ya jotoardhi katika eneo hilo.

### b) Kampuni ya Kuzalisha Nguzo za Umeme za Zege Tanzania *(TCPM)*

83. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Kampuni tanzu ya TANESCO ya TCPM imekamilisha ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza nguzo za zege kilichopo mkoani Tabora na kuanza uzalishaji wa nguzo hizo tarehe 18 Februari, 2026. Kukamilika kwa kiwanda hicho chenye uwezo wa kuzalisha nguzo 80 - 120 kwa siku ni mojawapo ya utatuzi wa kimkakati wa changamoto ya upatikanaji, usafirishaji na bei ya nguzo za zege hususan kwa mikoa ya Kanda za Magharibi, Ziwa na Kati. Vilevile, Serikali inakusudia kuanza ujenzi wa kiwanda cha pili mkoani Mbeya ambapo kwa sasa usanifu wa awali unaendelea. Pia, Serikali kupitia TCPM inaendelea kushirikiana na wazalishaji binafsi wa nguzo za zege kwa lengo la kuimarisha uzalishaji na usambazaji wa nguzo hizo na hivyo kukabiliana na ongezeko la uhitaji wake katika maeneo mbalimbali nchini.

### c) Kampuni ya Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Usafirishaji na Usambazaji Umeme (ETDCO)

84. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Kampuni tanzu ya TANESCO ya ETDCO imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji wa umeme nchini. Hadi Machi, 2026 miradi iliyokuwa inaendelea kutekelezwa ni pamoja na:

i. Mradi wa ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme katika vitongoji mkoani Mbeya ambao umefikia asilimia 83 na unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2027;

ii. Mradi wa usambazaji wa umeme katika maeneo ya Kilindi na Simanjiro ambao unahusisha ujenzi wa miundombinu ya usambazaji umeme katika maeneo ya makazi ya wananchi; na

iii. Mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 220 ya Masasi – Mahumbika pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme, ambapo Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA) pamoja na kuweka

mipaka (*demarcation)* ya njia ya kusafirisha umeme vimekamilika na kazi ya usanifu (*design)* inaendelea. Gharama za mradi huu ni **Shilingi bilioni 210.02.**

## B 1.5: MIRADI YA NISHATI VIJIJINI

85. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) imeendelea na utekelezaji wa miradi ya kusambaza nishati vijijini, ikiwa ni pamoja na miradi ya kusambaza umeme vitongojini, mradi wa kufunga na kusambaza mifumo ya kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya jua katika makazi yaliyo vijijini na maeneo yaliyo mbali na Gridi ya Taifa ikiwemo visiwa vya Tanzania Bara pamoja na ujenzi wa vituo vya mafuta vijijini. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi hii ni kama ifuatavyo:

### a) Mradi wa Kupeleka Umeme katika Vitongoji Awamu ya Pili B *(Hamlet Eletrification Project – HEP IIB)*

86. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kuhakikisha kuwa vitongoji vyote Tanzania Bara vinafikishiwa

umeme ifikapo mwaka 2030/31. Ikiwa ni utekelezaji wa azma hiyo, tarehe 17 Januari, 2026 Serikali kupitia REA ilisaini Mikataba 30 na Kampuni 17 (za ndani 11 na za nje 6) kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi mahsusi wa kupeleka umeme katika Vitongoji 9,009 kwenye mikoa 25 (ukiondoa Dar es Salaam). Kwa sasa Wakandarasi wanaendelea na usanifu wa kina na kuandaa michoro katika maeneo ya mradi, ikiwa ni hatua za awali kabla ya kuagiza vifaa vya mradi na kuanza utekelezaji. Mradi huu unagharimu jumla ya **Shilingi trilioni 1.416** na unahusisha ujenzi wa njia za umeme wa msongo wa kati (kilovoti 33) zenye urefu wa kilomita 13,181; njia za msongo mdogo (kilovoti 0.4/0.23) zenye urefu wa kilomita 14,016; ufungaji wa transfoma 9,009 zenye uwezo wa kVA100 na kVA200; na kuunganisha wateja wa awali 290,300.

**b) Mradi wa Kuunganisha Wateja Vitongojini – *Universal Hamlet Electrification and Last Mile Customers Connection***

87. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA imeanza utekelezaji wa mradi wa kuongeza uunganishaji wa wateja katika vitongoji *(Universal Hamlet Electrification and Last Mile Customers Connection)* ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Mahsusi wa Nishati wa Taifa *(National Energy Compact)* ulioridhiwa katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika (*Mission 300*) mwezi Januari, 2025. Serikali kupitia REA imeanza utekelezaji wa mradi huu katika mikoa mitatu ya Pwani, Morogoro na Dodoma ambao unalenga kusambaza umeme katika jumla ya mitaa 279. Hadi Machi, 2026 taratibu za kuwapata Wakandarasi wa kutekeleza mradi huu zilikuwa zimekamilika na mikataba kusainiwa.

c) **Mradi wa Kusambaza Umeme katika Vitongoji Awamu ya Pili A – *(Hamlet Electrification Project – HEP IIA*)**

88. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa kilomita 528 za njia za umeme msongo wa kati na kilomita 6,158 za njia za umeme msongo mdogo pamoja na kufunga transfoma 3,056 ili kufikisha umeme kwenye vitongoji 3,060 sawa na vitongoji 15 kwa kila Jimbo pamoja na kuunga wateja wa awali 101,106. Hadi Machi, 2026 njia za umeme za msongo wa kati zenye urefu wa kilomita 371, na njia za msongo mdogo zenye urefu wa kilomita 5,408 zilikuwa zimejengwa. Aidha, maeneo 2,089 na wateja wa awali 29,326 walikuwa wamefikishiwa huduma za umeme. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 80**.

d) **Mradi wa Kupeleka Umeme katika Vitongoji vya Mikoa ya Songwe na Kigoma**

89. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kupeleka umeme katika vitongoji 667 katika mikoa ya Songwe (vitongoji 307) na Kigoma (vitongoji 360). Mradi unahusisha pia ujenzi wa njia za umeme msongo wa kati

zenye urefu wa kilomita 698; ujenzi wa njia za umeme msongo mdogo zenye urefu wa kilomita 1,336; ufungaji wa transfoma 694 pamoja na kuunganisha wateja wa awali 20,622. Hadi Machi, 2026 njia za umeme za msongo wa kati zenye urefu wa kilomita 683, na njia za umeme msongo mdogo zenye urefu wa kilomita 1,317 zilikuwa zimejengwa. Aidha, jumla ya vitongoji 661, Songwe (vitongoji 301) na Kigoma (vitongoji 360) vimeunganishwa na jumla ya wateja wa awali 10,523 wameunganishiwa umeme. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 97**.

### e) Mradi wa Kusambaza Umeme katika Vijiji-Miji (*Peri Urban III*)

90. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kusambaza umeme katika vijiji-miji, mitaa na vitongoji 516 ambavyo havijafikiwa na miundombinu ya umeme katika maeneo ya pembezoni mwa miji katika mikoa nane (8) ambayo ni Geita, Kigoma, Kagera, Mbeya, Mtwara, Singida, Tabora na Tanga. Mradi pia unahusisha ujenzi wa njia za umeme wa msongo wa kati zenye urefu wa kilomita 467; ujenzi wa njia za umeme wa msongo mdogo zenye urefu wa kilomita 1,178; ufungwaji wa transfoma 484

pamoja na kuunganisha wateja wa awali 24,463. Hadi Machi, 2026 maeneo 511 yalikuwa yamefikiwa na umeme na wateja 16,620 kati ya 24,463 wameunganishiwa umeme. Utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia wastani wa **asilimia 97**.

### f) Mradi wa Kupeleka Umeme katika Maeneo ya Migodi Midogo, Viwanda na Maeneo ya Kilimo katika Mikoa ya Ruvuma, Njombe, Mbeya na Rukwa

91. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa kilomita 1,396 za msongo wa kati na kilomita 1,010 za msongo mdogo pamoja na kufunga transfoma 621 ili kufikisha umeme katika migodi midogo, viwanda na maeneo ya kilimo 619 pamoja na wateja wa kawaida 13,011. Hadi Machi, 2026 ujenzi wa njia za kusambaza umeme wa msongo wa kati zenye urefu wa kilomita 1,396.42 na njia za msongo mdogo zenye urefu wa kilomita 987.15 zilikuwa zimejengwa. Aidha, maeneo 594 na wateja 6,869 walikuwa wamefikishiwa umeme ambapo kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 94**.

## g) Mradi wa Kusambaza Umeme katika Vitongoji vya Mkoa wa Lindi

92. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu ni mahsusi kwa ajili ya kusambaza umeme katika vitongoji vya Mkoa wa Lindi. Mradi unahusisha ujenzi wa kilomita 352.45 za njia za umeme msongo wa kati na kilomita 430 za njia za umeme msongo mdogo pamoja na kufunga transfoma 230 ili kufikisha umeme katika vitongoji 230 na kuunga wateja wa awali 7,590. Hadi Machi, 2026 mkandarasi alikuwa amesimika nguzo za msongo wa kati kilomita 304 kati ya kilomita 352.5 na kilomita 411 kati ya kilomita 429.9 za msongo mdogo, na kazi za uvutaji wa nyaya na ufungaji wa transfoma pamoja na uwashaji wa vitongoji zimeanza. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 46**.

## h) Mradi wa Kuwezesha Waendelezaji Binafsi wa Miradi ya Nishati katika Maeneo Yaliyo Mbali na Ambayo Hayajafikiwa na Gridi ya Taifa

93. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa maeneo yaliyo mbali na Gridi ya Taifa yanafikiwa na huduma za umeme, Serikali kupitia REA imewezesha waendelezaji

binafsi kutekeleza miradi mbalimbali ya nishati jadidifu inayotokana na nguvu za jua, upepo, maji na tungamotaka katika maeneo ambayo yapo nje ya Gridi ya Taifa ikiwemo visiwani, kwa kuwapatia ruzuku na mikopo ya masharti nafuu. Miradi inayotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa gridi ndogo na uunganishaji wateja na mifumo inayojitegemea ya umeme jua. Ruzuku zinazotolewa kwa waendelezaji binafsi zinahusu maandalizi ya miradi; ujenzi wa miradi; na ufadhili wa mradi wa nishati jadidifu kwa utaratibu wa malipo kwa matokeo. Aidha, Serikali kupitia REA inatoa mikopo ya riba nafuu kwa ajili ya uendelezaji wa miradi.

94. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia programu hii miradi inayotekelezwa ni kama ifuatavyo:

**(i) Mradi wa Kusambaza Mifumo ya Jua Inayojitegemea *(Solar Home System - SHS)* katika Makazi 20,000**

95. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha usambazaji na ufungaji wa mifumo ya jua inayojitegemea *(Solar Home System - SHS)* katika makazi 20,000 katika

visiwa vidogo 143 vilivyopo katika Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika unaofadhiliwa na Benki ya Dunia kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 4** sawa na takriban **Shilingi bilioni 11** kupitia Mpango wa *Tanzania Rural Electrification Expansion Program - TREEP*. Aidha, Serikali kupitia REA ilisaini mikataba na watoa huduma sita (6) (Greenleaf Technology Solution Company Ltd, Trinity Solar Energy Ltd, L'S Solution Ltd, Rafiki Energy Ltd, JV: Star Media (T) Ltd & Kangala Engineering Co. Ltd pamoja na Volt Africa Limited) kwa ajili ya kutekeleza mafungu 17 ya mradi huo ambao watasambaza mifumo 20,000 ambapo hadi Machi, 2026 jumla ya makazi 1,302 yamefungiwa mifumo na wananchi wanaendelea kupata huduma.

**(ii) Mradi wa Kuwezesha Upatikanaji Umeme kwa Matokeo Awamu ya Pili Kupitia Gridi Ndogo**

96. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA imeendelea na utekelezaji wa Mpango wa Malipo kwa Matokeo Awamu ya Pili (*Result Based Financing - RBF II)* ili kusambaza nishati katika maeneo ya

vijijini. Mpango huu unafadhiliwa na Serikali za Sweden na Uingereza. Aidha, baada ya kukamilika kwa RBF I, Serikali kupitia REA ilitoa fursa kwa waendelezaji wa miradi ya umeme kupitia vyanzo vya nishati jadidifu kuomba ufadhili ambapo waendelezaji wanne (4) ambao ni Mwenga Hydro Limited (Mufindi), Luponde Hydro (Njombe), Volt Africa (Ukerewe) na Matembwe Village (Njombe) wamejitokeza kuwekeza katika miradi ya kuanzisha gridi ndogo au kuunga wateja wapya kwenye gridi ndogo zinazofanya kazi. Jumla ya gharama za miradi yote ni **Dola za Marekani milioni 8.5** sawa na takriban **Shilingi bilioni 23.39** na Serikali itachangia **Dola za Marekani milioni 3.56** sawa na takriban **Shilingi bilioni 9.79** ambapo wateja wa awali 6,063 katika vijiji 44 watаunganishiwa huduma za umeme.

**(iii) Mradi wa Kuwezesha Ujenzi wa Vituo Vidogo vya Kusambaza Bidhaa za Mafuta ya Petroli Vijijini**

97. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA inalenga kusogeza huduma ya bidhaa za mafuta ya petroli kwa wananchi katika

maeneo ya vijijini kwa kutoa mikopo kwa waendelezaji wa vituo hivyo ili waweze kujenga vituo husika katika maeneo ya vijijini. Maeneo yanayolengwa ni yale yaliyopo umbali usiopungua kilomita saba (7) kutoka barabara za TANROADS na kusiwe na kituo kingine cha mafuta. Kiasi cha juu cha mkopo kinachotolewa ni **Shilingi 133,000,000.00** ambazo zitarejeshwa kwa kipindi kisichozidi miaka saba (7) kwa riba ya **asilimia 5**.

98. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuendelea kupokea maombi kutoka kwa waombaji, kuyachambua na kuyawasilisha Benki maombi yanayokidhi vigezo kwa ajili ya kufanyiwa tathmini ya kifedha. Jumla ya maombi 32 yamepokelewa katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 ambapo maombi 11 yaliwasilishwa Benki kwa kuwa yalikidhi vigezo vilivyotolewa na REA. Aidha, Benki ya Azania baada ya kupitia maombi hayo inaendelea na zoezi la utoaji wa mikopo kwa waendelezaji watatu (3) wa miradi waliokidhi vigezo vya kibenki vya kupata mikopo ya kuendeleza miradi hiyo. Serikali kupitia REA inaendelea

kupokea maombi ya mikopo kutoka kwa waendelezaji.

## B 1.6: UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA TAIFA WA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

99. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, inaendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 - 2034) uliozinduliwa Mei, 2024. Lengo la Mkakati huo ni kuhakikisha kuwa angalau asilimia 80 ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034. Ili kufikia lengo hilo, Mkakati umejikita katika kupunguza gharama za nishati, vifaa na majiko sanifu ya kupikia; kuimarisha upatikanaji wa malighafi na miundombinu ya uhakika ya nishati safi ya kupikia; na kuandaa, kuhuisha na kuoanisha Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo wezeshi ya kufanikisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

100. ***Mheshimiwa Spika,*** Mkakati umejikita pia katika kuhamasisha uwekezaji katika nishati safi ya kupikia; kuongeza wigo wa tafiti na bunifu za teknolojia

zinazohusu nishati safi ya kupikia; na kuimarisha uelewa wa jamii kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia. Kutokana na jitihada zinazotekelezwa, kiwango cha watanzania wanaotumia nishati safi ya kupikia kimeongezeka kutoka **asilimia 6.9** mwaka 2021 hadi kufikia **asilimia 28.6** ya watanzania wenye nishati safi ya kupikia mwaka 2025. Kazi zilizofanyika katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 ni pamoja na:

### a) Utoaji wa Elimu Kuhusu Umuhimu wa Nishati Safi ya Kupikia

101. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuhamasisha wananchi katika maeneo ya mijini na vijijini kutumia nishati safi ya kupikia. Uhamasishaji huo umefanyika kupitia vyombo vya habari ikiwemo redio na televisheni, mitandao ya kijamii, makongamano, maonesho, warsha na mikutano ya hadhara. Aidha, ili kuimarisha utoaji wa elimu kwa wananchi, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo pamoja na Sekta Binafsi inaendelea na shughuli za

uhamasishaji wa matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa wananchi *(community outreach)* katika mikoa yote nchini.

**b) Ujenzi wa Miundombinu ya Kusambaza Gesi Asilia kwa Ajili ya Kupikia katika Mikoa ya Pwani na Lindi**

102. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unatekelezwa na TPDC kwa kushirikiana na REA na unahusisha ujenzi wa mabomba ya kusambaza gesi asilia yenye urefu wa kilomita 44.4 pamoja na kuunganisha gesi asilia kwenye nyumba 1,000 katika maeneo yanayopitiwa na bomba hilo hususan kwa mikoa ya Lindi na Pwani. Hadi Machi, 2026 ujenzi wa kilomita 28 umekamilika na nyumba 471 pamoja na shule moja (1) zimeunganishiwa mfumo wa matumizi ya gesi asilia kwa ajili ya kupikia katika eneo la Mnazi Mmoja – Lindi na nyumba 530 katika Mkoa wa Pwani eneo la Kisemvule – Mkuranga zimeunganishwa na miundombinu ya gesi asilia kwa ajili ya kupikia.

### c) Usambazaji wa Mitungi ya Gesi ya LPG (*LPG Starter Packs*)

103. ***Mheshimiwa Spika,*** mpango huu unahusisha usambazaji wa mitungi 452,455 ya LPG ya kilo 6 pamoja na vichomeo *(burners*) na figa (*trivet*) kwa bei ya ruzuku ya **asilimia 50**. Hadi Machi, 2026 jumla ya mitungi 346,251 sawa na **asilimia 76.5** ya mitungi yote iliyo katika mpango huu imesambazwa kwa wananchi katika maeneo mbalimbali nchini.

### d) Usambazaji wa Majiko Banifu kwa Bei ya Ruzuku

104. ***Mheshimiwa Spika,*** mpango huu unahusisha usambazaji wa majiko banifu 200,000 katika maeneo ya vijijini na pembezoni mwa miji katika mikoa yote ya Tanzania Bara kwa bei ya ruzuku kati ya asilimia 80 hadi asilimia 85. Gharama ya mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 6** sawa na takriban **Shilingi bilioni 16.50** kupitia mpango wa *Tanzania Rural Electrification Expansion Program – TREEP*. Hadi Machi, 2026 Serikali kupitia REA ilikuwa imesambaza jumla ya majiko banifu

49,136 pamoja na majiko janja ya umeme (*induction cookers*) 7,292.

### e) Ufungaji wa Mifumo ya Nishati Safi ya Kupikia katika Taasisi Zinazohudumia Watu Zaidi ya 100

105. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatekeleza mpango wa usambazaji wa nishati safi ya kupikia kwa taasisi kubwa zinazolisha zaidi ya watu 100 kwa siku nchini. Kipaumbele cha utekelezaji wa programu hii kimeanza kwa kuhakikisha taasisi za elimu, afya na huduma za kijamii zinapata suluhisho kwa kufungiwa miundombinu ya nishati safi ya kupikia. Kwa kuanzia, Serikali ilitekeleza programu hii katika taasisi za magereza, kambi za Jeshi la Kujenga Taifa, Shule za Sekondari na Chuo cha VETA Mtwara. Hadi Machi, 2026 jumla ya taasisi 1,350 zinazohudumia zaidi ya watu 100 kwa siku zimehamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia.

## B.2 SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ASILIA

106. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta hii inajumuisha mnyororo mzima wa thamani wa mafuta na gesi asilia; ikihusisha mkondo wa juu (utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia) na mkondo wa kati na chini (uchakataji, usafirishaji na usambazaji wa mafuta na gesi asilia). Aidha, sekta hii inahusisha pia ujenzi wa miundombinu ya kimkakati ya usafirishaji, uhifadhi na biashara ya mafuta na gesi asilia. Katika mwaka 2025/26 Serikali iliendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuendeleza Sekta hii ambapo mafanikio mbalimbali yaliweza kupatikana.

### B.2.1 MIRADI YA UENDELEZAJI NA UZALISHAJI WA GESI ASILIA

107. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki uzalishaji wa gesi asilia uliendelea kwenye vitalu viwili (2) vya Mnazi Bay na Songo Songo ambavyo ndivyo vinavyozalisha nishati hiyo kwa sasa. Aidha, hatua zilichukuliwa katika uendelezaji wa vitalu vya gesi asilia ambavyo tayari kuna ugunduzi vya Ruvuma

(Ntorya) pamoja na vilivyopo baharini (Kitalu Na. 1, 2 na 4) kwa ajili ya mradi wa LNG. Hatua ya utekelezaji ni kama ifuatavyo:

**a) Kitalu cha Uzalishaji wa Gesi Asilia cha Mnazi Bay**

108. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa gesi asilia katika kitalu hiki kilichopo katika Mkoa wa Mtwara uliendelea ambapo wastani wa futi za ujazo bilioni (bcf) 23.60, sawa na wastani wa futi za ujazo milioni 110 kwa siku (mmscfd) zilizalishwa. Utekelezaji wa mpango wa kuchoronga visima vitatu (viwili vya uzalishaji [MB-5 na MS-2] na kimoja cha utafutaji [KASA-1]) umeendelea. Hadi Machi 2026, uchorongaji wa kisima kimoja (MB-5) cha uzalishaji ulikamilika na sasa uzalishaji wa majaribio unaendelea katika kisima hicho. Aidha, uchorongaji wa kisima cha pili (MS-2) umefikia asilimia 40 na utakamilika mwishoni mwa mwezi Mei, 2026. Ukamilishaji wa shughuli za uchorongaji wa visima vyote vitatu unatarajiwa kuongeza uzalishaji wa gesi asilia kwa kiasi cha futi za ujazo milioni 45 hadi 55 kwa siku.

**b) Kitalu cha Uzalishaji wa Gesi Asilia cha Songo Songo**

109. ***Mheshimiwa Spika,*** Kitalu cha uzalishaji wa gesi asilia cha Songo Songo kimeendelea na uzalishaji wa wastani wa futi za ujazo bilioni (bcf) 17.9 sawa na futi za ujazo milioni 84.7 kwa siku (mmscfd) kulingana na mahitaji. Aidha, kufuatia leseni ya kitalu hiki kufikia ukomo mwezi Oktoba, 2026 Serikali inaendelea kufanya majadiliano na Mwekezaji kwa lengo la kuhuisha muda wa leseni kwa kipindi cha pili cha uendelezaji wa gesi asilia katika kitalu hiki.

**c) Kitalu cha Ruvuma (Eneo la Ntorya)**

110. ***Mheshimiwa Spika,*** maandalizi ya uzalishaji wa gesi asilia katika Kitalu cha Ruvuma kilichopo eneo la Ntorya mkoani Mtwara yanaendelea. Kazi zilizofanyika hadi Machi, 2026 ni pamoja na kuanza ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia lenye urefu wa kilomita 34.20 kutoka Ntorya hadi Kiwanda cha kuchakata gesi asilia cha Madimba. Gharama za ujenzi wa bomba hilo

ni **Shilingi bilioni 106** ambapo kwa sasa utekelezaji wake umefikia **asilimia 37**. Aidha, maandalizi ya uchorongaji wa kisima cha uzalishaji cha Chikumbi-1 yanaendelea. Vilevile, taratibu za kuwapata wakandarasi kwa ajili ya majaribio ya uzalishaji wa kisima cha Ntorya-2 pamoja na marekebisho ya kisima cha Ntorya-1 zinaendelea.

111. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2026 ambapo kukamilika kwake kutawezesha uzalishaji wa gesi asilia kwa kuanzia na kiasi cha futi za ujazo milioni 40 hadi 60 kwa siku (mmscfd) na kuongezeka hadi kufikia futi za ujazo milioni 140 kwa siku pindi uendelezaji zaidi utakapokamilika.

### d) Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika *(Liquefied Natural Gas – LNG)*

112. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kusindika gesi asilia iliyogunduliwa katika Vitalu namba 1, 2 na 4 vilivyopo katika kina kirefu cha bahari ili kuwa kimiminika kwa ajili ya kuuzwa katika masoko ya kimataifa na matumizi ya ndani

ya nchi. Hadi Machi, 2026 Serikali na wawekezaji wa mradi wameendelea na majadiliano katika maeneo mbalimbali ya mradi huo ambapo makubaliano yamefikiwa katika maeneo ya kibiashara na kikodi.

Kwa sasa majadiliano hayo yapo katika hatua za ukamilishwaji wa masuala ya kisheria kwa pande zote mbili za majadiliano ambapo kwa upande wa Serikali suala hilo linaratibiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, Serikali imekwishatwaa eneo la mradi baada ya kukamilika kwa taratibu za ulipaji wa fidia kwa wananchi na pia imeendelea kutekeleza miradi ya uwajibikaji kwa jamii (CSR) kwa kushirikiana na wabia wa mradi, ikiwemo ujenzi wa Shule ya Msingi Likong'o mkoani Lindi.

### B.2.2 MIRADI YA UTAFUTAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA KATIKA VITALU VYA KIMKAKATI

113. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC iliendelea na utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vinne (4) vya kimkakati kama ifuatavyo:

### a) Kitalu cha Eyasi – Wembere

114. ***Mheshimiwa Spika,*** Kitalu hiki kipo kwenye Bonde la Ufa la Afrika Mashariki, Kaskazini Mashariki mwa Tanzania katika mikoa ya Arusha, Manyara, Shinyanga, Simiyu, Singida na Tabora. Hadi Machi, 2026 kazi za mradi zilizotekelezwa ni pamoja na kukamilisha uchukuaji wa taarifa za mitetemo za mfumo wa 2D za urefu wa kilomita 484.70. Aidha, kazi za uchukuaji wa taarifa za mitetemo aina ya 2D zenye urefu wa kilomita 914 zinaendelea na hadi sasa zimefikia **asilimia 67.72** ya utekelezaji. Pia, uchakataji wa taarifa za mitetemo kilomita 1,174.70 umeshaanza na unaendelea (zaidi ya kilomita 690 zimeshaanza kufanyiwa kazi). Matokeo ya tathmini ya taarifa hizi zinazokusanywa yatawezesha kufahamu eneo lenye mashapo yanayohifadhi mafuta, hivyo kuwezesha uchorongaji wa kisima cha utafiti katika eneo hilo. Vilevile, Serikali kupitia TPDC inaendelea kumtafuta Mbia mwenye uzoefu, utaalamu na fedha wa kushirikiana naye katika kuendeleza kazi za kitalu hiki.

### b) Kitalu cha Lindi – Mtwara

115. ***Mheshimiwa Spika,*** Kitalu cha Lindi–Mtwara ni eneo maalum lililotengwa kwa ajili ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia lililopo katika Halmashauri za Wilaya ya Mtwara na Mtama. Hadi Machi, 2026 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuendelea na zoezi la uchukuaji wa taarifa za mitetemo katika mfumo wa 3D kwa eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 736 ambao umefikia **asilimia 31.6**. Aidha, kazi ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii inaendelea na imefikia **asilimia 90**; na kazi za utambuzi na uthamini wa mali zitakazoathiriwa na ujenzi wa njia na mkuza wa pembezoni zimefikia **asilimia 52**. Vilevile, maandalizi ya uchakataji na tafsiri ya taarifa ili kubaini maeneo yenye mashapo yanayofaa kwa ajili ya kuchoronga visima vya utafutaji yanaendelea. Kazi hizi za awali hadi kukamilika kwake, zitagharimu takriban **Shilingi bilioni 86.56**.

### c) Kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini

116. ***Mheshimiwa Spika,*** Kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini kipo baharini, Kusini Mashariki mwa Tanzania. Hadi Machi, 2026 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kufanyika kwa stadi na tafiti za awali katika kitalu, mapitio ya taarifa za mitetemo za mfumo wa 3D (*3D seismic data*) zenye urefu wa kilomita za mraba 131 zilizofanyika hapo awali na kubaini viashiria vya uwepo wa mafuta au gesi asilia katika kitalu hicho. Aidha, mpango wa uchorongaji kisima (*drilling plan*) umekamilika. Serikali kupitia TPDC inaendelea na taratibu za kumtafuta mbia wa kimkakati mwenye uzoefu, utaalamu na fedha za uchorongaji wa kisima cha utafutaji ili kushirikiana naye katika uendelezaji wa kitalu hiki.

### d) Kitalu cha Songo Songo Magharibi

117. ***Mheshimiwa Spika,*** Kitalu cha Songo Songo Magharibi kipo katika kina kifupi cha bahari, Magharibi mwa Kitalu cha Uzalishaji cha Songo Songo. Hadi Machi, 2026 kazi zilizoendelea kufanyika ni pamoja na Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii

(ESIA) kwa ajili ya ukusanyaji wa taarifa za mitetemo. Aidha, taratibu za kumpata mkandarasi wa kukusanya taarifa za mitetemo zenye urefu wa kilomita 240 zimekamilika na pia Serikali kupitia TPDC inaendelea na utafutaji wa mbia wa kimkakati mwenye uzoefu na utaalamu wa kiteknolojia na fedha atakayeshirikiana na TPDC katika hatua ya kuchoronga kisima cha utafutaji.

### B.2.3 MIRADI YA USAFIRISHAJI NA USAMBAZAJI WA GESI ASILIA

118. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali iliendelea na utekelezaji wa miradi ya usafirishaji na usambazaji wa gesi asilia ndani na nje ya nchi, ambapo hatua za utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

#### a) Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani

119. ***Mheshimiwa Spika,*** usambazaji wa gesi asilia katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani umekuwa ukifanyika kwa njia mbili ambazo ni kwa njia ya mabomba na katika mfumo wa gesi iliyoshindiliwa (CNG) na kusafirishwa kwa kutumia malori

*(CNG tube trailer trucks)*. Hadi Machi, 2026 Serikali kupitia TPDC ilikamilisha uunganishaji wa mfumo wa mawasiliano (SCADA) kati ya kituo kikuu cha CNG kilichopo eneo la Mlimani City (*mother station*) na vituo vya kusambazia gesi asilia (*daughter stations*) vilivyopo Muhimbili na Kibaha. Aidha, Serikali kupitia TPDC imeendelea na uendeshaji wa kituo kikuu cha CNG cha Mlimani City pamoja na kuuza gesi asilia kupitia kituo hicho chenye uwezo wa kuhudumia hadi **bajaji 2,000**, **magari madogo 1,200**, **mabasi makubwa 60** pamoja na magari ya kusafirishia gesi iliyoshindiliwa ***(CNG tube trailers)*** **10** kwa siku.

120. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na bei za mafuta zisizotabirika kwenye Soko la Dunia, Serikali ya Awamu ya Sita pamoja na mambo mengine, imeendelea na jitihada za kuhakikisha kuwa matumizi ya CNG katika vyombo vya moto yanaendelea kuimarika nchini. Ikiwa ni utekelezaji wa azma hiyo, Serikali kupitia TPDC kwa kushirikiana na Sekta Binafsi imewezesha ujenzi wa vituo 18 vya CNG ambavyo vinaendelea kutoa huduma, na vituo vingine nane (8) vipo katika hatua za ujenzi.

121. ***Mheshimiwa Spika,*** uwepo wa miundombinu hiyo umeendelea kuhamasisha wamiliki wa vyombo vya usafiri kuongeza mifumo ya matumizi ya gesi asilia kwenye vyombo hivyo. Hadi sasa kuna jumla ya vyombo vya usafiri na usafirishaji zaidi ya 20,000 vinavyotumia gesi asilia vikihusisha magari madogo, magari makubwa, malori, mabasi ya abiria (yakiwemo ya mwendokasi) na bajaji. Vilevile, hadi Machi, 2026 zaidi ya kampuni binafsi 86 za ndani na nje ya nchi zilikuwa zimepewa idhini ya kuwekeza katika mnyororo wa thamani wa gesi asilia nchini.

122. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuchochea matumizi ya gesi asilia kwenye vyombo vya usafiri, Serikali ilishaondoa kodi ya ushuru wa forodha kwa magari yanayoagizwa yakiwa yameshafungwa mfumo wa matumizi ya gesi asilia na inaendelea kufanyia kazi mapendekezo ya punguzo la kodi kwenye vifaa vinavyotumika kwenye uongezaji wa mfumo wa matumizi ya gesi asilia kwenye magari. Aidha, kupitia uhamasishaji mkubwa wa matumizi ya gesi asilia uliofanywa na Serikali, Sekta Binafsi imeendelea kuwekeza katika Karakana za kufunga mfumo wa

matumizi ya gesi asilia kwenye vyombo vya usafiri ambapo hadi sasa kuna jumla ya karakana 13.

123. ***Mheshimiwa Spika,*** Ongezeko la karakana hizi limesaidia kupungua kwa gharama za uwekaji wa mifumo ya matumizi ya gesi asilia kwenye magari ambapo kwa sasa, kwa magari madogo gharama ni kati ya Shilingi **1,500,000** hadi **1,800,000** ikilinganishwa na awali ilipokuwa Shilingi **2,000,000** hadi **2,500,000.** Katika hatua nyingine, Serikali kupitia TPDC imejenga Karakana na kuikabidhi kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambapo pamoja na kazi ya kuweka mifumo ya matumizi ya gesi kwenye vyombo vya usafiri, Karakana hiyo imekuwa sehemu ya mafunzo ya kuandaa vijana watakaoongeza wataalam wa eneo hili watakaoweza kujiajiri na kuongeza Karakana binafsi nyingi zaidi.

124. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa usambazaji wa CNG unafikia maeneo mengi ya nchi, Serikali kupitia TPDC ipo katika hatua za ununuzi wa vituo vitano (5) vya CNG vinavyohamishika (*Mobile CNG stations*) ambapo utengenezaji wa vituo

hivyo unaendelea. Vituo hivyo vinatarajiwa kuwekwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma kwa awamu ya kwanza na mikoa ya Arusha, Tanga na Kilimanjaro kwa awamu ya pili. Aidha, katika kuhakikisha kuwa gesi asilia inafika maeneo mbalimbali ya nchi yaliyo mbali na miundombinu ya gesi kwa sasa, Serikali kupitia TPDC imeingia makubaliano ya awali na kampuni binafsi sita (6) kwa ajili ya uendelezaji wa miradi ya Min – LNG nchini ili kuhakikisha matumizi ya gesi asilia yanafika maeneo mengi ya nchi.

**b) Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Gesi Asilia Kuanzia Kinyerezi - Dar es Salaam hadi Chalinze – Pwani**

125. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC imeanza maandalizi ya ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Kinyerezi - Dar es Salaam hadi Chalinze – Pwani, ili kuimarisha usambazaji wa gesi asilia katika maeneo ya kongani ya viwanda Zegereni – Kibaha, viwanda vya Mlandizi, Bandari kavu ya Kwala na Chalinze. Hadi Machi, 2026 Mshauri Mwelekezi alikuwa anaendelea na kazi ya upembuzi wa kina wa

njia ya kupitisha bomba hilo. Gharama za utekelezaji wa mradi huu zinakadiriwa kuwa **Shilingi bilioni 300.**

### c) Mradi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Asilia kutoka Tanzania hadi Uganda

126. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda ziliendelea na maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Asilia kutoka Tanzania hadi Uganda. Hadi Machi, 2026, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kusainiwa kwa mkataba baina ya Tanzania na Uganda *(Bilateral Agreement)* wa namna ya utekelezaji wa mradi katika hatua ya Upembuzi Yakinifu; na kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya Upembuzi Yakinifu huo.

### d) Mradi wa Kusafirisha Gesi Asilia Kutoka Dar es Salaam (Tanzania) hadi Mombasa (Kenya)

127. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Kenya ziliendelea na

maandalizi ya utekelezaji wa mradi huu, ambapo kazi zilizotekelezwa ni pamoja na Wataalamu kuendelea kuboresha nyaraka za maridhiano kwa ajili ya kuidhinisha nyaraka muhimu za kumpata Mshauri Mwelekezi atakayefanya Upembuzi Yakinifu wa mradi.

### B.2.4 MIRADI YA KUHIFADHI, KUSAFIRISHA NA BIASHARA YA MAFUTA

128. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya kuhifadhi na kusafirisha mafuta nchini kama ifuatavyo:

a) **Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani (Tanga) Tanzania (*East African Crude Oil Pipeline - EACOP)***

129. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mradi huu umeendelea katika mwaka 2025/26 ambapo kwa ujumla umefikia **asilimia 82.6**. Aidha, kazi zilizotekelezwa katika kipindi hiki ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa kambi 14 zinazotumika kwa ajili

ya wafanyakazi na hifadhi ya mabomba. Vilevile, ujenzi wa vituo vinne (4) vya kuongeza msukumo wa mafuta *(pump stations)* na vituo viwili (2) vya kupunguza msukumo wa mafuta *(pressure reduction stations)* umekamilika kwa **asilimia 74.60.** Pia, ujenzi wa miundombinu ya matenki ya kupokelea na kuhifadhi mafuta katika eneo la Chongoleani, Tanga umekamilika kwa **asilimia 89.20** na ujenzi wa miundombinu ya kituo cha kupokea mafuta (*terminal*) umekamilika kwa **asilimia 60.90**. Aidha, ujenzi wa Ghati pamoja na miundombinu ya kupakilia mafuta ghafi kwenye meli (*Load off Facility - LoF*) umefikia **asilimia 88.10;** na kiwanda cha kuweka mifumo ya upashaji na utunzaji joto (*Thermal Insulation System - (TIS) plant*) katika Kijiji cha Sojo, Wilaya ya Nzega kimekamilisha kazi kwa mabomba yote ya mradi yenye urefu wa kilomita 1,462. Gharama za utekelezaji wa mradi huu ni **Dola za Marekani bilioni 5.65** sawa na takriban **Shilingi trilioni 15.54.**

### b) Mradi wa Uanzishwaji wa Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta (*Strategic Petroleum Reserve - SPR*)

130. ***Mheshimiwa Spika,*** katika miaka ya karibuni Dunia imeshuhudia migogoro ya kisiasa, vita na changamoto za kiusalama, hususan katika kanda za nchi zinazozalisha mafuta ya petroli kwa wingi duniani. Hali hiyo imekuwa ikiathiri mnyororo wa upatikanaji wa bidhaa hizo kwa nchi mbalimbali, ikiwemo Tanzania na kusababisha bei za bidhaa hizo kuongezeka na hivyo kuathiri shughuli za kiuchumi na kijamii katika nchi husika. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali inakusudia kujenga kituo kikubwa cha kupokea na kuhifadhi mafuta jijini Dar es Salaam ili kuendelea kuhakikisha usalama na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za petroli nchini pamoja na nchi jirani *(petroleum hub)*. Aidha, Serikali imekamilisha andiko la mradi wa uanzishaji wa hifadhi ya kimkakati ya mafuta (SPR) na inaendelea na uboreshaji wa nyaraka mbalimbali za kisheria zitakazowezesha uanzishwaji na uendeshaji wa hifadhi ya mafuta ya kimkakati.

### c) Mradi wa Ukarabati wa Tenki Namba 8 Kigamboni

131. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC imekamilisha taratibu za kumpata mkandarasi wa ukarabati wa Tenki Na. 8 ambapo majadiliano na mkandarasi huyo yamekamilika. Aidha, Mshauri Mwelekezi wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira zitokanazo na ukarabati wa Tenki hilo amekamilisha kazi hiyo na TPDC imepata cheti cha Mazingira toka Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC). Vilevile, zabuni ya kumpata mkandarasi atakayefanya kazi ya kuondoa mabaki ya mafuta ghafi (*sludge disposal*) imekamilika.

### d) Ushiriki wa TPDC katika Biashara ya Mafuta kupitia Mfumo wa Uagizaji kwa Pamoja (*Bulk Procurement System - BPS*)

132. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 TPDC imeendelea kushiriki katika zabuni za kila mwezi za uagizaji wa mafuta kupitia Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (*Bulk Procurement System - BPS).* Aidha, TPDC ilishinda zabuni sita (6) na

kuingiza nchini tani za ujazo 609,668.39 za mafuta ya dizeli kupitia mfumo huo.

### e) Mradi wa Bomba Jipya la Kusafirisha Mafuta Safi kutoka Tanzania hadi Zambia (New TAZAMA)

133. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta safi kutoka Dar es Salaam - Tanzania hadi Ndola – Zambia lenye urefu wa kilomita 1,710. Kulingana na makadirio ya mwanzo, bomba hili litakuwa na uwezo wa kusafirisha angalau tani milioni tano (5) kwa mwaka. Bomba hili pia litakuwa na matoleo matatu (3) kwa upande wa Tanzania katika maeneo ya Morogoro, Makambako na Songwe. Aidha, kutakuwepo na matoleo mawili (2) kwa upande wa nchi ya Zambia katika maeneo ya Mpika na Serenje. Lengo la kujenga bomba hili ni kukidhi mahitaji ya sasa na baadaye ya usafirishaji wa bidhaa za mafuta kwa nchi za Tanzania, Zambia na nchi za jirani zikiwemo DRC na Malawi. Hadi Machi, 2026 Upembuzi Yakinifu ulikuwa umekamilika na maandalizi ya utekelezaji wa mradi yanaendelea.

## B.2.5 MRADI WA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA NDANI NA UTAWALA WA RASILIMALI ZA ASILI NCHINI

134. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Desemba, 2025 Serikali ilikamilisha utekelezaji wa mradi huu uliolenga kuzijengea uwezo taasisi mbalimbali kusimamia rasilimali za asili zilizopo nchini kwa njia ya mafunzo na ununuzi wa vifaa. Mradi huu ulianza kutekelezwa Juni, 2017 kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB). Gharama za mradi ni **Dola za Marekani milioni 29.54** sawa na **Shilingi bilioni 64.8** ambapo AfDB imechangia **Dola za Marekani milioni 26.59** sawa na **Shilingi bilioni 61.85** na Serikali ya Tanzania itachangia **Dola za Marekani milioni 2.95** sawa na **Shilingi bilioni 6.86**. Taasisi zilizonufaika na mradi huu ni pamoja na Wizara ya Nishati, Wizara ya Fedha, TPDC, TPA, PURA, ZURA, EWURA, NEEC, TRA na ZRB.

135. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizotekelezwa hadi kukamilika kwa mradi ni pamoja na: kukamilisha uundaji wa mfumo wa uondoshaji shehena mipakani kwa

Tanzania Bara na Zanzibar; ununuzi na usimikaji wa midaki (*X Ray Portal Scanner*) miwili katika Bandari ya Dar es Salaam ikiwemo vifaa vya kuhodhi mfumo wa dirisha la pamoja la kieletroniki; uhuishaji wa Mkataba Kifani wa Uzalishaji na Ugawanaji Mapato (*Model Production Sharing Agreement - MPSA*) kupitia PURA; uanzishaji wa vituo vya kujengea wananchi uwezo chini ya Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC); na kuwajengea uwezo wataalamu wa Serikali kupitia mafunzo ya muda mfupi na mrefu kuhusu masuala ya mafuta na gesi.

### B.2.6 UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMPUNI TANZU ZA TPDC

#### a) TANOIL Investments Limited (TANOIL)

136. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Kampuni tanzu ya TPDC ya TANOIL Investments Limited imeendelea kusimamia biashara ya uuzaji wa mafuta kama kampuni ya kununua na kuuza mafuta (*Oil Marketing Company - OMC*) ambapo hadi Machi, 2026 imefanikiwa kuuza lita za ujazo 12,033,500 kwa bidhaa za petroli na dizeli. Aidha, ili kutanua wigo wa biashara,

TANOIL inakamilisha taratibu za kuanzisha biashara ya vilainishi na uuzaji wa gesi ya LPG ambapo Upembuzi Yakinifu na Mpango wa Biashara hiyo vimekamilika.

**b) GAS Company (T) Limited (GASCO)**

137. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Kampuni tanzu ya TPDC ya GASCO imeendelea kusimamia kwa ufanisi uendeshaji, matengenezo na ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia nchini ambapo hadi Machi, 2026 Kampuni hiyo imeendelea kuendesha kwa ufanisi kituo kikubwa cha CNG kilichopo Mlimani City – Dar es Salaam; kushiriki na kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya vituo vinne (4) vya CNG vinavyomilikiwa na kampuni binafsi; na kuendelea kusimamia uendeshaji wa mitambo ya kuchakata na kusafirisha gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam.

## B.3 USIMAMIZI NA UDHIBITI WA SEKTA YA NISHATI KUPITIA PURA NA EWURA

138. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali iliendelea kutekeleza jukumu la udhibiti wa shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli kupitia Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) pamoja na udhibiti wa mkondo wa kati na chini (usafirishaji, uhifadhi na usambazaji) kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ili kuhakikisha shughuli za Sekta ya Nishati zinaendeshwa kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizopo pamoja na utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

### B.3.1 MAMLAKA YA UDHIBITI MKONDO WA JUU WA PETROLI (PURA)

139. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia PURA imeendelea kutekeleza jukumu la usimamizi na udhibiti wa shughuli za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia nchini. Katika kipindi cha hadi Machi, 2026, PURA imesimamia uzalishaji wa gesi asilia katika vitalu vya Mnazi Bay na Songo Songo ambapo

uzalishaji umeendelea kuwa wa uhakika kwa ajili ya matumizi mbalimbali nchini. Aidha, katika kipindi hicho, usimamizi wa shughuli za uchorongaji wa visima vitatu (3), viwili (2) vya uzalishaji na kimoja (1) cha utafutaji katika Kitalu cha Mnazi Bay uliendelea. Kwa sasa uchorongaji wa kisima kimoja cha uzalishaji umekamilika na uzalishaji wa majaribio unaendelea. PURA inaendelea kusimamia ukamilishaji wa uchorongaji wa visima viwili (2) vilivyosalia. Sambamba na hilo, PURA inaendelea kusimamia shughuli za utafiti wa awali wa mafuta na gesi asilia katika Vitalu vya Eyasi – Wembere na Lindi – Mtwara ambapo kazi za uchukuaji wa data za mitetemo zinaendelea.

140. ***Mheshimiwa Spika,*** PURA imeendelea pia kufanya uhakiki, udhibiti na ukaguzi wa gharama na mapato katika mikataba hai ya Ugawanaji Mapato (PSA) kati ya Serikali na Wawekezaji 11 ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2026 ukaguzi wa gharama za mwaka 2023 na 2024 ulikamilika. Tangu Mamlaka imeanza kuhakiki mikataba hiyo mwaka 2017, Serikali imeweza kuokoa jumla ya **Shilingi bilioni 322** kutoka katika madai

ya wawekezaji na kurudishwa kwenye Mfuko wa Ugawanaji Mapato kati ya Serikali na Wawekezaji hao.

141. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na shughuli hizo, Serikali kupitia PURA imeendelea kutangaza fursa za uwekezaji katika shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli nchini kupitia makongamano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ya mafuta na gesi asilia. Hadi kufikia Machi, 2026, PURA imeshiriki katika makongamano ya Kimataifa ya mafuta na gesi asilia mawili (2) yaliyofanyika Afrika Kusini na Ghana. Lengo la kuhamasisha uwekezaji huo ni kutoa fursa kwa wawekezaji katika maandalizi ya duru ya tano ya kunadi vitalu.

## B.3.2 MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

142. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara kupitia EWURA ilitekeleza majukumu mbalimbali ya kiudhibiti kama ifuatavyo:

### a) Usimamizi na Udhibiti wa Shughuli za Mkondo wa Kati na Chini wa Gesi Asilia

143. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia EWURA imeendelea kusimamia shughuli za udhibiti katika Mkondo wa Kati na Chini wa gesi asilia kwa kufanya kaguzi katika miundombinu iliyopo katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Dar es Salaam. Miundombinu hiyo ni ya uchakataji minne (4), usafirishaji miwili (2), mtandao wa usambazaji wenye urefu wa kilomita 243 na vituo 18 vya kujazia gesi asilia iliyoshindiliwa (CNG) kwenye magari. Hadi Machi, 2026, jumla ya kaguzi 68 zilifanyika katika miundombinu hiyo zikijumuisha kaguzi 50 katika miundombinu ya usambazaji na vituo vya CNG na kaguzi 18 katika miundombinu ya uchakataji na usafirishaji wa gesi asilia. Miundombinu iliyokaguliwa ilikidhi viwango vya ubora unaotakiwa.

144. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2026 EWURA ilitoa vibali 9 vya ujenzi wa vituo vya CNG katika Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Ruvuma. Katika Mkoa wa Dar es Salaam vibali vya ujenzi saba (7)

vilitolewa katika maeneo ya Mbezi Beach, Mbagala, Kigamboni, Buguruni, Mwenge, Kinyerezi na Gongolamboto. Aidha, katika Mkoa wa Morogoro kibali kimoja (1) kimetolewa katika eneo la Msamvu na Mkoa wa Ruvuma kibali kimoja (1) kimetolewa katika Wilaya ya Tunduru. Vilevile, EWURA imetoa vibali viwili (2) vya ujenzi wa vituo vya kupokelea gesi asilia iliyoshindiliwa *(CNG receiving facility)* kwa viwanda vilivyopo Kibaha mkoani Pwani.

145. ***Mheshimiwa Spika,*** EWURA ilitoa jumla ya vibali saba (7) vya ujenzi wa mabomba ya kuunganisha na kusafirisha gesi asilia kwa kampuni binafsi na TPDC, kati ya hivyo vibali vinne (4) ni vya ujenzi wa mabomba ya kuunganisha gesi asilia kwenye viwanda, taasisi, migahawa ya chakula na majumbani, viwili (2) kwa ajili ya ujenzi wa mabomba ya kuunganisha gesi asilia kwenye vituo vya CNG na kimoja (1) ni cha ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Ntorya mpaka Madimba. Sambamba na vibali hivyo, EWURA ilitoa jumla ya leseni 17 ambapo tisa (9) ni za uendeshaji wa vituo vya CNG, saba (7) za usafirishaji wa CNG na moja (1) ni leseni ya

usambazaji wa gesi asilia kwa mkoa wa Pwani. Mchanganuo wa leseni na vibali vilivyotolewa hadi Machi, 2026 ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 5.

***Jedwali Na. 5:*** **Mchanganuo wa Leseni na Vibali vya Ujenzi Vilivyotolewa kwa ajili ya Ujenzi na Uendeshaji wa Miundombinu ya Gesi Asilia**

| Na. | Aina ya leseni/kibali | Idadi | Maeneo |
|---|---|---|---|
| 1. | Vibali vya ujenzi wa vituo vya CNG | 9 | Dar es Salaam, Morogoro na Ruvuma |
| 2. | Vibali vya ujenzi wa vituo vya kupokelea gesi asilia iliyoshindiliwa | 2 | Pwani |
| 3. | Vibali vya ujenzi wa mabomba ya kupeleka gesi asilia kwenye vituo vya CNG | 2 | Dar es Salaam |
| 4. | Vibali vya ujenzi wa mabomba ya kupeleka gesi asilia kwenda kwenye viwanda, taasisi, migahawa ya chakula na majumbani | 4 | Dar es Salaam na Pwani |
| 5. | Kibali cha ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Ntorya mpaka Madimba | 1 | Mtwara |
| 6. | Leseni za uendeshaji wa vituo vya CNG | 9 | Dar es Salaam |
| 7. | Leseni za usafirishaji wa CNG (CNG Supply licence) | 7 | Pwani na Dar es Salaam |
| 8. | Leseni ya usambazaji wa gesi asilia mkoa wa Pwani (Distriubution License) – TPDC | 1 | Pwani |
| **Jumla** | | **35** | |

Chanzo : **EWURA**

146. ***Mheshimiwa Spika***, utoaji wa vibali na leseni umeendelea kuongezeka kila mwaka ambapo hadi Machi, 2026 EWURA ilitoa jumla ya leseni 18 za uendeshaji wa vituo vya CNG. Hatua hii inaonesha mwitikio mkubwa wa ushiriki wa sekta binafsi katika mnyororo wa usambazaji wa gesi asilia kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo usafirishaji, viwandani na katika taasisi. Kufuatia mwamko huo, Serikali itaendelea kuimarisha na kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kuchochea kasi ya ushiriki wa sekta binafsi katika usambazaji wa gesi asilia hususan katika mikoa ya kimkakati kama vile Morogoro, Dodoma, Mbeya na Tanga. Nitumie fursa hii kuendelea kutoa wito kwa sekta binafsi kuchangamkia fursa za uwekezaji katika mnyororo wa thamani wa gesi asilia nchini, kutokana na mwamko mkubwa wa wananchi katika kutumia nishati hiyo kwa matumizi mbalimbali, ikiwemo katika vyombo vya moto.

### b) Usimamizi na Udhibiti wa Shughuli za Bidhaa za Mafuta ya Petroli

147. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia EWURA imeendelea kusimamia Mkondo wa Kati na Chini unaohusisha shughuli za mafuta na gesi, ili kuhakikisha upatikanaji wa uhakika na usalama wa bidhaa za mafuta nchini pamoja na ubora wa miundombinu yake. Usimamizi huo umefanyika kwa kutoa vibali vya ujenzi wa mindombinu, leseni za biashara pamoja na kufanya kaguzi mbalimbali. Aidha, hadi Machi, 2026, EWURA ilitoa jumla ya **leseni 636** kwa ajili ya biashara mbalimbali katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi kama inavyofafanuliwa katika Jedwali Na.6.

***Jedwali Na.6:*** **Leseni za Biashara ya Mafuta Zilizotolewa Kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026**

| Aina ya Leseni | Mpya | Zilizohuishwa | Jumla |
|---|---|---|---|
| Kituo cha Mafuta Mijini | 177 | 267 | **444** |
| Kituo cha Mafuta Vijijini | 49 | 30 | **79** |
| Ghala la kuhifadhia Mafuta | 1 | 4 | **5** |
| Kituo cha Mafuta kwa Matumizi Binafsi | 16 | 13 | **29** |

| Aina ya Leseni | Mpya | Zilizohuishwa | Jumla |
| --- | --- | --- | --- |
| Usambazaji wa gesi ya LPG | 21 | 4 | **25** |
| Uuzaji Jumla wa gesi ya LPG | 1 | 2 | **3** |
| Uuzaji Jumla wa Mafuta | 36 | 3 | **39** |
| Uuzaji Jumla wa Vilainishi | 8 | 4 | **12** |
| **Jumla Kuu** | **309** | **327** | **636** |

Chanzo: **EWURA**

148. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2026 EWURA ilitoa vibali 288 vya ujenzi wa miundombinu ya mafuta ambapo vibali 137 vilikuwa kwa ajili ya mjini na vibali 143 kwa vituo vya vijijini. Aidha, vibali vitano (5) vilitolewa kwa ajili ya miundombinu ya kuhifadhi mafuta kwa watumiaji wakubwa kama vile viwanda na migodi, kibali kimoja (1) kwa ajili ya maghala ya kuhifadhi na kujaza LPG, kibali kimoja (1) kwa ajili ya maghala ya kuhifadhi mafuta na kibali kimoja (1) kwa ajili ya kiwanda cha kutengeneza vilainishi.

149. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa na EWURA ni kusimamia taratibu za uagizaji na usambazaji wa mafuta nchini; kusimamia ubora wa bidhaa za mafuta ambapo jumla ya sampuli 648

kutoka katika vituo na maghala ya mafuta zilipimwa ubora na sampuli 608 sawa na **asilimia 93.83** zilikidhi viwango stahiki vya ubora. Vituo 22 ambavyo vilikutwa na mafuta yasiyokidhi viwango vilichukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kufungiwa na kutozwa faini. Aidha, EWURA ilikagua ubora wa miundombinu 544 ya mafuta ambapo miundombinu 473 sawa na **asilimia 86.95** ilikidhi viwango vya ubora ikiwemo vigezo vya masuala ya afya, usalama na mazingira. Wamiliki wa vituo 95 ambavyo havikukidhi viwango walielekezwa kufanya marekebisho.

150. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia EWURA ilifanya marekebisho ya Kanuni mbili (2) ili kuimarisha usambazaji wa mafuta na gesi ya LPG nchini. Kanuni zilizofanyiwa marekebisho ni *The Petroleum (Retail Operations in Townships and Villages), (Amendments) Rules, 2025* ili kujumuisha matumizi ya vituo vya mafuta vya mfumo wa kontena *(containarised petrol station)* kwa lengo la kuchochea uwekezaji wa vituo vya gharama nafuu vijijini na kuongeza upatikanaji wa mafuta. Aidha, *The Petroleum (Liquefied Petroleum Gas*

*Operations) (Amendment) Rules, 2025* zilifanyiwa marekebisho ili kuboresha masharti ya utoaji leseni na kujumuisha matumizi ya gesi ya LPG kwenye magari *(Autogas)* ili kuongeza chaguo la nishati mbalimbali kwa watumiaji na kupunguza athari kwa mazingira.

### c) Utekelezaji wa Programu ya Uwekaji Vinasaba katika Mafuta

151. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia EWURA imeendelea kutekeleza programu ya uwekaji vinasaba katika mafuta ili kudhibiti ubora na kuhakikisha Serikali inapata mapato stahiki ya kodi. Hadi Machi, 2026 kiasi cha lita bilioni 1.51 za mafuta ya petroli, lita bilioni 2.02 za mafuta ya dizeli na lita milioni 2.80 za mafuta ya taa ziliwekewa vinasaba. Hii ni sawa na ongezeko la **asilimia 14** na **asilimia 10** kwa mafuta ya petroli na dizeli mtawalia na pungufu ya **asilimia 40** kwa mafuta ya taa yaliyowekewa vinasaba kwa kipindi kama hicho mwaka 2024/25.

152. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile EWURA ilifanya ukaguzi na kupima vinasaba katika vituo 672, ambapo vituo 50 sawa na asilimia 7.44 vilikutwa na mafuta yasiyokidhi viwango na kuchukuliwa hatua za kisheria, ikiwemo kufungiwa, kutozwa faini na kupelekwa katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa ajili ya kulipa kodi walizokwepa. Pia, EWURA ilifanya ufuatiliaji wa usambazaji wa mafuta na kubaini vituo vitatu (3) vilikuwa vimeficha mafuta kwa jili ya kusubiri bei mpya. Hatua za kisheria zilichukuliwa kwa vituo hivyo ikiwemo kufungiwa na kutozwa faini.


### d) Matumizi ya Mafuta Nchini

153. ***Mheshimiwa Spika,*** wastani wa matumizi ya mafuta kwa siku nchini umeendelea kuongezeka na kufikia lita milioni 6.28 kwa petroli na lita milioni 8.42 kwa dizeli ikilinganishwa na lita milioni 5.45 kwa petroli na lita milioni 7.61 kwa dizeli zilizotumika kila siku kwa mwaka 2024/25. Ongezeko hilo ni sawa na **asilimia 15.23** kwa petroli na **asilimia 10.64** kwa dizeli ambalo linaashiria kuendelea kuongezeka kwa mahitaji ya mafuta kutokana na kukua

kwa shughuli za kiuchumi na kijamii nchini zikiwemo kilimo, ujenzi, usafirishaji, migodi na maendeleo ya viwanda.


154. ***Mheshimiwa Spika,*** mwenendo wa wastani wa matumizi ya mafuta ya petroli na dizeli kwa mwezi hadi kufikia Machi, 2026 ni kama inavyoonekana katika Kielelezo Na.1 na Kielelezo Na. 2.

***Kielelezo Na.1*: Mwenendo wa Wastani wa Matumizi ya Petroli (Lita) kwa Mwezi, Mwaka 2024/25 na 2025/26**




Chanzo : **EWURA**


***Kielelezo Na.2:* Mwenendo wa Wastani wa Matumizi ya Dizeli (Lita) kwa Mwezi, Mwaka 2024/25 na 2025/26**




Chanzo: **EWURA**

155. ***Mheshimiwa Spika,*** matumizi ya mafuta ya taa yameendelea kupungua kutokana na juhudi za Serikali zinazoendelea katika kuunganisha umeme vijijini na kwenye vitongoji pamoja na matumizi ya taa zinazotumia nishati ya jua. Matumizi ya mafuta ya taa yameendelea kupungua kutoka wastani wa lita 19,185 kwa siku mwaka 2024/25 hadi lita 11,628 kwa siku mwaka 2025/26. Kielelezo Na.3 kinaonesha mwenendo wa matumizi ya mafuta ya taa kwa mwaka 2024/25 na 2025/26.

***Kielelezo Na.3:*** **Mwenendo wa Wastani wa Matumizi ya Mafuta ya Taa (Lita) kwa Siku, Mwaka 2024/25 na 2025/26**




Chanzo : **EWURA**

## B.3.3 MWENENDO WA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA DUNIA

156. ***Mheshimiwa Spika,*** bei za mafuta katika soko la dunia ziliendelea kushuka ambapo kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026 bei ya mafuta ghafi ilishuka kwa **asilimia 14** na kufika wastani wa **Dola za Marekani 66** kwa pipa ikilinganishwa na wastani wa **Dola za Marekani 76** kwa pipa kwa kipindi kama hicho mwaka 2024/25.

Hata hivyo, bei hizo zimeanza kuongezeka kutokana na vita inayoendelea Mashariki ya Kati. Jedwali Na.7 linaonesha mwenendo wa bei za mafuta ghafi katika Soko la Dunia.

***Jedwali Na.7*: Mwenendo wa Bei ya Mafuta Ghafi katika Mwaka 2024/25 na 2025/26 (Dola za Marekani kwa Pipa)**

| Mwezi | 2024/25 | 2025/26 |
|---|---|---|
| Julai | 84 | 71 |
| Agosti | 79 | 68 |
| Septemba | 73 | 67 |
| Oktoba | 75 | 65 |
| Novemba | 73 | 63 |
| Desemba | 73 | 61 |
| Januari | 78 | 63 |
| Februari | 75 | 67 |
| Machi | 71 | 102 |
| **Wastani** | **76** | **70** |
| Badiliko | | **- 8%** |


Chanzo**: EWURA**

157. ***Mheshimiwa Spika,*** mwenendo wa bei za mafuta ghafi katika Soko la Dunia ulisababisha kushuka kwa bei za mafuta yaliyosafishwa kuanzia mwezi Julai, 2025 hadi Februari, 2026. Hata hivyo, kuanzia mwezi Machi, 2026 bei hizo zimeanza kuongezeka kwa kasi kufuatia uwepo wa vita katika nchi za Mashariki ya Kati. Athari za vita zimesababisha kufungwa kwa mlango wa bahari wa Hormuz ambapo meli

nyingi za mafuta zinatumia mlango huo na hivyo kusitisha usafirishaji wa mafuta kwenda nchi mbalimbali.

158. ***Mheshimiwa Spika,*** kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026, bei za mafuta yaliyosafishwa katika Soko la Dunia zilikuwa na wastani wa **Dola za Marekani 679.60** kwa tani ya petroli, **Dola za Marekani 715.27** kwa tani ya dizeli na **Dola za Marekani 757.11** kwa tani ya mafuta ya taa na ndege ikilinganishwa na wastani wa **Dola za Marekani 687.64** kwa tani ya mafuta ya petroli, **Dola za Marekani 660.90** kwa tani ya dizeli na **Dola za Marekani 694.48** kwa tani ya mafuta ya taa na ndege katika kipindi kama hicho mwaka 2024/25. Mabadiliko haya ni sawa na punguzo la **asilimia moja** kwa mafuta ya petroli, ongezeko la **asilimia 8** kwenye mafuta ya dizeli na ongezeko la **asilimia 9** kwenye mafuta ya taa na ndege. Kielelezo Na. 4 kinaonesha mwenendo wa bei za mafuta yaliyosafishwa katika Soko la Dunia kati ya Julai, 2025 na Machi, 2026.

***Kielelezo Na.4:*** **Mwenendo wa Bei za Mafuta Yaliyosafishwa katika Soko la Dunia katika Kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 (USD kwa Tani)**




Chanzo**: EWURA**

159. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia vita inayoendelea katika nchi za Mashariki ya Kati bei za mafuta zimeendelea kupanda katika Soko la Dunia kwa **asilimia 69.12** kwa mafuta ya petroli, **asilimia 104.30** kwa mafuta ya dizeli na **asilimia 115.83** kwa mafuta ya taa na ndege kati ya mwezi Februari na Machi, 2026.


## B.3.4 MWENENDO WA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI

160. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia EWURA iliendelea kutoa bei kikomo za bidhaa za mafuta ya dizeli, petroli na mafuta ya taa kwa kuzingatia sheria na kanuni zinazosimamia ukokotoaji wa bei za mafuta. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026, EWURA imetangaza bei za mafuta ya petroli, dizeli na taa ambazo ni stahimilivu. Bei hizo zilishuka mfulululizo *(continous decreasing trend)* kuanzia Septemba hadi Desemba, 2025 ambapo ilichangiwa na kupungua kwa bei ya mafuta yaliyosafishwa katika Soko la Dunia (*FOB price*) na kushuka kwa wastani wa gharama za kubadilisha fedha za kigeni (*applicable exchange rate*). Hata hivyo, bei zilianza kupanda kuanzia mwezi Januari, 2026 hadi Machi, 2026, hii ni kutokana na kuongezeka kwa bei ya mafuta katika Soko la Dunia na kupanda kwa gharama za kubadilisha fedha za kigeni.

161. ***Mheshimiwa Spika,*** wastani wa bei za mafuta nchini hadi Machi, 2026 zimeendelea kushuka ikilinganishwa na

mwaka uliopita. Mathalani, kwa Mkoa wa Dar es Salaam bei za mafuta kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 zilishuka kwa wastani wa **asilimia 4.0** kwa mafuta ya petroli, **asilimia 2** kwa mafuta ya dizeli na **asilimia 1** kwa mafuta ya taa na ndege, ambapo wastani wa bei ya petroli kwa lita ilikuwa **Shilingi 2,838**, dizeli **Shilingi 2,791** na mafuta ya taa **Shilingi 2,827** ikilinganishwa na wastani wa bei za mafuta hayo kwa kipindi cha mwaka 2024/25 ambapo zilikuwa petroli **Shilingi 2,957**, dizeli **Shilingi 2,845** na mafuta ya taa **Shilingi 2,842** kwa lita. Kielelezo Na. 5. kinaonesha ulinganifu wa wastani wa bei za mafuta nchini mwaka 2024/25 na 2025/26.

***Kielelezo Na. 5*: Wastani wa Bei za Rejareja Nchini (TZS/Lita) Mwaka 2024/25 na 2025/26**




Chanzo: **EWURA**

## B.3.5 USIMAMIZI NA UDHIBITI WA SHUGHULI ZA UMEME

162. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2026 Serikali kupitia EWURA ilikuwa imetoa leseni tatu (3) kwa kampuni za kuzalisha umeme kiasi cha **Megawati 48.72** kwa ajili ya matumizi binafsi na leseni sita (6) za muda mfupi kwa kampuni zinazotarajia kuzalisha umeme kiasi cha **Megawati 29.55**. Aidha, EWURA iliidhinisha

mikataba minne (4) ya kuuziana umeme kati ya TANESCO na wazalishaji binafsi ya jumla ya **Megawati 19.9** na hivyo kufanya umeme unaotarajiwa kuongezeka kupitia mikataba na leseni hizo kufikia jumla ya **Megawati 98.17** kama inavyoonekana katika *Kiambatisho Na.5A na 5B*. Vilevile, hadi Machi, 2026 jumla ya **leseni 1,002** za mafundi umeme zilitolewa. Utoaji wa leseni hizo umewezesha kuwapata mafundi wenye elimu na ujuzi wa ufungaji wa mifumo bora na salama ya umeme kwenye majengo ya wananchi ikiwemo maeneo ya vijijini.


## B.4 HALI YA UAGIZAJI NA UPATIKANAJI WA BIDHAA ZA MAFUTA NCHINI

163. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutumia Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (*Bulk Procurement System - BPS*) katika uagizaji wa bidhaa za mafuta ya petroli nchini tangu ulipoanza kutumika rasmi mwezi Januari, 2012. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, jumla ya zabuni 83 zilitangazwa kwa njia ya ushindani wa kimataifa kwa kigezo cha gharama ndogo za uletaji wa mafuta nchini (*premium*). Aidha, kati ya zabuni 10 hadi 12

zilishindanishwa kila mwezi ambapo wazabuni tisa (9) hadi 10 ikiwemo TPDC walishiriki katika zabuni hizo.

164. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya lita bilioni 5.84 za bidhaa za mafuta ya petroli ziliagizwa ambapo petroli ilikuwa lita bilioni 1.63, dizeli lita bilioni 3.94 na mafuta ya taa/ndege lita milioni 260 katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026. Kati ya mafuta hayo yaliyoagizwa katika kipindi husika, lita bilioni 2.56 sawa na **asilimia 43.83** yalikuwa kwa ajili ya matumizi ya ndani na lita bilioni 3.28 sawa na **asilimia 56.16** yalikuwa kwa ajili ya nchi jirani. Aidha, bidhaa hizo ziliagizwa na kupokelewa kupitia Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Kielelezo Na. 6 kinaonesha jumla ya kiasi cha bidhaa za mafuta kilichoagizwa kwa mgawanyo wa kila aina ya mafuta kwa kipindi cha mwezi Julai, 2025 hadi Machi, 2026.

***Kielelezo Na. 6*: Mchanganuo wa Bidhaa za Mafuta zilizoagizwa kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026**





Chanzo***:* PBPA**

165. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na ufanisi wa mfumo wa BPS hali ya upatikanaji wa mafuta imeendelea kuwa imara na kuhakikisha usalama wa upatikanaji wa mafuta katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, ufanisi wa mfumo huo umewezesha nchi jirani kuendelea kuutumia katika uagizaji wa mafuta kupitia bandari zilizopo

nchini. Kielelezo Na.7 kinaonesha jumla ya kiasi cha mafuta kilichoagizwa kwa ajili ya matumizi ya ndani na nchi jirani.

***Kielelezo Na.7* : Kiasi cha Mafuta Kilichoagizwa kwa ajili ya Matumizi ya Ndani na Nchi Jirani kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026**




Chanzo**: PBPA**

166. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutumia miundombinu ya Kampuni ya TIPER kama kituo cha kupokea mafuta kwa pamoja (*Single Receiving Terminal - SRT*).

Kituo hicho kina uwezo wa kupokea meli mbili (2) hadi tatu (3) za mafuta ya dizeli kwa mwezi ambapo kila meli ina ujazo wa hadi lita milioni 120. Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) inaendelea na ujenzi wa maghala mapya ya kupokelea mafuta kwa pamoja (SRT) katika eneo la Kigamboni ambapo mwezi Machi, 2026 Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliweka jiwe la msingi. Ujenzi wa miundombinu hiyo unatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2027 na utasaidia kupunguza gharama za ucheleweshaji wa meli (*demurrage*) kwa kuongeza ufanisi wa upakuaji mafuta kuendana na muda unaotakiwa kimataifa (chini ya saa 72 kwa meli kubwa na saa 36 kwa meli za kati).

167. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia PBPA imeendelea kuongeza ufanisi wa usimamizi wa upakuaji mafuta kutoka kwenye meli kwenda kwenye hifadhi za kampuni za mafuta kwa kutumia mfumo wa kielektroniki (SCADA). Hatua hii imeimarisha udhibiti wa upotevu wa mafuta wakati wa upakuaji wa mafuta hayo kutoka kwenye meli. Mfumo huu unasoma kiasi cha mafuta

yanayopita katika mita (*flowmeter*) za Serikali zilizopo Kurasini (KOJ), Kigamboni (SBM), Tanga na Mtwara na kulinganisha kiasi hicho na mafuta yanayopita mita za kampuni za mafuta na kupokelewa kwenye maghala ya kuhifadhi mafuta. Uwepo wa mfumo huu umepunguza upotevu wa mafuta kutoka **asilimia 0.5** kabla ya mfumo hadi **asilimia 0.1** baada ya mfumo huo.

## B.5 USHIRIKI WA SEKTA BINAFSI NA USHIRIKISHWAJI WA WATANZANIA KATIKA SEKTA YA MAFUTA NA GESI ASILIA

168. ***Mheshimiwa Spika,*** Watanzania wameendelea kunufaika na fursa mbalimbali za kiuchumi na kijamii zilizopo katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia kupitia shughuli zinazotekelezwa. Jitihada mbalimbali zinafanyika ikiwa ni pamoja na kuboresha na kusimamia miongozo na kanuni zinazosimamia ushirikishwaji *(local content)* na urejeshaji kwa jamii (CSR) katika miradi ya mafuta na gesi asilia nchini. Jitihada hizo ni pamoja na Serikali kuendelea kuhakikisha kuwa Kampuni zilizowekeza katika shughuli za mafuta na gesi asilia zinatoa

kipaumbele cha ajira kwa wazawa na zinawajibika kuishirikisha jamii husika ipasavyo katika kuibua na kutekeleza miradi kwenye jamii husika.

169. ***Mheshimiwa Spika,*** ushiriki wa wazawa na urejeshaji kwa wananchi kwenye miradi mbalimbali ya mafuta na gesi asilia unaendelea kuongezeka, ambapo hadi Machi, 2026 kampuni za kitanzania 186 zilisajiliwa na kufikia jumla ya kampuni 2,535 zenye sifa ya utoaji wa huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na afya, fedha, chakula, ulinzi, mafuta ya kuendesha mitambo na ukarabati wa miundombinu ya gesi asilia. Aidha, urejeshaji kwa jamii unaendelea kuimarika hususan katika utekelezaji wa miradi ya elimu, afya, maji, usafirishaji na upatikanaji wa nishati. Kampuni hizo pamoja na kampuni zinazotoa huduma zimefaidika kwa kupata kandarasi na kutoa huduma zenye thamani ya zaidi ya **Shilingi trilioni 1.325** ambapo fedha hizo zimeingia kwenye mzunguko wa uchumi wa nchi.

170. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya watanzania 110 wamepata ajira katika shughuli mbalimbali katika sekta ikiwemo shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya Eyasi-Wembere na Lindi-Mtwara, uendelezaji na uzalishaji katika vitalu vya Mnazi Bay, Songo Songo na Ruvuma (eneo la Ntorya). Shughuli hizi zimewezesha idadi ya ajira kuongezeka na kufikia 335 kutoka 225 Machi, 2025, ambapo ongezeko limechagizwa na kuongezeka kwa ujuzi na uwezo wa wataalamu wa ndani.

171. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa mkondo wa kati na chini ikiwemo utekelezaji wa mradi wa EACOP, hadi Machi, 2026 jumla ya watanzania 2,431 wenye ujuzi wa chini na kati wameajiriwa katika fani mbalimbali za uhandisi (ujenzi, mitambo, umeme), usimamizi wa mazingira na usalama, maendeleo ya jamii na nyinginezo. Vilevile, mafunzo mbalimbali ya kuimarisha uwezo katika teknolojia ya ujenzi na usimamizi wa mitambo ya mafuta na gesi yameendelea kutolewa kupitia mradi wa EACOP na kuwezesha idadi ya ajira kufikia 9,194 katika mradi huo hadi sasa.

Aidha, EACOP inashirikiana na Chuo cha Ufundi Arusha na Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) Moshi kuhaulisha teknolojia kwa makundi mbalimbali kwa vijana ili kuwaimarisha katika kazi mbalimbali. Kupitia programu hiyo jumla ya vijana 120 wamepatiwa mafunzo ya kuendesha shughuli za mradi mara utakapokamilika.

172. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu pia umezalisha jumla ya ajira 11,155 ambapo ajira 8,756 zimetolewa kwa watanzania na 2,399 zimetolewa kwa raia wa kigeni. Vilevile, jumla ya bidhaa na huduma zenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 141.68** sawa na takriban **Shilingi bilioni 389.63** zilinunuliwa kutoka soko la ndani.

173. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia Serikali kwa kushirikiana na wawekezaji inaendelea kuwajibika kwa jamii kwa kutekeleza miradi mbalimbali kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma na uhusiano kati ya wawekezaji na jamii husika katika eneo la mradi. Hadi Machi, 2026 miradi mbalimbali ilikuwa

inaendelea kutekelezwa, ikiwa ni pamoja na:

(i) Ujenzi wa Shule ya Msingi Likong’o katika Manispaa ya Lindi ambapo utekelezaji wake umefikia **asilimia 81**; na

(ii) Ujenzi wa kivuko kitakachounganisha Songo Songo na Kilwa kinachojengwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 5.2** na kinatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2026.

## B.6 UIMARISHAJI UTENDAJI KAZI NA UTOAJI WA HUDUMA

174. ***Mheshimiwa Spika***, kuwepo kwa tija na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara kunahitaji pamoja na mambo mengine, nguvu kazi inayokidhi mahitaji na yenye utaalamu, sifa na uzoefu stahiki. Wizara na Taasisi zake ina jumla ya watumishi 8,078 wa kada mbalimbali ambao wanatekeleza majukumu kwa mujibu wa Miundo ya Maendeleo ya Utumishi wa Umma. Serikali katika mwaka 2025/26 iliwapeleka mafunzo watumishi 2,120,

kuwapandisha vyeo watumishi 1,614 pamoja na kuajiri watumishi 38. Vilevile, Taasisi ya TANESCO inatarajia kuajiri watumishi 1,940 kabla ya kumalizika kwa mwaka 2025/26. Aidha, ili kuhakikisha kunakuwepo na mazingira bora ya utekelezaji wa majukumu, Wizara ilikamilisha ujenzi wa jengo la ofisi Mtumba na imehamia katika jengo hilo.

175. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara pia iliendelea kusimamia masuala mbalimbali ya Kiutumishi na Utawala ili kuimarisha tija na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake na utoaji wa huduma, ikiwa ni pamoja na kununua vitendea kazi, kusimamia mfumo wa upimaji utendaji kazi Serikalini, kusimamia mifumo ya kielekroniki inayotumika katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na kushughulikia masuala mtambuka ikiwemo utawala bora, magonjwa sugu na yasiyoambukizwa na UKIMWI katika eneo la kazi.

## B.7 MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2025/26

176. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/26 Wizara imepata mafanikio mbalimbali katika utekelezaji wa Bajeti ikiwa ni pamoja na:

a. Kuimarika kwa uzalishaji wa umeme ambapo uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme umeongezeka na kufikia Megawati 4,522.54 ikilinganishwa na Megawati 4,031.71 zilizokuwepo mwezi Machi, 2025 sawa na ongezeko la **asilimia 12.17**;

b. Kukamilika kwa awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya jua uliopo Kishapu, mkoani Shinyanga, inayohusisha uzalishaji wa Megawati 50 na hivyo kuiwezesha nchi yetu kuweka historia ya kuanza uzalishaji wa kiwango kikubwa cha umeme utokanao na jua. Aidha, hatua hii imeongeza wigo wa vyanzo vya

kuzalisha umeme nchini ambavyo ni safi na rafiki wa mazingira;

c. Kiwanda cha kutengeneza nguzo za zege kilichojengwa na TCPM mkoani Tabora chenye uwezo wa kuzalisha wastani wa nguzo 120 kwa siku kimekamilika, na hivyo kuongeza wigo na uhakika wa upatikanaji wa nguzo za zege kwa ajili ya usafirishaji na usambazaji wa umeme hususan katika mkoa wa Tabora na mikoa ya jirani;

d. Miundombinu ya kusafirisha umeme nchini imeongezeka na kufikia jumla ya kilomita 8,500.38, ikilinganishwa na kilomita 7,809.67 zilizokuwa zimefikiwa Machi, 2025 sawa na ongezeko la **asilimia 9**. Aidha, miundombinu ya kusambaza umeme, imeongezeka na kufikia kilomita 240,229.56 ikilinganishwa na kilomita 200,266.25 zilizofikiwa mwezi Machi, 2025 sawa na ongezeko la **asilimia 20**;

e. Serikali imekamilisha kuunganisha Mkoa wa Katavi katika Gridi ya Taifa na hivyo kuimarisha upatikanaji wa umeme katika mkoa huo pamoja na kuipunguzia TANESCO gharama za uzalishaji wa umeme kwa kutumia mafuta katika mkoa huo, ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 68.4** zimeweza kuokolewa. Aidha, utekelezaji wa mradi wa njia ya kusafirisha umeme ya Ibadakuli - Simiyu pamoja na kituo cha kupoza umeme cha Simiyu unaendelea, ambapo kukamilika kwake kutaimarisha upatikanaji wa umeme katika mkoa wa Simiyu;

f. Serikali imeanza kutekeleza mradi mkubwa wa kupeleka umeme katika Vitongoji 9,009 ambao utakamilika katika kipindi cha miaka mitatu ijayo. Hatua hii pamoja na miradi inayoendelea kutekelezwa ya kupeleka umeme vitongojini, itawezesha vitongoji 50,453 sawa na **asilimia 78.4** ya vitongoji vyote 64,359 vya Tanzania Bara kufikishiwa huduma ya umeme ifikapo mwaka 2028, hatua ambayo itachochea kasi ya maendeleo ya kiuchumi na

kijamii vitongojini pamoja na utoaji wa huduma bora katika maeneo hayo;

g. Kuongezeka kwa hali ya upatikanaji wa umeme nchini (*accesibility*) kutoka wastani wa **asilimia 78.4** mwaka 2020 na kufikia wastani wa **asilimia 85.5**. Aidha, kiwango cha wananchi waliounganishiwa umeme nchini (*connectivity*) kimeongezeka kutoka **asilimia 37.7** mwaka 2020 hadi **asilimia 52.1**;

h. Matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini yameendelea kuimarika kutoka **asilimia 6.9** mwaka 2021 hadi kufikia **asilimia 28.6** ya watanzania wenye nishati safi ya kupikia mwaka 2025. Kwa namna ya kipekee, nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongea Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maono na uongozi wake uliotuwezesha kuwa na mwelekeo huu wa kitaifa wa kuhakikisha wananchi wetu wanatumia nishati safi ya kupikia, agenda ambayo imempa heshima ya kuwa kinara wa nishati safi ya kupikia Barani Afrika na kimataifa;

i. Vituo vya kujazia gesi asilia katika vyombo vya moto *(CNG filling stations)* vimeongezeka na kufikia vituo 18 mwezi Machi, 2026 ikilinganishwa na vituo tisa (9) mwezi Aprili, 2025. Aidha, kampuni binafsi zaidi ya 86 za ndani na nje ya nchi zimepewa idhini ya kuwekeza katika miradi ya gesi asilia kama mbadala wa mafuta ya petroli na dizeli kwenye vyombo vya moto;

j. Utekelezaji wa Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani (Tanga) Tanzania (*East African Crude Oil Pipeline - EACOP)* umefikia **asilimia 82.60**, ikilinganishwa na **asilimia 55**, mwezi Aprili, 2025; na

k. Nchi imeendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta ya petroli (petroli, dizeli na taa) na bei za bidhaa hizo zimeendelea kuwa himilivu na hivyo kutoathiri shughuli za uzalishaji, usafirishaji na utoaji wa huduma kwa jamii.

## B.8 CHANGAMOTO NA UTATUZI WAKE

177. ***Mheshimiwa Spika***, miradi ya nishati inahitaji uwekezaji mkubwa *(capital intensive)* ili kupata matokeo yanayotarajiwa, hatua ambayo pamoja na jitihada kubwa za uwekezaji zinazofanywa na Serikali, bado ni muhimu kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Washirika wa Maendeleo na Sekta Binafsi katika kufanikisha utekelezaji wake. Hivyo, mwelekeo wa Wizara ni kuendelea kushirikiana na wadau hawa ili mchango wao uweze kutumika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya nishati ambayo ipo katika hatua za maandalizi.

## C. MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2026/27

178. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa taarifa kuhusu hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2025/26, na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho katika Sekta ya Nishati, napenda sasa kuwasilisha Mpango na Bajeti kwa mwaka 2026/27.

179. ***Mheshimiwa Spika,*** usimamizi na uendelezaji wa Sekta ya Nishati pamoja na mambo mengine, unaongozwa na Sera, Mikakati, Mipango na Malengo mbalimbali ya kisekta, kitaifa na kimataifa. Hivyo, katika uandaaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mwaka 2026/27, Wizara imezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2025 - 2030; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 (Dira 2050); Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP IV), 2026/27–2030/31; Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, wakati wa Kufungua Rasmi Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dodoma, tarehe 14 Novemba 2025; na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2026/27;

180. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imezingatia pia maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na Kamati nyingine za Bunge uliotolewa kwa nyakati tofauti; Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Nne 2023-2030 (*National Anti - Corruption Strategy and Action Plan Phase*

*Four (NACSAP IV) 2023-2030*); Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 - 2034); Mpango Mahususi wa Taifa wa Nishati wa Mwaka 2025 - 2030 (*National Energy Compact 2025 - 2030*) ulioidhinishwa katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali za Afrika kuhusu Nishati; Sera, Sheria, Mikakati na Programu mbalimbali za Kisekta na Taifa pamoja na maoni ya wadau wa kisekta; Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs) ya Mwaka 2030 na Mikataba na Itifaki mbalimbali za Kimataifa zinazohusu Sekta ya Nishati ambazo Tanzania ni Mwanachama.

181. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27 Serikali kupitia Wizara ya Nishati itaendelea kuchukua hatua za kuimarisha na kuendeleza Sekta ya Nishati kwa kutekeleza vipaumbele mbalimbali kwa kushirikiana na wadau ikiwemo Sekta Binafsi. Vipaumbele vitakavyotekelezwa ni pamoja na kuimarisha uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme, ikiwemo kuunganisha mikoa ya Rukwa, Kagera, Lindi na Mtwara katika Gridi ya Taifa; kuongeza kasi ya kuunganisha umeme kwa wananchi ili kuchochea ukuaji wa shughuli

za kiuchumi na kijamii*;* kuendelea kutekeleza mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa (*National Grid Stabilization Project-Gridi Imara)* ili kuwezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini; kufanya matengenezo na ukarabati wa miundombinu ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme; na kuendelea na usambazaji wa umeme katika vitongoji, ikiwemo kwenye shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo hayo (migodi, kilimo, viwanda, shule, pampu za maji na vituo vya afya) pamoja na kuwezesha ujenzi wa vituo vya mafuta vijijini ili kuimarisha upatikanaji wa nishati safi na salama kwa vyombo vya moto katika maeneo hayo.

182. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia itaendelea kukuza matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa kuendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024-2034) na Mpango Mahususi wa Taifa wa Nishati wa Mwaka 2025 - 2030 *(National Energy Compact 2025 - 2030);* na kuimarisha uzalishaji wa gesi asilia kwa kutekeleza miradi ya utafutaji na uendelezaji wa nishati hiyo ikiwemo mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia

kuwa Kimiminika *(Liquefied Natural Gas – LNG Project)*, mradi wa uendelezaji wa gesi asilia iliyogunduliwa eneo la Ntorya katika Kitalu cha Ruvuma na miradi ya kielelezo na kimkakati ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya Eyasi – Wembere, Lindi - Mtwara na Mnazi Bay. Maeneo mengine ya kipaumbele ni kuimarisha upatikanaji wa gesi asilia kwa ajili ya vyombo vya moto (CNG), viwandani, katika taasisi na majumbani pamoja na kuendelea na majadiliano ya kibiashara ya nishati hiyo na nchi nyingine ikiwemo Kenya na Uganda.

183. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na changamoto zitokanazo na vita, ambazo zinaathiri upatikanaji wa bidhaa za mafuta duniani, Serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu hali ya upatikanaji wa mafuta duniani na kuchukua hatua stahiki, ili kuhakikisha Taifa letu linaendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa hizo ambazo ni muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi, usafiri na usafirishaji. Vilevile, jitihada zitaelekezwa katika ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi na usafirishaji wa bidhaa za mafuta ya petroli ndani na nje ya

nchi na kutekeleza shughuli za kiudhibiti katika Sekta ya Nishati. Pia, Wizara itaendelea kuimarisha ushiriki wa wazawa katika shughuli za mafuta na gesi asilia; kuendelea kuimarisha utendaji wa Taasisi/ Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya TANESCO, REA, TPDC, PBPA, EWURA na PURA pamoja na Kampuni Tanzu kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma, tija na ufanisi katika uendeshaji na mapato; na kuimarisha na kusimamia nguvu kazi ya Wizara, mifumo ya utendaji kazi, upatikanaji wa vitendea kazi pamoja na kushughulikia masuala mtambuka ikiwemo utawala bora, Magonjwa Sugu na Yasiyoambukizwa na UKIMWI katika eneo la kazi.

## C.1 SEKTA NDOGO YA UMEME NA NISHATI JADIDIFU

### C.1.1 MIRADI YA KUZALISHA UMEME

184. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27 Serikali kupitia Wizara ya Nishati itatekeleza miradi mbalimbali ya uzalishaji wa umeme ili kuendelea kuhakikisha nchi inakuwa na umeme wa kutosha, uhakika na endelevu, kutokana na umuhimu wa

nishati hii katika ukuaji wa Taifa letu, maendeleo ya kijamii na utoaji wa huduma bora. Miradi itakayotekelezwa ni kama ifuatavyo:

**a) Miradi Iliyopo katika Hatua za Utekelezaji**

**(i) Mradi wa Kuzalisha Umeme Jua Mkoani Shinyanga – MW 150**

185. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kukamilisha utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi utakaohusisha ukamilishaji wa majengo *(buildings finishing and furniture),* ujenzi wa barabara za ndani pamoja na kazi ndogo ndogo zilizosalia *(snags).* Vilevile, Serikali itakamilisha usanifu wa awamu ya pili ya mradi na kuanza ujenzi wa miundombinu ya kuzalisha umeme wa jua wa Megawati 100. Jumla ya **Shilingi bilioni 83.49** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

### (ii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Malagarasi – MW 49.5

186. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea na ujenzi wa tuta kuu (*main dam),* njia ya kusafirisha maji kuelekea kwenye jengo la mitambo (*headrace culvert*), tenki la kupumulia (*surge tank*) na jengo la mitambo *(power house)*. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa kituo cha kupoza na kusafirisha umeme *(switch yard*) na ujenzi wa nyumba za kudumu. Jumla ya **Shilingi bilioni 74.82** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

### (iii) Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP – MW2,115)

187. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea na usimamizi na uratibu wa mradi huu, kulipa fedha za zuio (*retention money*) kulingana na masharti ya mkataba, kulipa stahiki za Mshauri Mwelekezi (TECU) kwa huduma za usimamizi wa mradi, pamoja na kugharamia shughuli za usimamizi na ufuatiliaji wa mradi katika kipindi cha matazamio (*Defects Notification Period –*

*DNP*) ili kuhakikisha mradi unakamilika na kuendeshwa kwa kuzingatia viwango vya kimkataba na kitaalamu. Jumla ya **Shilingi bilioni 350** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

### (iv) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Kakono MW - 87.8

188. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zilizopangwa kutelekezwa ni kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha mradi, kukamilisha taratibu za kuwapata wakandarasi wa ujenzi, Mshauri Mwelekezi wa kusimamia mradi na kuanza ujenzi wa bwawa na njia ya kusafirisha umeme. Jumla ya **Shilingi bilioni 2** fedha za ndani na **Shilingi billioni 93.19** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

### (v) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi I Extension – MW 185

189. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa katika mradi huu ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa mitambo na vituo vya kupoza umeme wa msongo wa kilovolti 132/33

katika maeneo ya Mbagala na Gongolamboto na kukamilisha kazi ndogo ndogo (*snags*) zilizosalia katika kipindi cha matazamio ya mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 20** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 3.85** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi tajwa.

**b) Miradi ya Uzalishaji wa Umeme Iliyopo katika Hatua za Maandalizi**

**(i) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Ruhudji – MW 358**

190. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27 kazi zitakazotekelezwa ni kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha eneo la mradi, kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya usimamizi wa mradi na kukamilisha taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mradi *(EPC contractor)* wa bwawa la kuzalisha umeme pamoja na njia ya kusafirisha umeme. Jumla ya **Shilingi bilioni 115** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

### (ii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Rumakali – MW 222

191. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi, kukamilisha taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi (*Transaction Adviser*) kwa ajili ya maandalizi ya zabuni, na kuendelea na taratibu za kumpata mwekezaji wa mradi kwa utaratibu wa *Build, Operate and Transfer* (BOT). Aidha, Serikali kupitia TANESCO inaendelea kufanya majadiliano na wawekezaji mbalimbali waliooonesha nia ya kushiriki utekelezaji wa mradi huu kupitia utaratibu wa Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP) hatua inayolenga kuongeza kasi ya utekelezaji wake. Jumla ya **Shilingi bilioni 20** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(iii) Mradi wa Kuzalisha Umeme Jua - MW 100 Same na MW 100 Singida**

192. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka ujao wa fedha 2026/27 kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kufanya Upembuzi Yakinifu wa mradi na Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (*Environmental and Social Impact Assessment – ESIA).* Jumla ya **Shilingi bilioni 1.15** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(iv) Maandalizi ya Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Nishati ya Nyuklia Pamoja na Vyanzo Vingine**

193. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza wigo wa mchanganyiko wa vyanzo vya nishati ya umeme nchini, Serikali katika mwaka 2026/27 itaanza maandalizi ya miradi mikubwa ya kuzalisha umeme kwa kutumia vyanzo vipya ikiwa ni mwelekeo wa kuwa na Megawati 70,000 za umeme ifikapo mwaka 2050 kwa mujibu wa Dira 2050. Kazi zitakazotekelezwa ni kuratibu utekelezaji wa hatua za awali za maandalizi ya kiufundi ili kuanza utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya

nyuklia pamoja na vyanzo vingine nchini ili kufikia MW 8,000 ifikapo mwaka 2030. Jumla ya **Shilingi bilioni 7** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mpango huu.

**(v) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Kikonge – MW 321**

194. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa Megawati 321 kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Ruhuhu mkoani Ruvuma na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilomita 96 kutoka Kikonge hadi kituo cha kupoza umeme cha Madaba. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya awali ya mradi ili kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya maandalizi ya zabuni za utekelezaji wa mradi kwa utaratibu wa PPP. Jumla ya **Shilingi milioni 100** zimetengwa na TANESCO kwa ajili ya kazi hiyo.

### (vi) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia Mtwara - MW 300

195. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha wananchi waliopisha mradi huu mkoani Mtwara wanalipwa viwango stahiki vya fidia, Serikali itahuisha daftari la uthamini wa mali za wananchi hao na kuendelea na ulipaji wa fidia. Hatua hiyo itawezesha utekelezaji wa mradi huu ambao kukamilika kwake kutaongeza kiwango cha umeme katika Gridi ya Taifa. Jumla ya **Shilingi milioni 500** zimetengwa na TANESCO kwa ajili ya mradi huu.

### (vii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia Kinyerezi III - MW 1,000

196. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha Megawati 1,000 za umeme kwa kutumia gesi asilia katika eneo la Kinyerezi – Dar es Salaam. Kazi zitakazotekelezwa ni kuhuisha Upembuzi Yakinifu, kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA) na tathmini ya mali kwa wananchi watakaopisha

eneo la mradi. Jumla ya **Shilingi milioni 200** zimetengwa na TANESCO kwa ajili ya mradi huu.

## C.1.2 MIRADI YA KUSAFIRISHA NA KUSAMBAZA UMEME

### a) Miradi ya Kusafirisha na Kusambaza Umeme Iliyopo katika Hatua za Utekelezaji

#### (i) Mradi wa Kusafirisha Umeme kutoka Rufiji hadi Chalinze – Kilovoti 400 na Kituo cha Kupoza Umeme, Chalinze

197. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa kufanyika katika mradi huu ni kukamilisha malipo ya mkandarasi wa mradi kwa mujibu wa mkataba ili kuwezesha kukamilisha majukumu ya kimkataba na kufunga rasmi utekelezaji wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 10** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(ii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya na Tunduma (TAZA)**

198. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kukamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi waliopisha mradi, kukamilisha ujenzi wa njia na vituo vya kupoza umeme pamoja na shughuli ndogo ndogo (*snags*). Jumla ya **Shilingi bilioni 4** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 167.78** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

**(iii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze – Dodoma (*NEG Phase 2*)**

199. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi waliopisha eneo la mradi, kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme pamoja na kufanya majaribio ya kiufundi, uhakiki na kuwasha rasmi njia ya umeme. Jumla ya **Shilingi bilioni 200**

fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

### (iv) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze - Kinyerezi - Mkuranga (*NEG Phase 1*)

200. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya njia ya kusafirisha umeme, usimikaji wa nguzo za umeme, uvutaji wa nyaya pamoja na kufanya majaribio na kuwasha rasmi njia ya umeme. Jumla ya **Shilingi bilioni 5.05** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

### (v) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma

201. ***Mheshimiwa Spika***, kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kukamilisha kazi ndogo ndogo zilizosalia *(snags),* kukamilisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kidahwe mkoani Kigoma na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi.

Jumla ya **Shilingi bilioni 28.43** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(vi) Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa (*National Grid Stabilization Projects)* – Gridi Imara**

202. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa zitahusisha kukamilisha malipo ya hati za madai ya wakandarasi kwa mujibu wa masharti ya mikataba, kutekeleza miradi 20 iliyosalia kati ya 27 ya umeme inayojumuisha njia za kusafirisha umeme, vituo vya kupoza umeme na njia za kusambaza umeme kwa kuzingatia mikataba husika. Jumla ya **Shilingi bilioni 265** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(vii) Mradi wa Ukarabati na Uboreshaji wa Gridi ya Taifa *(TANESCO Transmission Grid Rehabilitation and Upgrading - TTGRUP)***

203. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kukamilisha malipo ya wakandarasi na Mshauri Mwelekezi sambamba na kukamilisha kazi zilizosalia wakati wa kipindi cha uangalizi wa mradi.

Jumla ya **Shilingi bilioni 26.89** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

### (viii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Benaco hadi Kyaka

204. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itakamilisha malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha eneo la mradi na kuanza ujenzi na usimikaji wa misingi ya minara ya kusafirishia umeme. Aidha, kazi nyingine zitakazofanyika ni uvutaji wa nyaya pamoja na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Benaco. Jumla ya **Shilingi bilioni 3** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 63.47** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

### (ix) Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Ibadakuli, Shinyanga

205. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kukamilisha ulipaji wa fidia, ujenzi wa kituo cha kupoza umeme na ununuzi na ufungaji wa kifaa cha kudhibiti umeme (STATCOM). Jumla ya **Shilingi bilioni 20** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**b) Miradi ya Kusafirisha na Kusambaza Umeme Iliyopo Katika Hatua ya Utayarishaji**

**(i) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze – Segera, Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Segera – Tanga na Msongo wa kilovoti 220 kutoka Chalinze – Bagamoyo**

206. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kumpata Mshauri Mwelekezi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Chalinze – Segera, kilovoti 220 Segera – Tanga na kilovoti 220 kutoka Chalinze – Bagamoyo, kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha eneo la mradi na kuanza ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 15** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 151.38** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(ii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Segera – Same - Arusha (*Lemugur*)**

207. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuanza taratibu za awali za ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha eneo la mradi pamoja na kuendelea na majadiliano na Wadau wa Maendeleo ili kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Jumla ya **Shilingi milioni 200** zimetengwa na TANESCO kwa ajili ya mradi huu.

**(iii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme (SGR *Lot* 3, *Lot* 4, *Lot* 5 na *Lot* 6)**

208. ***Mheshimiwa Spika***, kazi zilizopangwa kufanyika katika kipande cha *Lot 3* ni pamoja na kumpata Mshauri Mwelekezi; kulipa fidia wananchi wanaopisha mradi; na kuanza taratibu za kumpata mkandarasi wa ujenzi wa mradi. Vilevile, katika *Lot 4* kazi zitakazotekelezwa ni kukamilisha Upembuzi Yakinifu na Tathmini ya Athari

kwa Mazingira na Jamii; na kufanya uthamini wa mali za wananchi wanaopisha mradi. Aidha, kazi zitakazotekelezwa katika *Lot 5* ni kukamilisha malipo ya fidia; na kuendelea na ujenzi wa mradi. Vilevile, katika *Lot 6* (Tabora hadi Kigoma), Serikali itafanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii na kuanza uthamini wa mali za wananchi wanaopisha eneo la mradi. Jumla ya **Dola za Marekani milioni 125** sawa na takriban **Shilingi bilioni 343.80** zimetengwa kupitia Fungu la SGR kwa ajili ya kutekeleza miradi hii.

**(iv) Ujenzi wa Njia za Kusafirisha Umeme *(Submarine Cables)* Msongo wa Kilovoti 220 Kutoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar na Mafia**

209. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha eneo la mradi, kumpata Mshauri Mwelekezi wa kusimamia ujenzi wa mradi na kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 1.5** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 31.28** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(v) Mradi wa Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Tanzania hadi Uganda (Ibadakuli - Masaka)**

210. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa ni kumpata Mshauri Mwelekezi, kuendelea na taratibu za ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha eneo la mradi pamoja na kuwapata wakandarasi. Jumla ya **Shilingi bilioni 1.9** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(vi) Mradi wa Njia ya Mzunguko wa Kusafirisha Umeme (*Dodoma Ring Circuit*) Msongo wa Kilovoti 220**

211. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali italipa fidia wananchi wanaopisha eneo la mradi wa njia ya mzunguko wa kusafirisha umeme katika Jiji la Dodoma, kuwapata wakandarasi na kuanza ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 6.06** zimetengwa na TANESCO kwa ajili ya mradi huu.

### (vii) Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Misigiri, Singida

212. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa katika mradi huu ni kufanya uthamini wa mali za wananchi wanaopisha mradi, kuweka mipaka ya eneo la mradi pamoja na kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi milioni 150** zimetengwa na TANESCO kwa ajili ya mradi huu.

### (viii) Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Mbinga, Ruvuma

213. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mradi huu ni kufanya uthamini wa mali za wananchi wanaopisha mradi, kuweka mipaka ya eneo la mradi pamoja na kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi milioni 100** zimetengwa na TANESCO kwa ajili ya mradi huu.

c) **Ukarabati wa Vituo vya Kuzalisha Umeme vya Mtera (MW 80), Kihansi (MW 180), Pangani (MW 68) na Nyumba ya Mungu (MW 8)**

214. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali itaendelea na ukarabati wa vituo hivi vya kuzalisha umeme ili kuhakikisha vituo hivyo vinafanya kazi kwa ufanisi. Kazi zitakazotekelezwa ni kukamilisha Upembuzi Yakinifu, kuanza taratibu za kuwapata Washauri Elekezi na kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii. Jumla ya **Shilingi bilioni 1.03** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

### C.1.3 UTENDAJI WA KAMPUNI TANZU ZA TANESCO (ETDCO, TCPM NA TGDC)

a) **Kampuni ya Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Usafirishaji na Usambazaji Umeme (ETDCO)**

215. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia kampuni tanzu ya TANESCO ya ETDCO, itaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 132 kutoka Urambo hadi Kidahwe

kupitia kituo cha kupoza umeme cha Nguruka. Aidha, Serikali itakamilisha utekelezaji wa miradi ya umeme katika vitongoji 105 mkoani Mbeya inayosimamiwa na REA; kuendelea na utekelezaji wa mradi wa kuunganisha vitongoji 262 katika Wilaya ya Nyasa na Mbinga mkoani Ruvuma; vitongoji 358 wilayani Mpanda, Mlele na Tanganyika mkoani Katavi; kuendelea na usambazaji wa umeme katika maeneo ya Kilindi na Simanjiro; na kuanza ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilometa 128 kutoka Masasi hadi Mahumbika pamoja na kituo cha kupoza umeme.

**b) Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania (TCPM)**

216. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia kampuni tanzu ya TANESCO ya TCPM itaendelea na uzalishaji na usambazaji wa nguzo za zege kupitia kiwanda chake cha Tabora. Aidha, Serikali itaanza maandalizi ya awali ya ujenzi wa kiwanda cha pili kitakachokuwa kinamilikiwa na TCPM mkoani Mbeya pamoja na kuendelea na utaratibu wa kushirikiana na Wawekezaji Binafsi kujenga viwanda vya kuzalisha

nguzo za zege katika mikoa mbalimbali isiyokuwa na viwanda hivyo.

### c) Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC)

217. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia kampuni tanzu ya TANESCO ya TGDC itaendelea na utekelezaji wa miradi ya jotoardhi ambapo kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kukamilisha uhakiki wa rasilimali ya jotoradhi na kufanya tathmini ya visima vya uhakiki katika eneo la mradi wa Ngozi. Vilevile, Serikali itaajiri Mshauri Mwelekezi (*Drilling Consultant*) wa kusimamia programu ya uchorongaji wa visima vya uhakiki katika mradi wa Kiejo-Mbaka. Pia, kazi nyingine itakayofanyika ni kukamilisha utafiti wa kina wa kisayansi katika eneo la Natron mkoani Arusha. Jumla ya **Shilingi bilioni 25.00** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 2.33** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

## C.1.4 MIRADI YA NISHATI VIJIJINI

218. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA itaendelea kutekeleza programu na miradi mbalimbali ya nishati vijijini na vitongojini

ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya jamii katika maeneo hayo. Programu na miradi itakayotekelezwa ni kama ifuatavyo:

a) **Mradi wa Kupeleka Umeme katika Vitongoji Awamu ya Pili B (*Hamlet Eletrification Project – HEP IIB*)**

219. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi wa uunganishaji wa umeme katika vitongoji 9,009 kwa kujenga miundombinu ya kilomita 13,181 za njia za msongo wa kati, kilomita 14,016 za msongo mdogo, ufungaji wa transfoma 8,003 za kVA 100 na 1,006 za kVA 200 na uunganishaji wa wateja wa awali 290,300. Mradi unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia mwaka 2025/26 kwenye mikoa 25 (isipokuwa Dar es Salaam). Kwa mwaka 2026/27, jumla ya **Shilingi bilioni 20** fedha za ndani zitatumika kutekeleza mradi huu.

**b) Mradi wa Kupeleka Umeme katika Vitongoji Awamu ya Pili A (*Hamlet Eletrification Project – HEP IIA*)**

220. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi wa uunganishaji wa umeme katika vitongoji 3,060 vya Majimbo 204 ya Uchaguzi nchini sawa na wastani wa vitongoji 15 kwa kila Jimbo. Wigo wa mradi unahusisha ujenzi wa miundombinu ya kilomita 528 za njia ya msongo wa kati, kilomita 6,040 za msongo mdogo, ufungaji wa transfoma 3,056 na uunganishaji wa wateja wa awali 100,704. Jumla ya **Shilingi bilioni 75** fedha za ndani zitatumika kutekeleza mradi huu.

**c) Mradi wa Kuunganisha Wateja Vitongojini – *Universal Hamlet Eletrification and Last Mile Customer Connection***

221. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA itaendelea kutekeleza mradi wa kuongeza uunganishaji wa wateja vitongojini *(Universal Hamlet Eletrification and Last Mile Customers Connectivity)* ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Mahsusi wa Nishati

wa Taifa *(National Energy Compact)* ulioridhiwa katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika *(Mission 300)* mwezi Januari, 2025. Katika mwaka 2026/27, Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi huu katika mikoa mitatu ya Pwani, Morogoro na Dodoma ambao unalenga kusambaza umeme katika jumla ya mitaa 279. Aidha, Serikali itatekeleza mradi huu kwa kujumuisha vitongoji vya mikoa mingine iliyosalia. Jumla ya **Shilingi bilioni 188.8** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 127.98** fedha za nje zitatumika kutekeleza mradi huu.

**d) Mradi wa Kupeleka Umeme katika Vitongoji Mkoa wa Lindi (*Hamlet Electrification Project - Lindi*)**

222. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Norway itaendelea kutekeleza mradi wa kusambaza umeme katika Mkoa wa Lindi ambapo kazi zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme msongo wa kati yenye urefu wa kilomita 352.45, msongo mdogo wa kilomita 430 na kufunga transfoma 230. Lengo la mradi huu ni

kufikisha umeme katika vitongoji 230 ambapo wateja wa awali 7,590 wataunganishiwa umeme. Aidha, Serikali kupitia REA itaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu matumizi ya umeme katika shughuli za uzalishaji na matumizi ya nishati safi ya kupikia. Jumla ya **Shilingi bilioni 2.00** fedha za ndani zitatumika kutekeleza mradi huu.

**e) Mradi wa Ufungaji wa Mifumo ya Umeme Jua Visiwani (*Island Densification Project – IDP*)**

223. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha usambazaji na ufungaji wa mifumo ya jua inayojitegemea kwa wakazi 20,000 katika visiwa vidogo 143 vilivyopo katika Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Sambamba na kuendelea na utekelezaji wa mradi huu, Serikali kupitia REA itawaunganishia umeme jumla ya wateja 7,257, kati ya hao wateja 4,400 wataunganishwa na mifumo ya umeme jua inayojitegemea na wateja 2,857 wataunganishwa na gridi ndogo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa *National Energy Compact*. Jumla ya **Shilingi**

**bilioni 18** fedha za ndani zitatumika kutekeleza mradi huu.

### f) Mradi wa Kusambaza Umeme katika Vitongoji Pembezoni mwa Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki (EACOP)

224. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA kwa kushirikiana na Kampuni ya EACOP itaanza kutekeleza mradi wa kusambaza umeme katika vitongoji vilivyopo pembezoni mwa vituo vya kusukuma mafuta katika bomba la kusafirisha mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania katika mikoa nane (8) inayopitiwa na bomba hilo. Kazi zitakazofanyika ni kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme wa msongo wa kati ya urefu wa kilomita 18.42 na msongo mdogo ya urefu wa kilomita 40 katika vitongoji 17 vya mikoa ya Kagera (13) na Geita (4) ili kuunganisha wateja 759. Aidha, Serikali itaainisha wigo wa kazi katika mikoa ya Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga ikiwa ni hatua ya awali kabla ya kuanza ujenzi wa miundombinu ya umeme katika mikoa hiyo. Jumla ya **Shilingi bilioni 5.20** fedha za

ndani na **Shilingi bilioni 2.60** fedha kutoka Kampuni ya EACOP zitatumika kutekeleza kazi hizo.

### g) Mpango wa Matumizi ya Nishati kwa ajili ya Kuzalisha Mali – (*Productive Use of Energy*)

225. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA imekusudia kuendelea kuwezesha mpango wa kuhamasisha wananchi kutumia nishati kwa ajili ya kuzalisha mali ili kuongeza thamani ya mazao na huduma mbalimbali zikiwemo za umwagiliaji katika mashamba ya kilimo; mashine za kukoboa na kusaga nafaka mchangayiko; kuongeza thamani ya mazao ya bahari na maziwa ikiwemo mwani, dagaa na samaki; kuwezesha kuunganisha nishati katika viwanda vidogo vijijini; kuwezesha kuunganisha umeme katika migodi midogo ikiwemo Chunya (Mbeya) na kwa Msisi-Handeni (Tanga); na kuwezesha maeneo ya biashara kufikiwa na huduma za nishati ili kuboresha utolewaji wa huduma mbalimbali na kuongeza kipato kwa wananchi na Taifa.

226. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazofanyika ni kuwapata watoa huduma kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa vifaa; na kutoa ruzuku kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum pamoja na taasisi binafsi kwa ajili ya kuwapatia vifaa vya matumizi bora ya nishati. Jumla ya **Shilingi bilioni 3.00** fedha za ndani zitatumika kutekeleza Mpango huu.

**h) Mpango wa Kuwezesha Waendelezaji wa Nishati Jadidifu**

227. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA itaendelea kuwawezesha waendelezaji wa miradi ya nishati jadidifu katika maeneo yaliyo mbali na Gridi ya Taifa. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea kutoa ruzuku za ujenzi wa miradi hiyo na kutoa msaada wa kiufundi kwa waendelezaji hao ili kuwajengea uwezo wa kuendeleza miradi hiyo. Jumla ya **Shilingi bilioni 2.0** fedha za ndani zitatumika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

### C.1.5 UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA TAIFA WA MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

228. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi itaendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia wa Mwaka 2024 – 2034 ambapo kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kushirikiana na wadau kusambaza nishati safi ya kupikia na teknolojia zake kwa gharama nafuu; kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kupitia njia mbalimbali ikiwemo vyombo vya habari, ushiriki katika maonesho na mikutano ya kitaifa, kikanda na kimataifa na makongamano; na kuhamasisha Sekta Binafsi na Umma kushiriki katika kuimarisha upatikanaji wa malighafi na miundombinu ya uhakika ya nishati safi ya kupikia katika maeneo mbalimbali nchini. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia mijini na vijijini ikiwa ni pamoja na kuandaa, kuhuisha na kuoanisha Sera, Sheria, Kanuni na miongozo wezeshi itakayofanikisha matumizi ya nishati safi ya kupikia; na

kushirikiana na Taasisi za umma na binafsi ili kuongeza wigo wa tafiti na ubunifu wa teknolojia zinazohusu nishati safi ya kupikia. Jumla ya **Shilingi bilioni 10** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo. Hatua nyingine zitakazochukuliwa ni:

**a) Uwezeshaji wa Nishati Safi ya Kupika katika Kaya**

229. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA itaendelea na usambazaji wa mifumo mbalimbali ya nishati safi ya kupikia ikiwemo mitungi ya LPG, majiko banifu, na majiko ya umeme kwenye kaya 200,000 katika maeneo ya vijijini na vijiji-miji. Kazi zitakazofanyika ni kuwapata watoa huduma wa nishati safi ya kupikia na kusambaza mifumo ya nishati hizo katika mikoa 25 Tanzania Bara. Jumla ya **Shilingi bilioni 15.00** fedha za ndani zitatumika kwa ajili ya kazi hizo.

### b) Uwezeshaji wa Nishati Safi katika Taasisi Zinazohudumia Chakula Zaidi ya Watu 100 kwa Siku

230. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA itaendelea kuwezesha usambazaji wa mifumo mbalimbali ya nishati safi ya kupikia ikiwemo mifumo ya LPG, majiko banifu, mkaa mbadala pamoja na majiko ya umeme katika taasisi 300 zinazotoa huduma ya chakula kwa watu zaidi ya 100 kwa siku. Kazi zitakazofanyika ni kupata taasisi zitakazofungiwa mifumo hiyo kupitia fursa zitakazotangazwa na Serikali kupitia REA; kuwapata watoa huduma wa nishati safi ya kupikia; na kusimika mifumo hiyo kwa taasisi zitakazokidhi vigezo. Jumla ya **Shilingi bilioni 15.00** fedha za ndani zitatumika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

### c) Kuwezesha Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) Kusambaza Gesi Asilia katika Mkoa wa Pwani Awamu ya Pili

231. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA na TPDC zitaendelea kushirikiana kutekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu

ya kusambaza gesi asilia kwa ajili ya kupikia katika kaya 500 za Kijiji cha Kisemvule kilichopo Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani. Jumla ya **Shilingi bilioni 3.00** fedha za ndani zitatumika kutekeleza mradi huo.

### d) Uwezeshaji wa Mitambo ya Kutengeneza Mkaa Mbadala

232. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA itaendelea kutoa ruzuku kwa wajasiriamali vijana, wanawake na watu wenye mahitaji maalum ili kutengeneza mkaa mbadala na majiko banifu. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kupata vikundi vitakavyonufaika na kuwapata watoa huduma watakaosambaza mashine za kutengeneza mkaa na majiko hayo ili kusambaza huduma hizo kwa makundi hayo. Jumla ya **Shilingi bilioni 3.0** fedha za ndani zitatumika kugharamia mpango huu.

## C.1.6 KURATIBU, KUSIMAMIA NA KUFUATILIA UTEKELEZAJI WA MIPANGO NA MIKAKATI MBALIMBALI KATIKA SEKTA NDOGO YA UMEME NA NISHATI JADIDIFU

233. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kuandaa, kuhuisha na kutekeleza Mipango na Mikakati mbalimbali katika Sekta Ndogo ya Umeme na Nishati Jadidifu ili kuendeleza Sekta hiyo. Mipango na Mikakati hiyo ni pamoja na Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta Ndogo ya Umeme (*Power System Master Plan 2024 Update*); Mkakati wa Taifa wa Matumizi Bora ya Nishati (*National Energy Efficiency Strategy*) wa Mwaka 2024 – 2034; Mkakati wa Maboresho ya Sekta Ndogo ya Umeme (*Electricity Supply Industry Reform Strategy and Roadmap – ESI-RSR, 2025 - 2035*); Mpango Kabambe wa Kupeleka Nishati Vijijini (*Rural Energy Master Plan - REMP*) wa Mwaka 2022; Mkakati wa Taifa wa Nishati Jadidifu (*National Renewable Energy Strategy and its Implementation Roadmap*) wa Mwaka 2024 - 2034; na Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (*National Clean Cooking Strategy 2024 - 2034*).

234. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia itaendelea na utekelezaji wa Mpango Mahususi wa Taifa wa Nishati *(National Energy Compact 2025 - 2030)* ikiwa ni pamoja na kuunganishia umeme kaya 1,700,000 kwa mwaka, kuimarisha ushiriki wa Sekta Binafsi katika Sekta Ndogo ya Umeme na Nishati Jadidifu pamoja na uratibu wa utekelezaji wa Mpango huu ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 5.4** zimetengwa.

## C.2 SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ASILIA

235. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika mwaka 2026/27 itaendelea kusimamia na kuendeleza Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia ili kuhakikisha uhakika wa upatikanaji na usalama wa bidhaa za petroli na gesi asilia nchini. Miradi na kazi zitakazotekelezwa zinahusisha utafutaji, uendelezaji, uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa mafuta na gesi asilia kama ifuatavyo:

## C.2.1 MIRADI YA UTAFUTAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA KATIKA VITALU VYA KIMKAKATI

### a) Kitalu cha Eyasi – Wembere

236. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC itaendelea na shughuli za utafiti wa awali wa mafuta na gesi asilia katika Kitalu cha Eyasi–Wembere ambapo kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha awamu ya pili ya uchukuaji wa taarifa za mitetemo za mfumo wa 2D za urefu wa kilomita 321; kukamilisha, kuchakata na kutafsiri taarifa za mtetemo za mfumo wa 2D za urefu wa kilomita 1,360; na kuendelea na stadi za kijiolojia na kijiofizikia. Jumla ya **Shilingi bilioni 20** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo.

### b) Kitalu cha Lindi - Mtwara

237. ***Mheshimiwa* Spika,** Serikali kupitia TPDC itaendelea na kazi za utafiti wa awali wa mafuta na gesi asilia katika Kitalu cha Lindi-Mtwara ikiwa ni pamoja na kuchukua taarifa za mitetemo za mfumo wa 3D kwa awamu ya pili katika eneo la kilomita za

mraba 386.3; kukamilisha uchakataji na kutafsiri taarifa za mitetemo zilizochukuliwa katika eneo la kilomita za mraba 739.3 na kuendelea na stadi za kijiolojia na kijiofizikia. Aidha, Serikali kupitia TPDC itaendelea na kazi ya kumtafuta mbia wa kimkakati mwenye uzoefu, utaalamu na fedha kwa ajili ya kushirikiana nae katika kuendeleza kazi za kitalu hicho. Jumla ya **Shilingi bilioni 20** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo.

### c) Kitalu cha Songo Songo Magharibi

238. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC itaendelea na kazi za utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika Kitalu cha Songo Songo Magharibi kwa kukamilisha uchukuaji na uchakataji wa taarifa za mitetemo za mfumo wa 3D katika eneo la kilomita za mraba 421 zilizo katika kina kifupi cha bahari. Jumla ya **Shilingi bilioni 83.21** zimetengwa na TPDC kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo.

## C.2.2: MIRADI YA UENDELEZAJI NA UZALISHAJI WA GESI ASILIA

### a) Kitalu cha Uzalishaji wa Gesi Asilia cha Mnazi Bay

239. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa katika kitalu hiki ni pamoja na kuendelea na uzalishaji wa gesi asilia kulingana na mahitaji na kukamilisha kazi ya uchorongaji wa kisima cha utafiti (Kasa - 1). Jumla ya **Shilingi bilioni 81.04** zimetengwa na TPDC kwa ajili kutekeleza kazi hizo.

### b) Kitalu cha Ruvuma (Eneo la Ntorya)

240. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na mwekezaji itaendelea na shughuli za uendelezaji wa gesi asilia katika Kitalu cha Ruvuma eneo la Ntorya kwa kuchoronga kisima kimoja (1) cha utafutaji cha Chikumbi-1 na ukarabati wa visima viwili (2) vya Ntorya-1 & 2 vitakavyotumika katika uzalishaji wa gesi asilia. Kukamilika kwa kazi hizo kutawezesha kuanza uzalishaji ambapo kiasi cha futi za ujazo milioni 40 hadi 60 kinatarajiwa kuzalishwa kwa siku. Jumla ya **Shilingi bilioni 20.35**

zimetengwa na TPDC kwa ajili utekelezaji wa mradi huu.

### c) Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika *(Liquefied Natural Gas – LNG)*

241. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inashirikiana na makampuni ya kimataifa ya nishati katika utekelezaji wa mradi huu ambapo kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha majadiliano na kuandaa mikataba ya utekelezaji wa mradi kati ya Serikali na wawekezaji; kuandaa na kutekeleza mpango wa matumizi ya ardhi ya eneo la mradi; kushiriki katika utayarishaji wa Mpango wa Uendelezaji wa Mradi *(Project Development Plan);* na kuendelea na utoaji wa elimu na kuhamasisha wananchi kuhusu fursa na manufaa ya mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 20** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya shughuli hizo.

242. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia mradi huu Tanzania itatambulika kimataifa katika biashara ya LNG, mapato ya Serikali yatokanayo na mauzo ya gesi asilia yataimarika, uwekezaji katika utafutaji na uendelezaji wa gesi asilia nchini utaongezeka, ukuaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii utaimarika, matumizi ya gesi asilia nchini yataongezeka, na kuongezeka kwa fedha za kigeni nchini. Aidha, mradi utaongeza fursa za ushiriki wa Watanzania na kampuni za ndani katika mnyororo wa thamani wa gesi asilia.

## C.2.3: MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA USAFIRISHAJI WA GESI ASILIA

### a) Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Asilia kutoka Ntorya (Kitalu cha Ruvuma) hadi Kiwanda cha Kuchakata Gesi Asilia cha Madimba

243. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa bomba lenye urefu wa kilomita 34.2 la kusafirisha gesi asilia itakayozalishwa katika Kitalu cha Ruvuma eneo la Ntorya hadi kiwanda cha kuchakata

gesi asilia cha Madimba. Bomba hilo linatarajiwa kuwa na uwezo wa kusafirisha gesi asilia takriban futi za ujazo milioni 140 kwa siku kwa ajili ya kuchakatwa katika kiwanda hicho na kuingizwa katika miundombinu ya Taifa ya usafirishaji na usambazaji wa gesi asilia kwa matumizi mbalimbali nchini. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi ghafi yenye mgandamizo mkubwa na miundombinu yake. Jumla ya **Shilingi bilioni 21.82** zimetengwa na TPDC kwa ajili utekelezaji wa mradi huu.

**b) Upanuzi wa Kiwanda cha Kuchakata Gesi cha Madimba – (*Madimba Gas Processing Plant Expansion*)**

244. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC imepanga kuongeza mtambo mmoja (1) mpya wenye uwezo wa kuchakata futi za ujazo milioni 70 kwa siku katika kiwanda cha Madimba ili kukidhi ongezeko la kiasi cha gesi kinachotarajiwa kuchakatwa kwa siku kutokana na ongezeko la uzalishaji kutoka visima vya Ntorya na Mnazi Bay. Kwa sasa kiwanda kina uwezo wa kuchakata futi za ujazo milioni 210 kwa

siku ambapo baada ya upanuzi huo uwezo wa kiwanda utafikia futi za ujazo milioni 280 kwa siku. Jumla ya **Shilingi bilioni 143.2** zimetengwa na TPDC kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

**c) Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Gesi Asilia kutoka Kinyerezi - Dar es Salaam hadi Chalinze – Pwani**

245. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa bomba lenye urefu wa kilomita 93 la kusafirisha gesi asilia yenye mgandamizo mkubwa kutoka kituo cha kupokelea gesi asilia kilichopo Kinyerezi - Dar es Salaam hadi Chalinze. Bomba hilo litawezesha upatikanaji wa gesi asilia katika maeneo ya kongani ya viwanda Zegereni - Kibaha, viwanda vya Mlandizi, Bandari Kavu ya Kwala na Chalinze na hivyo kuchochea kasi ya maendeleo ya kiuchumi na viwanda katika ukanda husika. Kazi zitakazotekelezwa ni kukamilisha usanifu wa mradi na kuanza maandalizi ya awali ya ujenzi wa bomba. Jumla ya **Shilingi bilioni 121.70** zimetengwa na TPDC kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

## C.2.4: MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA USAMBAZAJI WA GESI ASILIA

246. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inaendelea kuongeza mtandao wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia katika maeneo mbalimbali nchini ili kuongeza kasi ya matumizi ya gesi asilia kwa shughuli mbalimbali ikiwemo uzalishaji wa umeme, viwandani, vyombo vya moto, katika taasisi na majumbani. Ili kuongeza mtandao wa usambazaji wa gesi asilia nchini, Serikali kupitia TPDC imejipanga kutekeleza miradi ifuatayo:

### a) Miradi ya Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani

#### i) Ujenzi wa Miundombinu ya Usambazaji wa Gesi Asilia Katika Mkoa wa Dar es Salaam

247. ***Mheshimiwa Spika*** mradi huu unalenga kujenga mtandao wa usambazaji wa gesi asilia katika maeneo mbalimbali yaliyo karibu na miundombinu ya gesi asilia jijini Dar es Salaam. Kazi zitakazotekelezwa

ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia na kuunganisha wateja wapya 1,000 kwa ajili ya matumizi ya taasisi na majumbani katika maeneo ya Ubungo, Sinza, Mikocheni na Lugalo Barracks. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii katika maeneo ya Upanga, Muhimbili, Masaki, Kawe na Mbweni kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa bomba la kusambaza gesi asilia. Jumla ya **Shilingi bilioni 6.00** zimetengwa na TPDC kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

**ii) Ujenzi wa Bomba la Kusambaza Gesi Asilia kutoka Kisemvule hadi Mbagala**

248. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia kutoka eneo la Kisemvule mkoani Pwani hadi kituo cha CNG kilichopo Mbagala pamoja na kufikisha huduma ya gesi kwa wateja wa viwandani waliopo katika eneo la viwanda Zakhiem. Pia, mradi unahusisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia kwa ajili ya kuwaunganishia wateja wa viwandani. Shughuli za ujenzi zitaanza

kutekelezwa katika mwaka 2026/27 ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 8.23** zimetengwa na TPDC kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizo.

### b) Mradi wa Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mikoa ya Lindi na Mtwara

249. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kusambaza miundombinu ya gesi asilia katika maeneo ya Mtwara Mjini, hususan Soko la Samaki la Mtwara, maeneo ya Kata ya Shangani, maeneo ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, nyumba za makazi ya watumishi wa Benki Kuu - Mtwara, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, pamoja na taasisi mbalimbali za Serikali, majengo ya biashara, hoteli, migahawa na makazi yaliyopo katika eneo hilo. Kazi zitakazotekelezwa ni kukamilisha taratibu za kuanza kwa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji na kuunganisha taasisi na wateja wa majumbani kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Jumla ya **Shilingi bilioni 5.20** zimetengwa na TPDC kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizo.

### c) Ujenzi wa Vituo vya Kugandamiza na Kusambaza Gesi Asilia *(Compressed Natural Gas – CNG)*

250. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC itaendelea na ujenzi wa vituo vinavyohamishika vya kusambaza gesi asilia iliyoshindiliwa *(Mobile CNG stations)* kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa gesi asilia katika Mikoa iliyo mbali na miundombinu ya gesi hiyo. Usambazaji huo utafanyika kwa kutumia magari maalum ya kusafirisha gesi *(CNG trucks)* kutoka vituo mama vilivyopo Dar es Salaam na kufikisha katika maeneo husika. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na usimikaji wa vituo vitano (5) katika mikoa ya Dar es Salaam (2), Morogoro (1) na Dodoma (2). Vilevile, Serikali kupitia TPDC itaendelea na utafutaji wa maeneo na kuanza kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii katika mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha kwa ajili ya ujenzi wa vituo viwili (2) kwa kila Mkoa. Jumla ya **Shilingi bilioni 22.06** zimetengwa na TPDC kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizo.

**d) Mradi wa Usambazaji wa Gesi Asilia – Mtumba, Dodoma**

251. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kujenga miundombinu ya kusambaza gesi asilia katika Mji wa Serikali Mtumba – Dodoma. Utekelezaji wa mradi unahusisha ujenzi wa kituo cha kupokelea gesi (*Gas Receiving Terminal*) itakayosafirishwa na magari maalum kutoka kituo mama cha CNG kilichopo Mlimani City - Dar es Salaam; na ujenzi wa kituo cha kupunguza mgandamizo, mtandao wa usambazaji pamoja na kituo cha kujazia gesi asilia kwenye magari. Mtandao huo utaunganisha majengo ya Wizara, ofisi za Balozi, taasisi mbalimbali za Serikali, majengo ya biashara, hoteli, migahawa pamoja na makazi yaliyopo katika eneo hilo. Kazi zitakazotekelezwa ni kukamilisha Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii na kuanza taratibu za kumpata mkandarasi wa ujenzi wa mtandao wa usambazaji wa gesi hiyo. Jumla ya **Shilingi bilioni 14.40** zimetengwa na TPDC kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizo.

## C.2.5: MIRADI YA KUSAFIRISHA GESI ASILIA KWENDA NCHI JIRANI ZA UGANDA NA KENYA

252. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza azma ya kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara ya gesi asilia Afrika, Serikali itaendelea na maandalizi ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa bomba la gesi asilia kutoka Dar es Salaam (Tanzania) kwenda nchi za Uganda na Kenya ambapo kwa upande wa bomba la kwenda Uganda kazi zitakazofanyika ni kuendelea na Upembuzi Yakinifu na kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii. Aidha, kwa upande wa bomba la kwenda nchini Kenya Serikali inatarajia kuanza taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi atakayesimamia mradi huu. Jumla ya **Shilingi bilioni 4.18** zimetengwa na TPDC kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizo.

## C.2.6: MIRADI YA KUSAFIRISHA NA KUHIFADHI MAFUTA

### a) Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania *(East African Crude Oil Pipeline - EACOP)*

253. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC kwa kushirikiana na Kampuni ya EACOP itaendelea na utekelezaji wa mradi wa EACOP ambapo Serikali kwa kushirikiana na Kampuni hiyo itaendelea na ujenzi wa bomba, matenki ya kupokelea mafuta na gati inayoendelea kujengwa Chongoleani – Tanga kwa ajili ya upakiaji wa mafuta katika meli. Aidha, Serikali itafanya tathmini ya matumizi ya baadhi ya maeneo ya makambi ya ujenzi pamoja na karakana iliyopo Sojo – Tabora ili maeneo hayo yaweze kunufaisha wananchi baada ya mradi kukamilika. Vilevile, wananchi wataendelea kuelimishwa kuhusu utekelezaji wa mradi na fursa zilizopo hususan katika maeneo yanayopitiwa na mradi sambamba na kutekeleza miradi ya uwajibikaji kwa jamii katika sekta za elimu, afya, maji, mazingira na miundombinu. Jumla ya **Shilingi bilioni**

**100** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuchangia utekelezaji wa mradi huu.

### b) Mradi wa Bomba Jipya la Kusafirisha Mafuta Safi kutoka Tanzania hadi Zambia (*New TAZAMA Pipeline*)

254. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha majadiliano na kuandaa mikataba ya uendeshaji wa mradi kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Zambia, kufanya usanifu wa kihandisi *(Front End Engineering Design – FEED)* pamoja na Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA). Jumla ya **Shilingi bilioni 5.00** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

### c) Mradi wa Ukarabati wa Tenki Namba 8 – Kigamboni, Dar es Salaam

255. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC itaendelea na ukarabati wa Tenki Namba 8 lililopo katika eneo la TIPER – Kigamboni, Dar es Salaam lenye uwezo wa

kuhifadhi mafuta lita milioni 45. Kukamilika kwa Tenki hili kutaongeza uwezo wa kuhifadhi mafuta nchini. Jumla ya **Shilingi bilioni 9.72** zimetengwa na TPDC kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

## C.2.7: UTENDAJI WA KAMPUNI TANZU ZA TPDC

### a) TANOIL Investments Limited (TANOIL)

256. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TANOIL itaendelea kushiriki katika biashara ya kununua na kuuza mafuta kwa jumla na rejareja pamoja na kuanza biashara ya LPG na vilainishi vya vyombo vya moto na mitambo. Jumla ya **Shilingi bilioni 78.21** zimetengwa na TPDC kupitia TANOIL kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

### b) GAS Company (T) Limited (GASCO)

257. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia GASCO itaendelea kutekeleza majukumu yake ya uendeshaji na matengenezo ya miundombinu ya gesi asilia nchini pamoja na vituo vya CNG vinavyomilikiwa na

Serikali. Vilevile, Serikali kupitia kampuni hiyo itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia majumbani, kwenye taasisi, viwandani na katika vituo vya CNG. Jumla ya **Shilingi bilioni 124.18** zimetengwa na TPDC kupitia GASCO kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

### C.2.8: UDHIBITI WA MASUALA YA MKONDO WA JUU WA PETROLI KUPITIA PURA

258. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia PURA itaendelea kusimamia na kudhibiti shughuli za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia nchini. Usimamizi huo utajumuisha kuandaa Mpango wa Tafiti za Awali *(Reconnaissance Survey)* kwa maeneo yenye viashiria vya mafuta na gesi asilia; kugawanya maeneo katika vitalu vya utafutaji *(block demarcation)*; kuandaa taarifa za kina za kijiolojia na kijiofizikia katika vitalu vitakavyoingizwa kwenye mnada; kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii katika maeneo ya utafutaji pamoja na kushiriki katika maonesho na makongamano mbalimbali ya mafuta na gesi asilia kwa lengo la

kufanikisha Duru ya Tano ya Kunadi Vitalu vya Utafutaji. Jumla ya **Shilingi bilioni 4.00** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli hizo.

## C.2.9: UDHIBITI WA MASUALA YA NISHATI KUPITIA EWURA

259. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia EWURA itaendelea kusimamia na kudhibiti Sekta ya Nishati nchini kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma zilizo bora na uhakika na maendeleo ya Sekta. Usimamizi na udhibiti huo utafanyika kwa kutoa vibali vya ujenzi wa miundombinu, leseni za biashara pamoja na kufanya kaguzi mbalimbali kwa ajili ya kuhakiki ubora wa miundombinu, bidhaa za petroli na gesi asilia. Aidha, ili kuboresha usimamizi wa Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia, EWURA itaendelea kuboresha mfumo wa kidijitali wa usimamizi wa biashara ya mafuta na gesi asilia kuanzia uagizaji, usambazaji na uuzaji kwenye vituo vya mafuta na gesi asilia.

## C.2.10: URATIBU WA UAGIZAJI WA MAFUTA KWA PAMOJA

260. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia PBPA itaendelea kuratibu shughuli za uagizaji wa mafuta kwa pamoja kwa kutumia mfumo wa BPS. Aidha, PBPA itaendelea kuboresha mfumo wa usimamizi wa BPS (*BPS Management Information System*) ambao unalenga kuwezesha shughuli zote za BPS kufanyika kidijitali ikiwemo usajili wa kampuni za mafuta; uthibitishaji wa awali wa kampuni zinazoshiriki kwenye zabuni za uletaji mafuta nchini; maoteo ya mahitaji ya mafuta; usimamizi wa zabuni; usafirishaji wa mafuta; na masuala ya fedha. Vilevile, mfumo huo utasomana na mifumo ya taasisi nyingine za Serikali zinazoshirikiana na PBPA katika uagizaji wa mafuta. Jumla ya **Shilingi bilioni 3.00** zimetengwa na PBPA kwa ajili ya kazi hiyo.

## C.2.11 KUIMARISHA UTENDAJI KAZI NA UTOAJI HUDUMA

261. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio katika utekelezaji wa mipango ya Wizara yanahitaji rasilimaliwatu toshelevu na yenye sifa, maarifa, ujuzi na ubunifu. Wizara kwa

kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora itaendelea kuimarisha utendaji kazi kwa watumishi wa umma kwa kuboresha mazingira ya kazi pamoja na kuongeza motisha kwa watumishi. Katika mwaka 2026/27 Wizara na Taasisi zake zitaendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kuzingatia Mpango wa Mafunzo ambapo jumla ya watumishi 5,207 watapatiwa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ndani na nje ya nchi katika nyanja mbalimbali ili kuboresha utendaji kazi na kuimarisha huduma bora kwa wananchi.

262. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza fursa ya ajira pamoja na kuendana na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma, Wizara na Taasisi zake zitaajiri watumishi 1,439 na kuwapandisha vyeo watumishi 933. Vilevile, Wizara itaendelea kutekeleza programu mbalimbali zinazolenga kulinda na kuimarisha nguvukazi ya Wizara, ikiwemo udhibiti wa Magonjwa Sugu na Yasiyoambukizwa, Afya ya Akili, maambukizi ya VVU/UKIMWI, pamoja na kuendelea na kudhibiti masuala ya rushwa

kwa kutoa elimu pamoja na kuanzisha mifumo mbalimbali ya TEHAMA.

## D. USHIRIKISHWAJI WA SEKTA BINAFSI KATIKA SEKTA YA NISHATI

263. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kuvutia Sekta Binafsi ili iweze kushiriki katika utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali ya Sekta ya Nishati nchini ikiwemo uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme pamoja na mnyororo wa thamani wa mafuta na gesi asilia. Aidha, Serikali itaendelea kuandaa na kuhuisha miongozo mbalimbali ya umeme kwa lengo la kuendelea kuvutia wawekezaji binafsi kuwekeza katika sekta hiyo.

264. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kushirikiana na Sekta Binafsi katika miradi ya nishati vijijini ambapo kupitia REA, itaendelea kuziwezesha na kuzisimamia kampuni binafsi zinazotekeleza programu na miradi mbalimbali ya nishati vijijini na vitongojini. Pia, Serikali kupitia REA itaendelea kutoa fursa za mikopo nafuu kwa waendelezaji wa vituo vya mafuta vijijini kupitia utaratibu ulioainishwa kwenye Mwongozo wa Kutekeleza

Mradi wa Kuwezesha Ujenzi wa Vituo Vidogo vya Kuuza Mafuta Vijijini.

265. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia Serikali itaendelea kushirikisha Sekta Binafsi katika shughuli za utafutaji, uendelezaji, uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa mafuta na gesi asilia nchini. Aidha, ili kuhakikisha gesi asilia iliyopo nchini inaendelea kuwanufaisha watanzania, Serikali kupitia TPDC itaendelea kutoa idhini kwa wawekezaji binafsi kujenga vituo vya CNG katika maeneo mbalimbali nchini. Vilevile, Serikali kupitia EWURA itaendelea kutoa vibali na leseni za ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza mafuta na gesi asilia kwa Sekta Binafsi ili kuendelea kuongeza ushiriki wa sekta hiyo katika shughuli za mkondo wa kati na wa chini wa mafuta na gesi asilia.

## E. SHUKRANI

266. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kuendelea kuwashukuru Viongozi wenzangu katika Wizara ya Nishati, Mhe. Salome Wycliffe Makamba (Mb.), Naibu Waziri wa

Nishati; Mhandisi Felchesmi Jossen Mramba, Katibu Mkuu (Umeme na Nishati Jadidifu); na Dkt. James Peter Mataragio, Katibu Mkuu (Mafuta na Gesi Asilia) kwa namna wanavyonisaidia kuhakikisha majukumu tuliyokasimiwa yanatekelezwa ipasavyo kwa tija na ufanisi. Niendelee kuwashukuru pia Wakuu wa Idara na Vitengo, Wenyeviti wa Bodi, Wakuu wa Taasisi na watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa ujumla, kwa jitihada wanazoweka katika kuhakikisha malengo ya Wizara yanafikiwa. Aidha, naishukuru Sekta Binafsi na wananchi kwa ujumla kwa michango yao katika kuboresha usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Nishati. Vilevile, napenda kuvishukuru vyombo vya habari kwa ushirikiano wanaotupatia katika kutoa elimu na hamasa kwa umma kuhusu masuala ya nishati. Ni matumaini yangu kuwa, ushirikiano huu utazidi kuimarika katika mwaka 2026/27 kwa manufaa ya Taifa letu na Wananchi wake kwa ujumla.

## E.1: USHIRIKIANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA KATIKA SEKTA YA NISHATI

267. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2025/26 yalichangiwa pia na ushirikiano ambao Wizara iliupata kutoka kwa Wadau mbalimbali. Kwa niaba ya Serikali napenda kuwashukuru Washirika wa Maendeleo, Jumuiya na nchi wahisani ambao wameendelea kutoa michango yao katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara. Napenda kutambua mchango wa: Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Abu - Dhabi Fund for Development (ADFD), Economic Development Cooperation Fund (EDCF - Korea), Exim Bank (China), KfW (Germany), OPEC Fund for International Development, SWISS, Swedfund, Sida (Sweden), Saudi Fund for Developmnet (SFD), Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Umoja wa Ulaya (EU). Mashirika mengine ni Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA), Shirika la Mitaji ya Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNCDF), Geothermal Risk Mitigation Facility (GRMF), Arab Bank

for Economic Development in Afrika (BADEA), Shirika la Fedha Duniani (IMF), Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO), Shirika la Maendeleo la Canada (CIDA) pamoja na Shirika la Maendeleo la Uingereza (UKAid).

***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii pia kuzishukuru kwa dhati Serikali za Afrika Kusini, Algeria, Angola, Burundi, Canada, China, Ethiopia, Falme za Kiarabu, Japan, India, Indonesia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Korea Kusini, Malawi, Misri, Morocco, Msumbiji, Namibia, Norway, Oman, Rwanda, Saudi Arabia, Sweden, Ufaransa, Uganda, Uingereza, Ujerumani, Urusi, Zambia na nchi nyingine kwa kuendelea kushirikiana na Tanzania katika kuendeleza Sekta ya Nishati. Nazishukuru pia Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Umoja wa Afrika (AU) kwa ushirikiano katika masuala ya kikanda yanayohusu uendelezaji wa Sekta ya Nishati. Nizishukuru pia kampuni za Equinor Tanzania As, Shell Exploration and Production (T) Limited, Exxon Mobil na Ophir Energy, kwa ushirikiano zinazotupa

katika kufanikisha utekelezaji wa mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia Kuwa Kimiminika (*Liquefied Natural Gas – LNG*).

## F. HITIMISHO

268. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara ya Nishati katika mwaka 2026/27, itaendelea kuchukua hatua za kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na umeme wa kutosha unaokidhi mahitaji ya ndani na ziada itakayoweza kuuzwa nje ya nchi na kutupatia fedha za kigeni; kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika mijini, vijijini na vitongojini na kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini. Aidha, mkazo utaelekezwa katika shughuli za utafutaji, uendelezaji, uzalishaji na usambazaji wa mafuta na gesi asilia, kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta; pamoja na ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhi na kusambaza bidhaa hizo.

269. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Bajeti ya jumla ya **Shilingi Trilioni Mbili, Bilioni Mia Tano Ishirini na Tano, Milioni Mia Nne na Moja, Mia Moja Ishirini na Tisa Elfu (Shilingi 2,525,401,129,000)** kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa mwaka 2026/27. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:

**(i)** **Shilingi Trilioni Mbili, Bilioni Mia Nne Sitini na Mbili, Milioni Mia Tatu Sitini na Nne, Mia Nane Thelathini na Sita Elfu (Shilingi 2,462,364,836,000)** sawa na **asilimia 97.5** ya Bajeti yote ya Wizara ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Sita na Mbili, Milioni Mia Nne Arobaini na Tisa, Mia Saba Thelathini na Tano Elfu (Shilingi 1,602,449,735,000)** ni fedha za ndani, na **Shilingi Bilioni Mia Nane Hamsini na Tisa, Milioni Mia Tisa Kumi na Tano, Mia Moja na Moja Elfu (Shilingi 859,915,101,000)** ni fedha za nje; na

(ii) **Shilingi Bilioni Sitini na Tatu, Milioni Thelathini na Sita, Mia Mbili Tisini na Tatu Elfu (Shilingi 63,036,293,000)** sawa na **asilimia 2.5** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni Hamsini na Mbili, Milioni Mia Tisa Thelathini na Tisa, Sabini na Tano Elfu (Shilingi 52,939,075,000)** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi Bilioni Kumi, Milioni Tisini na Saba, Mia Mbili Kumi na Nane Elfu (Shilingi 10,097,218,000)** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) ya Watumishi wa Wizara na Taasisi ya PURA.

270. ***Mheshimiwa Spika,*** mwisho naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Pamoja na hotuba hii, vimeambatishwa vielelezo mbalimbali ambavyo vinafafanua masuala muhimu yanayohusu Sekta ya Nishati. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani ya *www.nishati.go.tz*

271. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.

***Kiambatisho Na. 1:*** **Uwezo wa Mitambo ya Kuzalisha Umeme Iliyounganishwa katika Gridi ya Taifa hadi Machi, 2026**

| **A.** | **Mitambo ya Maji** | **Uwezo (MW)** |
|---|---|---|
| 1. | JNHPP | 2,115.00 |
| 2. | Kidatu | 204.00 |
| 3. | Kihansi | 180.00 |
| 4. | Mtera | 80.00 |
| 5. | New Pangani Falls | 68.00 |
| 6. | Rusumo | 26.67 |
| 7. | Hale | 21.00 |
| 8. | Nyumba ya Mungu | 8.00 |
| 9. | Uwemba | 0.84 |
| 10 | Mwenga | 4.00 |
| 11 | Yovi | 1.00 |
| 12 | Matembwe | 0.59 |
| 13 | Darakuta | 0.32 |
| 14 | Luponde | 0.90 |
| 15 | Andoya | 1.00 |
| 16 | Tulila | 5.00 |
| 17 | Igola | 2.00 |
| 18 | Injangala | 0.36 |
| 19 | SUMA HPP | 4.00 |
| **Jumla ya Uwezo wa Mitambo ya Maji** | | **2,722.68** |
| **B.** | **Mitambo ya Gesi Asilia** | |
| 1. | SONGAS | 189.00 |
| 2. | Ubungo I | 102.00 |
| 3. | Tegeta | 45.00 |
| 4. | Ubungo II | 129.00 |
| 5. | Ubungo III | 72.50 |
| 6. | Kinyerezi I | 335.00 |
| 7. | Kinyerezi II | 248.22 |

| | | |
|---|---|---|
| **Jumla ya Uwezo wa Mitambo ya Gesi Asilia** | | **1,120.72** |
| **C.** | **Mitambo ya Mafuta** | |
| 1. | Zuzu | 7.44 |
| 2. | Nyakato Plant | 63.00 |
| 3. | Biharamulo | 1.50 |
| 4. | Songea | 5.74 |
| 5. | Liwale | 0.85 |
| 6. | Tunduru | 0.42 |
| 7. | Ludewa | 1.27 |
| 8. | Inyonga | 1.93 |
| 9. | Ngara | 1.25 |
| 10 | Kasulu | 4.55 |
| 11 | Kibondo | 2.50 |
| 12 | Kigoma | 8.75 |
| **Jumla ya Uwezo wa Mitambo ya Mafuta** | | **99.20** |
| **D.** | **Tungamotaka** | |
| 1. | TANWAT | 1.50 |
| 2. | TPC | 9.00 |
| 3. | Kilombero Sugar | 10 |
| 4. | Bagamoyo Sugar | 1.5 |
| **Jumla ya Tungamotaka** | | **22** |
| **E.** | **Umeme wa Jua** | |
| 1. | Kishapu Solar | 50.00 |
| 2. | Solar Wazi | 5.00 |
| 3. | Ushetu Solar | 5.00 |
| 4. | Bukombe Solar | 5.00 |
| **Jumla ya Umeme wa Jua** | | **65.00** |
| **JUMLA KUU KATIKA GRIDI YA TAIFA** | | **4,029.60** |

Chanzo: **TANESCO**

***Kiambatisho Na.2A:*** **Wazalishaji wa Umeme wa Kujitegemea Nje ya Gridi ya Taifa**

| Na | Kampuni | Eneo | Chanzo | Uwezo (MW) |
|---|---|---|---|---|
| | TANWAT | Njombe | Tungamotaka | 3.25 |
| | TPC | Kilimanjaro | Tungamotaka | 33.50 |
| | Kilombero Sugar | Morogoro | Tungamotaka | 2.55 |
| | Bagamoyo Sugar | Pwani | Tungamotaka | 3.50 |
| | Ngombeni Power Limited | Pwani | Tungamotaka | 1.40 |
| | Mkulazi Holding Company Limited | Morogoro | Tungamotaka | 15.00 |
| | Kilombero Plantations Limited | Morogoro | Tungamotaka | 1.69 |
| | Kagera Sugar Limited | Kagera | Tungamotaka | 27.20 |
| | Mufindi Paper Mills Limited | Iringa | Tungamotaka | 10.40 |
| | Mtibwa Sugar Estates Limited | Morogoro | Tungamotaka | 15.00 |
| | Lake Cement Limited | Dar es Salaam | Makaa ya Mawe | 15.40 |
| | Maweni Limestone Limited | Tanga | Makaa ya Mawe | 30.00 |

| Na | Kampuni | Eneo | Chanzo | Uwezo (MW) |
|---|---|---|---|---|
| | Dangote Cement Limited | Mtwara | Gesi | 50.00 |
| | Tanzania Cigarette Public Limited Company | Dar es Salaam | Gesi | 4.70 |
| | Kioo Limited | Dar es Salaam | Gesi | 12.20 |
| | Gas Company T LTD - GASCO | Lindi | Gesi | 10.70 |
| | Gas Company T LTD - GASCO | Mtwara | Gesi | 3.16 |
| | TPDC | Dar es Salaam | Gesi | 1.20 |
| | ALAF Limited | Dar es Salaam | Gesi | 4.00 |
| [illegible] | Tanga Cement Public Limited Company | Tanga | Mafuta Mazito | 11.48 |
| [illegible] | Shanta Mine Co. Ltd | Songwe | Mafuta Mazito | 8.20 |
| [illegible] | Stamigold Company Limited | Kagera | Mafuta Mazito | 7.00 |
| [illegible] | North Mara Goldmine Ltd | Mara | Mafuta Mazito | 18.00 |

| Na | Kampuni | Eneo | Chanzo | Uwezo (MW) |
|---|---|---|---|---|
| [illegible] | Nyati Mineral Sands Limited | Dar es Salaam | Mafuta Mazito | 2.00 |
| [illegible] | SBC Tanzania Limited | Dar es Salaam | Mafuta Mazito | 4.50 |
| [illegible] | Geita Gold Mining Limited | Geita | Mafuta Mazito | 47.00 |
| [illegible] | Buckreef Gold Co. Limited | Geita | Mafuta Mazito | 4.72 |
| [illegible] | Bulyanhulu Goldmine Ltd | Shinyanga | Mafuta Mazito | 40.00 |
| [illegible] | Tulila Hydro Electric Plant Co. Ltd | Ruvuma | Maji | 2.50 |
| [illegible] | Luponde Hydro Limited | Njombe | Maji | 0.16 |
| [illegible] | Madope Hydro Company Limited | Njombe | Maji | 1.84 |
| [illegible] | Darakuta | Manyara | Maji | 0.13 |
| [illegible] | Mwenga | Iringa | Upepo | 2.40 |
| **Jumla** | | | | **394.78** |

Chanzo**: EWURA**

***KIAMBATISHO Na.2B:*** **Mitambo Inayomilikiwa na TANESCO Iliyopo Nje ya Gridi ya Taifa**

| KITUO | Uwezo wa Mitambo (MW) |
|---|---|
| Mtwara I | 30.40 |
| Mtwara II | 40.00 |
| Somanga | 7.50 |
| **Jumla ya Mitambo inayotumia Gesi Asilia** | **77.90** |
| Bukoba | 2.56 |
| Mafia | 5.20 |
| Sumbawanga | 5.00 |
| Mpanda | 7.50 |
| **Jumla ya Mitambo inayotumia Mafuta** | **20.26** |
| **JUMLA YA UZALISHAJI NJE YA GRIDI YA TAIFA** | **98.16** |

Chanzo: **TANESCO**

***Kiambatisho Na. 3:*** **Miradi ya Gridi Imara Inayoendelea**

| Na. | Mradi unaotekelezwa | Hatua ya Utekelezaji Iliyofikiwa kufikia Machi, 2026 (Asilimia) |
|---|---|---|
| 1 | Shinyanga - Simiyu TL and Substation | 53 |
| 2 | Mkata - Kilindi TL &SS | 31 |
| 3 | Songea Tunduru TL and Substation | 51 |
| 4 | Tunduru Masasi TL and Substation | 6 |
| 5 | Ilala-Mabibo- Ubungo-Kimara 220kV transmission line | 34 |
| 6 | Mabibo Substation | 74 |
| 7 | Zegereni Substation | 3 |
| 8 | Pugu to Dundani Transmission Line | 13 |

| Na. | Mradi unaotekelezwa | Hatua ya Utekelezaji Iliyofikiwa kufikia Machi, 2026 (Asilimia) |
|---|---|---|
| 9 | Kiyungi - RomboTL 132kV and Substation | 15 |
| 10 | Kasiga Lushoto Transmission line and substation | 13 |
| 11 | 8 feeders from Lemugur SS Arusha | 62 |
| 12 | Mkata Substation and MV line (Mkata - KwaMsisi) | 22 |
| 13 | Transmission line from Ubungo to Ununio | 34 |
| 14 | Additional transformer at Dege substation | 68 |
| 15 | Urambo Kigoma TL Phase II | 52 |
| 16 | Bunda - Ukerewe TL and Substation | 26 |
| 17 | 400/220/33kV Shinyanga Substation | 44 |
| 18 | Mugumu Switching Station | 74 |
| 19 | Zuzu - Mbande Distribution Line Lot | 98 |
| 20 | 220kV Masasi Mahumbika Transmission Line & Substations | 1 |

Chanzo: **TANESCO**

***Kiambatisho Na. 4*: Vituo vya Kupoza Umeme Vilivyofanyiwa Maboresho**

| Na. | Kituo | Uwezo wa Kituo Kabla ya Maboresho (MVA) | Maboresho Yaliyofanyika |
|---|---|---|---|
| **I:Vituo vya Kupoza Umeme Vilivyofanyiwa Maboresho na Kukamilika** | | | |
| 1. | Njiro | 2x60MVA, 220/132/33 & 2x50MVA, 132/33 kilovoti | Kuongeza mashine umba kubwa 90MVA, 220/132/33 kilovoti na kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kupeleka umeme mkoa wa Kilimanjaro na Tanga. |
| 2. | Makambako | 30MVA, 220/132/33 kilovoti | Kuongeza mashine umba kubwa 90MVA, 220/132/33 kilovoti kwa kufunga mashine umba kubwa |
| 3. | Kange - Tanga | 15MVA, 132/33 kilovoti | Kuongeza mashine umba kubwa 45MVA, 132/33 kilovoti |
| 4. | Chang'ombe | 15MVA, 33/11kilovoti | Kuongeza mashine umba 15MVA, 33/11kilovoti |
| 5. | Ibadakuli | 2x60MVA, 220/132kilovoti | Kuongeza mashine umba 50MVA, 220/132kilovoti |
| 6. | Mahumbika | 20MVA, 132/33kilovoti | Kuongeza mashine umba 15MVA, 132/33kilovoti |
| 7. | Mlandizi | 90MVA, 132/33 kilovoti | Kuongeza mashine umba 50MVA, 132/33kilovoti |

| Na. | Kituo | Uwezo wa Kituo Kabla ya Maboresho (MVA) | Maboresho Yaliyofanyika |
|---|---|---|---|
| 8. | Dodoma Mjini | 15MVA, 33/11 kilovoti | Kuongeza mashine umba mbili za 20MVA, 33/11 kilovoti |
| 9. | Mwanza Kusini | 2x10MVA, 33/11 kilovoti | Upanuzi wa kituo cha kupoza umeme kwa kuongeza mashine umba kubwa 20MVA, 33/11 kilovoti |
| 10. | Mbagala | 30MVA, 33/11 kilovoti | Upanuzi wa kituo cha kupoza umeme kwa kuongeza mashine umba 20MVA, 33/11 kilovoti |
| **II: Vituo vya Kupoza Umeme Vinavyoendelea Kufanyiwa Maboresho** | | | |
| 11. | Lusu | 15MVA, 132/33 kilovoti | 60MVA, 132/33 kilovoti |
| 12. | Kiyungi – Kilimanjaro | 20MVA, 132/33 kilovoti, 19.9MVA, 132/66 kilovoti, 50MVA, 132/33 kilovoti | 120MVA, 132/33 kilovoti |
| 13. | Nyakato | 2X60MVA, 220/132/33 kilovoti, 55MVA, 220/132/33 kilovoti | 150MVA, 132/33 kilovoti |
| 14. | Majani mapana | 2X55MVA, 132/33 kilovoti | Kuongeza mashine umba 55MVA, 132/33 kilovoti & 45MVAr STATCOM |

| Na. | Kituo | Uwezo wa Kituo Kabla ya Maboresho (MVA) | Maboresho Yaliyofanyika |
|---|---|---|---|
| 15. | Mbulu | 20MVA, 66/33 kilovoti | Kuongeza mashine umba 20MVA, 66/33 kilovoti |
| 16. | Sahare | 20MVA, 33/1 kilovoti | Kuongeza mashine umba 20MVA, 33/11 kilovoti |
| 17. | Mzinga | 5MVA, 33/1 kilovoti | Kuongeza mashine umba 20MVA, 33/11 kilovoti |
| 18. | Ilala | 15MVA, 33/11 kilovoti | Kuongeza mashine umba 40MVA, 33/1 kilovoti |
| 19. | Ubungo | 117MVA, 132/33/11 kilovoti | Kuongeza mashine umba 120MVA, 132/33/11 kilovoti |
| 20. | Mabuki | 30MVA, 132/33 kilovoti | 120MVA, 220/33 kilovoti |
| 21. | Kasiga | 25MVA, 132/33 kilovoti | 60MVA, 132/33 kilovoti |
| 22. | Mnadani - Dodoma | 20MVA, 33/11 kilovoti | Kuongeza mashine umba 20MVA, 33/11 kilovoti |
| 23. | Zuzu - Dodoma | 10MVA, 33/11 kilovoti | Kuongeza mashine umba 20MVA, 33/11 kilovoti |
| 24. | Sabasaba - Mwanza | 10MVA, 33/11 kilovoti | Kuongeza mashine umba 20MVA, 33/11 kilovoti |
| 25. | KIA | 10MVA, 132/33 kilovoti | Kuongeza mashine umba 15MVA, 132/33 kilovoti |

Chanzo: **TANESCO**

***Kiambatisho 5A*: Leseni za Uzalishaji wa Umeme Zilizotolewa na Usajili wa Kampuni Binafsi hadi Machi, 2026**

| Na. | Jina la Mzalishaji | Aina ya Leseni | Eneo la Mradi | Uwezo (MW) |
|---|---|---|---|---|
| **I. Leseni za Muda Mrefu (zaidi ya miaka 3)** | | | | |
| 1. | Bulyanhulu Goldmining limited | Muda Mrefu (*Operational Licence*) | Mara | 40 |
| 2. | ALAF Limited | Muda Mrefu (*Operational Licence*) | Dar es Salaam | 4 |
| 3. | Buckreef Gold Company limited | Muda Mrefu (*Operational Licence*) | Geita | 4.72 |
| | **Jumla Ndogo** | | | **48.72** |
| **II. Leseni za Muda Mfupi ( Mwaka 1- 3)** | | | | |
| 4. | A TO Z Textile Mills Ltd | Muda Mfupi (*Provisional Licence*) | Arusha | 2.5 |
| 5. | Tanzania Portland Cement Public Limited Company | Muda Mfupi (*Provisional Licence*) | Dar es Salaam | 5.0 |
| 6. | Royal Soap and Detergent Industries Limited | Muda Mfupi (*Provisional Licence*) | Dar es Salaam | 2.45 |
| 7. | SSI Energy Tanzania Limited | Muda Mfupi (*Provisional Licence*) | Kahama, Shinyanga | 10.0 |
| 8. | Quality Packaging Tanzania Limited | Muda Mfupi (*Provisional Licence*) | Mkuranga, Pwani | 8.0 |
| 9. | Mwenga Hydro Limited | Muda Mfupi (*Provisional Licence*) | Mufindi | 1.6 |
| | **Jumla Ndogo** | | | **29.55** |

Chanzo**: EWURA**

***Kiambatisho Na. 5B:*** **Mikataba ya Kuuziana Umeme kati ya TANESCO na Wazalishaji Wadogo Iliyoidhinishwa na EWURA hadi Machi, 2026**

| **Na.** | **Jina la Mzalishaji** | **Eneo la Mradi** | **Chanzo** | **Uwezo (MW)** |
|---|---|---|---|---|
| 1. | TPC Limited | Moshi | Tungamotaka | 9.0 |
| 2. | Maximum Power Tanzania Limited | Rukwa | Jua | 5.0 |
| 3. | Ninety-Two Limited | Arusha | Maji | 1.9 |
| 4. | Suma Hydro Company Limited | Rungwe | Maji | 4.0 |
| **Jumla Kuu** | | | | **19.9** |

Chanzo**: EWURA**




Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Subira Mgalu ikiwa kwenye ziara katika kiwanda cha kuzalisha nguzo za zege cha TCPM kilichopo mkoani Tabora, kwa lengo la kujionea shughuli za uzalishaji zinavyoendeshwa.



Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Subira Mgalu ikiwa kwenye ziara katika kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia cha Kinyerezi I & II, kilichopo Dar es Salaam kwa lengo la kukagua maendeleo ya uzalishaji wa umeme na ufanisi wa matumizi ya gesi asilia.